# MDHIHIRIKO WA MWENDO KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI:
# MIFANO KUTOKA KATIKA DIWANI ZA *WASAKATONGE* NA *KIMBUNGA*

**PANDU MKOMBE VUAI**

**SHAHADA YA UMAHIRI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA DODOMA**

**NOVEMBA, 2020**

# MDHIHIRIKO WA MWENDO KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI:
# MIFANO KUTOKA KATIKA DIWANI ZA *WASAKATONGE* NA *KIMBUNGA*

VUAI PANDU MKOMBE

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTUNUKIWA
SHAHADA YA UMAHIRI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI
CHUO KIKUU CHA DODOMA
NOVEMBA, 2020

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, **VUAI PANDU MKOMBE**, ninathibitisha kwamba, tasinifu hii ni yangu; na kwamba, haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri au Shahada nyingine yoyote.

Tarehe:

Hairuhusiwi kuiga, kuchapisha, kutoa nakala, kutafsiri wala kusambaza sehemu yoyote ya tasinifu hii kwa namna yoyote ile bila ya kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma

## ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba, ameisoma tasinifu hii inayoitwa "**Mdhihiriko wa mwendo katika ushairi wa Kiswahili**"; **Mifano kutoka katika diwani za *Wasakatonge* na *Kimbunga*** na anapendekeza ikubaliwe kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri katika fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Dkt. Zuhura A Badru

Sahihi …………………………  Tarehe: 07/12/2020

(Msimamizi)

## SHUKURANI

Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya katika kipindi chote cha masomo yangu hadi kuikamilisha tasinifu hii katika muda uliopangwa. Pia ninawashukuru wale wote walioshirikiana na mimi mwanzo hadi mwisho wa tasinifu hii. Kwa uchache ninapenda kuwapa shukurani zangu za dhati kwa kuwataja hawa wafuatao;

Kwanza, ninapenda kumshukuru msimamizi wangu, Dkt. Zuhura A. Badru, ambaye alijikubalisha kuniongoza licha ya majukumu mengi ya kiofisi na kifamilia yaliyomkabili lakini alijitolea na kunishauri vizuri hatua kwa hatua hadi kuikamilisha kazi hii. Mwenyezi Mungu amjaaliye afya njema na umri mrefu wenye kheri ili azidi kuwatumikia na wengine.

Shukurani zangu zingine ziende kwa Dkt. Aginiwe Nelson Sanga ambaye alinivumilia na kunishauri na kuniongoza kila wakati hadi kuikamilisha tasinifu hii. Pia watafitiwa wangu wote niliofanya nao mahojiano na kushirikiana na mimi Mungu awalipe kila la kheri.

Napenda vilevile kuwashukuru wahadhiri wote waliotufundisha na waliotusimamia katika mambo mbalimbali ya kitaaluma katika kiwango hiki cha shahada ya umahiri, pamoja na wanafunzi wenzagu.

Kwa kumalizia ninapenda shukurani hizi zifike kwa familia yangu yote kwa kunivumilia kipindi chote cha masomo mbali na hali ngumu ya maisha waliokabiliana nayo.

## IKISIRI

Utafiti wa tasnifu hii ulichunguza mdhihiriko wa mwendo katika ushairi wa Kiswahili huku mifano ikitolewa katika diwani ya *Wasakatonge* na *Kimbunga* zilizotungwa na Mohammed S. Khatib na Gora Haji Gora. Mwendo katika ushairi wa Kiswahili ni kipengele cha kifani kinachotumiwa na watunzi kuboresha utunzi wa kazi za kifasihi na kudhihirisha ubingwa wa mtunzi katika kusana kazi zao. Hata hivyo, kipengele hiki cha mwedo hakijashughulikiwa sanakwa upande wa mashairi ukilinganisha na riwaya na tamthilia. Hivyo, mtafiti aliona ipo haja ya kukishughulikia.Kwa kiasi kikubwa, utafiti ulifanyika maktabani na uwandani. Data za uwandani zimepatikana kwa mahojiano ya sampuli iliyoteuliwa Data zilikusanywa katika mji wa Zanzibar. Mbinu ya maelezo ndiyo iliyotumika katika kutolea matokeo ya utafiti huu. Uchambuzi wa data umefanywa kwa kutumia nadharia ya upokezi kutokana na mihimili yake kufaa katika kubainisha aina, dhima na athari zake ukilinganisha na diwani teule na kufafanua miktadha mbalimbali inayohusiana na mwendo uliomo katika diwani hizo.

Utafiti umebaini kuwa matokeo ya utafiti yanakwenda sambamba na malengo ya tasnifu hii kwa kuonesha usawiri wa vipengele vya mwendo, dhima na athari zake. Vipengele vilivyoibuliwa ni lugha, muundo, vina, wizani, maudhui, uteuzi wa maneno, mandhari na wakati, lafudhi, taswira, kibwagizo na maghani. Kwa upande wa dhima zilizojadiliwa ni pamoja na kutia hamasa za usomaji, kuibua hisia kwa wasomaji, kupendezesha mtu kusikiliza, kumpa uhuru mtunzi, kudhihirisha matumizi ya takriri, kujenga uwezo wa kufikiri, kuibua taharuki, chanzo cha kuibua maudhui, kuweka wazi nafasi ya mahadhi, kuonesha upekee wa mwandishi, mwendo kama kipengele cha kifani. Athari zimegawika katika sehemu mbili ambazo ni athari chanya zinazotokana na mwendo wa mashairi na athari na hasi. Athari chanya zilikuwa kama kufikisha ujumbe, kuleta uvuto kwa hadhira, kuleta msisimko, na kuchochea ukuaji wa lugha. Vile vile kwa upande wa athari hasi zilikuwa ni taaluma ndogo kwa hadhira, taaluma ndogo kwa waandishi, kuichosha hadhira na kupoteza taharuki. Mwisho mchango mkubwa wa utafiti huu ulibaini kuwepo kwa mwendo wa katika uga wa ashairi na hata katika ushairi wa Kiswahili.

**YALIYOMO**

IKIRARI NA HAKIMILIKI ........................................ i
ITHIBATI YA MSIMAMIZI ........................................ ii
SHUKURANI ........................................ iii
IKISIRI ........................................ iv
YALIYOMO ........................................ v
ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ........................................ ix

**SURA YA KWANZA ........................................ 1**
**UTANGULIZI ........................................ 1**
1.1 Utangulizi ........................................ 1
1.2 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti. ........................................ 1
1.2.1 Mwendo ........................................ 1
1.2.2 Ushairi ........................................ 1
1.3.1 Historia ya Ushairi wa Kiswahili ........................................ 1
1.3.2 Historia na Maendeleo ya Ushairi wa Kiswahili ........................................ 2
1.4 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........................................ 4
1.5 Tamko la Tatizo la Utafiti ........................................ 6
1.6 Malengo ya Utafiti ........................................ 6
1.6.1 Lengo la Jumla ........................................ 6
1.6.2 Malengo Mahususi ........................................ 6
1.7 Maswali ya Utafiti ........................................ 7
1.8 Umuhimu wa Utafiti ........................................ 7
1.9 Mawanda ya Utafiti ........................................ 7
1.10 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ........................................ 8

**SURA YA PILI ........................................ 9**
**MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA ........................................ 9**
2.1 Utangulizi ........................................ 9
2.2 Historia ya Mwandishi Muhammed Seif Khatib ........................................ 9
2.2.1 Historia Fupi ya Mwandishi Haji Gora Haji ........................................ 10
2.3 Mapitio ya Maandiko ........................................ 11
2.3.1 Maandiko Kuhusu Mwendo katika Ushairi ........................................ 11

2.3.2 Mapitio ya Maandiko Kuhusu Ushairi wa Kiswahili ........................................ 13
2.4 Mwanya wa Utafiti Uliojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko.................. 15
2.5 Kiunzi cha Nadharia ........................................................................................ 15
2.6 Muhtasari wa Sura ya Pili................................................................................ 17

**SURA YA TATU ........................................................................................ 18**
**METHODOLOJIA YA UTAFITI ................................................................ 18**
3.1 Utangulizi ........................................................................................................ 18
3.2 Usanifu wa Utafiti ........................................................................................... 18
3.3 Eneo la Utafiti .................................................................................................. 19
3.4 Walengwa wa Utafiti ....................................................................................... 19
3.4.1 Wango la Watafitiwa ..................................................................................... 19
3.4.2 Mbinu ya Usampulishaji................................................................................ 20
3.5 Ukusanyaji wa Data ......................................................................................... 20
3.5.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data .................................................................. 21
3.5.1.1 Uchanganuzi wa matini ............................................................................... 21
3.5.1.2 Mahojiano.................................................................................................... 21
3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data ................................................................ 22
3.6 Uchanganuzi wa Data ...................................................................................... 22
3.7 Itikeli ya Utafiti ................................................................................................ 23
3.8 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti ...................................................... 23
3.10 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake ........................................................ 23
3.11 Muhtasari wa Sura ya Tatu............................................................................. 24

**SURA YA NNE ........................................................................................... 25**
**UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI .................... 25**
4.1 Utagulizi .......................................................................................................... 25
4.2 Vipengele Vinavyojenga Mwendo wa Mashairi katika Ushairi wa Kiswahili .... 25
4.2.1 Muhtasari wa Diwani za Wasakatonge na Kimbunga ...................................... 25
4.2.1.1 Muhtasari wa Diwani ya Wasakatonge ......................................................... 25
4.2.1.2 Muhtasari wa Diwani ya Kimbunga .............................................................. 26
4.2.2 Vipengele Vinavyojenga Mwendo wa Mashairi ............................................... 27
4.2.2.1 Lugha ........................................................................................................... 27

4.2.2.2 Muundo wa Mashairi ........ 32
4.2.2.3 Ujenzi wa Vina ........ 35
4.2.2.4 Mjengeko wa Wizani ........ 38
4.2.2.5 Ujenzi wa Maudhui ........ 39
4.2.2.6 Uteuzi wa Maneno ........ 42
4.2.2.7 Mandhari na Wakati ........ 44
4.2.2.8 Lafudhi ........ 47
4.2.2.9 Maghani ........ 48
4.2.2.10 Taswira ........ 51
4.2.2.11 Kibwagizo ........ 52
4.3 Dhima za Vipengele Vinavyojenga Mwendo wa Shairi ........ 54
4.3.1 Kufikisha Ujumbe ........ 54
4.3.2 Kutoa Hamasa katika Usomaji ........ 57
4.3.3 Kuibua Hisia kwa Wasomaji ........ 58
4.3.4 Kumpendezesha Mtu Kulisikiliza au Kusoma ........ 60
4.3.5 Mwendo Unampa Uhuru Mtunzi ........ 62
4.3.6 Kudhihirisha Matumizi ya Takriri ........ 63
4.3.7 Chanzo cha Kuibua Maudhui ........ 64
4.3.8 Kuonyesha Upekee wa Mwandishi ........ 66
4.3.9 Mwendo kama Kipengele cha Kisanaa ........ 67
4.3.10 Kujenga Uwezo wa kufikiri ........ 68
4.3.11 Kuibua taharuki ........ 70
4.4 Athari chanya za Mwendo katika Ushairi wa Kiswahili ........ 71
4.4.1 Kufikisha Ujumbe ........ 71
4.4.1.1 Huleta Mvuto kwa Hadhira ........ 73
4.4.1.2 Kuleta Msisimko kwa Washairi ........ 74
4.4.1.3 Kuchochea kwa Ukuaji wa Lugha ya Kishairi ........ 76
4.4.2 Athari Hasi za Mwendo katika Ushairi wa Kiswahili katika Diwani Teule ........ 77
4.4.2.1 Taaluma Ndogo ya Mwendo kwa Hadhira ya Shairi ........ 77
4.4.2.2 Msomaji Kuichosha Hadhira yake ........ 78
4.4.2.3 Kupoteza Taharuki kwa Wasikilizaji ........ 79
4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne ........ 80

**SURA YA TANO ........................................................................................................ 81**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ............................................ 81**
5.1 Utangulizi ........................................................................................................ 81
5.2 Muhtasari wa Tasnifu ...................................................................................... 81
5.3 Hitimisho ........................................................................................................ 82
5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika .................................................................. 82
5.3.2 Mchango Mpya wa Tasnifu Hii ............................................................................ 83
5.3.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zinazokuja .................................................................. 83
**MAREJELEO .......................................................................................................... 84**
**VIAMBATISHO ...................................................................................................... 88**

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| Dkt | Daktari |
| Khj | Kama hapo juu |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| Uk | Ukurasa |
| Bi | Bibi |
| Bw | Bwana |
| SUZA | Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Sehemu hii imehusisha mambo yafuatayo: ufafanuzi wa istilahi, historia ya ushairi wa Kiswahili, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti na muhtasari wa sura ya kwanza.

## 1.2 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti.

### 1.2.1 Mwendo

Tumaini (2010) anauzungumzia mwendo kuwa ni mtiririko wa kasi, wastani au polepole katika usomaji au uwasilishwaji wa kazi husika. Pia anaona mwendo unauhusisha mtiririko wa usimulizi wa matukio ya kazi za fasihi zikiwamo riwaya, tamthiliya na ushairi.

### 1.2.2 Ushairi

Ushairi ni sanaa yenye mpangilio maalum ya lugha ya mkato yenye ubunifu ndani yake yanayosawiri na kueleza jambo, hisi, hali au maono kwa ubunifu yenye kuvutia hisia na katika mpangilio wa sauti wenye kuongozwa na mizani (Mulokozi, 2017).

### 1.3.1 Historia ya Ushairi wa Kiswahili

Kama inavyotambulika ushairi wa Kiswahili ulianza kabla ya karne ya kumi kutokana na ushairi wa kibantu (Mulokozi, 2007) anendelea kusema ushairi huu uliathiriwa na maandishi (hati za kiarabu) na kutumika kikamilifu wakati huo kulingana na jamii za wakati huo. Tungo nyingi za kidini na za kidunia zilihifadhiwa kwa wingi maandishi yake hasa karne ya 16. Ilipofika karne ya 18 - 20 ushairi ulienea zaidi kutokana na kufundishwa maskulini kwa kutumia hati za kirumi na uchapishwaji vitabu, vipeperushi na vitabu mbalimbali.

Kuanzia karne ya 16 ushairi wa Kiswahili umekuwa ni suala telezi ambalo limezua mjadala mkubwa kwa muda sasa katika sehemu nyingi hasa katika makongamano yanayohusu ushairi. Mjadala mkubwa ulikuwa kuhusu kupewa maana ya ushairi (Ndungo & Mwai, 1991). Kuwepo kwa harakati kadhaa za kufasili dhana ya ushairi wa Kiswahili kumewagawa wataalamu wa fani ya ushairi katika matapo makuu mawili yaani tapo la wanamapokeo na wanausasa (Sengo, 1978; Senkoro, 1988;

Sanka, 1995). Katika kutoa fasili kila tapo limetoa fasili yake kuhusiana na dhana ya ushairi wa Kiswahili, wataalamu wa tapo la wanamapokeo walikuwa (Robert, 1958; Mayoka, 1986; Mnyampala 1970; Abdalla, 1973), wote wamefasili dhana ya ushairi wa Kiswahili huku wakiunga mkono urari wa vina na mizani kuwa ni nguzo muhimu katika utungaji wa mashairi ya Kiswahili. Kwa jumla, wanamapokeo wanauona ushairi kuwa ni wimbo, wenye maneno ya hekima, wenye lugha ya mkato, wenye urari wa mizani na vina na wenye hisia (unagusa moyo). Na kwa upande wa tapo la wanausasa, mfanoTopan (1974) Kezilahabi (1976) Mulokozi na Kahigi (1982) na Senkoro (1988), limetoa ufafanuzi kuhusiana na ushairi wa Kiswahili lakini tapo hili hawakulitilia maanani suali la urari wa vina na mizani.wataalam hawa wanatoa maana ya ushairi kama ushairi ni sanaa inayopagwa kwa mpangilio maalum wa maneno fasaha na yenye muala, kwa lugha ya mkato, picha, sitiari au ishara, kwa kutumia maandishi au mahadhi wa wimbo ili kuleta wazo la kufunza au kueleza tukio fulani kuhusu maisha ya binadamu kwa njia inayogusa moyo (Molokozi & Kahigi, 1982).

### 1.3.2 Historia na Maendeleo ya Ushairi wa Kiswahili

Ushairi wa Kiswahili ulianza katika umbo la fasihi simulizi na kutambulika kuwa ulikuwapo mara tu baada ya lugha ya Kiswahili ilipoanza kutumika. Mulokozi na Sengo (1995) wanasema, si rahisi kueleza ni lini ushairi simulizi wa Waswahili uliibuka. Ushairi wa Kiswahili ni fani kongwe kama kiumbe mwanadamu alivyo mkongwe hapa duniani (Maitaria, 2017). Na wataalamu wa sanaa ya mashairi ya Kiswahili walikuwepo kwa muda mrefu kabla ya lugha ya Kiswahili haijaenea kama inavyoonekana hivi leo. Wakati huo mashairi yalijuulikana kwa majina ya mashairi ya Kipemba, Kivumba, Kimvita, Kipate na mengineyo, hii ni kutokana na jamii ya Waswahili wa wakati huo wakitumia lahaja zenye mlingano na mashairi hayo. Kwa ushairi andishi wa Kiswahili, si rahisi kusema ni lini hasa uliibuka. Hali hii ilisababisha wataalamu wa arudhi ya Kiswahili kutofautiana kimtazamo kuhusiana na jambo hilo. Knappert (1979) aliona ushairi andishi wa mwanzo wa Kiswahili ni utendi wa *Hamziyya* ulioandikwa mwaka (1652). Wakati huo huo, Harries (1962) anatanabahisha kuwa ushairi andishi wa mwanzo wa Kiswahili ni utendi wa *Tambuka* ulioandikwa (1728). Hata hivyo, utafiti wa Mulokozi na Sengo (1995) umebainisha kuwa wataalamu wote wawili (Knappert na Harries) wana kasoro katika

mawazo yao kuhusiana na ushairi andishi wa mwanzo wa Kiswahili. Mulokozi na Sengo wanaona ushairi wa mwanzo wa Kiswahili ni "*Kumswifu Yunga*" unaonasibishwa kutungwa na Fumo Liyongo huko Pate. Wanaendelea kwa kusema fani ushairi iliibuka kutoka na jamii ya Waswahili wenyewe, kwani fani hiyo inawiyana na umri wa Waswahili hao. Wakati huo huo, fani ya ushairi imeonyesha matumizi mengi katika kazi zao za kuwasilianana burudani katika maisha yao. Shariff (1988) amezitaja sanaa kama vile, uchongaji, ususi, uchoraji, ufinyazi, ngoma na muziki, sanaa zote hizo hazijafikia ubora wautngaji kwa Waswahili wenyewe. Hivyo, inadhihirika wazi kuwa Waswahili ni wapenzi wa tungo kwa matumizi yao ya kawaida. Kwa upande mwengine ushairi umeshughulikiwa na wataalamu kadhaa, wakiwemo wataalam wa ndani na wa nje. Mfano wataalam wa nje ni W. Hichens, J. Knappert, J. W.T. Allen, na wengineo na wataalamu wenyeji mfano Kaluta. A. Abedi, S. Chiraghdin, E. Kezilahabi, A. G. Gibbe, Sengo, M. M. Mulokozi, Saadan. A. Kandoro na wengi wengineo.

Katika kuangaza asili ya ushairi wa Kiswahili, wataalamu wa arudhi ya Kiswahili wamekubaliana kuwa chimbuko la ushairi wa Kiswahili ni nyimbo zinazofungamana na ngoma (Edwin, 2006; Khatib, 2014; Mulokozi, 2017) na wenginezo. Nyimbo hizo ziliimbwa katika shughuli za harusi, kilimo, uvuvi, uwindaji, unyago na jando na kadhalika. Nyimbo nyimgine ziliimbwa wakati wa jioni baada ya shughuli za mchana kutwa kwa lengo la kuwaliwaza na kuwapumzisha. Pia tungo hizo zililenga kutoa hisia za jamii na kuweka wazi maendeleo ya jamii zao.

Upande wa kifasihi, Kezilahabi (1983) ameainisha mihula minne ya ambavyo ni muhula wa urasimi (1885) ambao kanuni zake za utunzi wa ushairi zilitawaliwa zaidi na itikadi za kidini na umwinyi. Kwa mfano *Utenzi wa Tambuka* (1728), *Utenzi wa Hamziyya* (1690), *Utenzi wa Al-Inkishafi* (1810-1820) na *Utenzi wa Mwanakupona* (1858). Muhula wa utasa (1885-1945) ni kipindi cha mabadiliko ya kiutawala na kielimu na kupelekea kuibuka kwa hati ya maandishi. Kipindi cha urasimi mpya (1945-60), kipindi kilichojikita katika ufufuaji wa kanuni za utunzi na kuzieneza kila sehemu ndani na nje ya nchi. Hii iliibua wasanii chipukizi wa ushairi, kwa mfano, Mathias Mnyampala, Ahmad Nassir, Khamis Amani Nyamaume na wengineo. Harakati zilipeleke kushamiri kwa utunzi wa vitabu vya mashairi kulingana na

kufuata kitabu cha *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* Sheikh K. A. Abedi kilichotumika kama kiungo muhimu kwa wakati huo hadi sasa.

Muhula wa sasa (1967) ni muhula wa kimambo leo wenye mtazamo mpya kimawazo na kisanaa. Hiki ni kipindi kilichoibua mgogoro wa ushairi wakati washairi walipokuwa wanatafuta uhuru wa kisanaa. Lakini pamoja na mgogoro huo yalifikiwa makubaliano ya pamoja kati ya wana usasa na wanamapokeo kama vile ushairi uwe na kauli zenye hisi na ubunifu, mpangilio wa vina na mizani (*metrical system*), uwasilishaji makini (*experience*) na lugha ya picha yenye wizani mzuri wa sauti (Mulokozi, 2007).

Kwa jumla, maandiko kuhusu historia ya ushairi wa Kiswahili yamemsaidia mtafiti kuweza kufahamu mapito mbalimbali ya kihistoria ambayo fani anayoifanyia kazi.

**1.4 Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Ushairi wa Kiswahili ni fani inayosonga mbele kila uchao. Hali hii inatokana na maendeleo yanayoibuka katika masuala ya uchumi, jamii, siasa na utamaduni. Maendeleo hayo yamesababisha kuibuka kwa mabadiliko katika sayansi na tekinolojia na kuufanya ushairi kubadilika kiumbo na kimaudhui (Wamitila, 2008). Hata hivyo, mbali na mabadiliko yaliyotokea bado ushairi unatajwa kuwa ni mgumu ukilinganishwa na riwaya pamoja na tamthiliya. Mawazo hayo yanaungwa mkono na Senkoro (1988), ambaye anauona ugumu wa kueleweka kwa ushairi unasababishwa na matumizi mengi ya lugha nzito, picha na mkato, tamathali za semi, methali na mbinu nyingine za kisanaa. Kutokana na ugumu unaojitokeza katika ushairi bado wajuzi wa fasihi na wataalamu wa lugha, hawajakata tamaa na ugumu huo katika tafiti zao ambazo zimeweza kuibua vipengele mbalimbali vya kifasihi kikiwemo kipengele cha mwendo katika kazi za fasihi. Mbali na kuwa kuna tofauti ya kudhihirika kwa mwendo baina ya ushairi na kazi nyingine za fasihi bado mwendo ni kipengele cha msingi katika kuielewa kazi ya fasihi, hususani utanzu wa ushairi. Kipengele cha mwendo tulikigundua kupitia maandishi ya wataalamu na wahakiki mbalimbali wa riwaya na tamthiliya waliopita, kwa mfano (Tumaini, 2010). Hapa mtafiti lilimjia wazo na kukichunguza kipengele hiki cha mwendo katika ushairi kutokana na upekee katika sanaa ya ushairi. Tumaini (2010) anauzungumzia mwendo kuwa ni mtiririko wa kasi, wastani au polepole katika usomaji au

uwasilishwaji wa kazi husika. Mwendo wa shairi unauhusisha mtiririko wa usimulizi wa matukio ya kazi za fasihi zikiwemo riwaya, tamthiliya na ushairi. Hivyo, suala la mwendo hubeba dhima, athari za usomaji na msomaji wakati wa kutafuta ujumbe husika. Hii hufanyika kutokana na kwamba mwendo katika ushairi hujengeka kulingana na lugha kuwa (ngumu, wastani au nyepesi), mshindilio wa utongoaji wa kisa (kurusha au kutongoa kila kitu), aina ya maudhui yanayoshabihiana na wakati na mahali. Hivyo kupitia vipengele vilivyopo hapo juu msomaji wa mashairi husika huweza kung'amua mwendo wa kazi husika. Mtaalamu huyo anaendelea kuonyesha wazi aina za mwendo katika ushairi kama zifuatavyo:

Mwendo wa kasi: Huu ni mwendo unaoangazia zaidi kufanyika kwa matukio ya kasi ambayo yanasababisha ugumu katika uwelewaji wa maudhui kwa kina. Hii ni kutokana na muda, wakati na matukio katika uwasilishwaji. Maudhui yake hurushwa kwa mshindilio hafifu pamoja na matumizi ya lugha rahisi na ya moja kwa moja. Pia katika kusana maudhui ya kazi za aina hizi za mwendo wa kasi maudhui yake huwa ya kufurahisha na kusisimua. Sifa za mwendo wa kasi huishia kwa kutaja majina tu ya maeneo au sehemu kulingana na mandhari iliyotumika katika andiko husika. Kazi nyingi za kifasihi za kimapenzi hutungwa kwa kusisimua na kwa kuhusisha matukio ambayo yanaendeshwa kwa haraka mno hadi kufikia wakati msomaji kujiuliza maswali mengi.Vilevile mwendo huu huwa matukio yake hayajirejei bali huwa ya moja kwa moja. Kwa kifupi aina hii ya mwendo hushughulikia suala la usomwaji na usikilizaji wa kazi za fasihi ili kufikisha ujumbe.

Mwendo wa wastani: Kazi zenye mwendo huu huwa na dhamira za mseto, kwa maana kusisimua na kuhuzunisha husanwa kwa wakati mmoja. Mwendo huu huchanganya dhamira za kitanzia na za kufurahisha, usomaji na uwasilishaji hutumia muda wa wastani katika dhamira moja. Sifa za mwendo wa wastani ni pamoja na kwamba wasomaji na wasikilizaji hupata ujumbe husika kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na mwendo wa kasi

Mwisho mwendo wa polepole: Mwendo huu kazi zake husanwa kwa maudhui ya kitanzia (kuhuzunisha), kutisha na kuogofya. Aghalabu mwendo huu hujumuisha wakati na masafa ya kijografia kwa "kasi" ya polepole. Kwa mfano kazi zilizosanwa kipindi cha kudai uhuru, kipindi cha machafuko ya kisiasa na kipindi cha njaa na

maradhi husanwa matukio yake kitanzia. Hivyo usomaji wa shairi huwa wa taratibu mno. Sifa ya mwendo huwa wa taratibu ili kujenga uelewa wa ujumbe husika. Kazi zilizotungwa kwa mwendo wa polepole huwachosha wasomaji au kuambulia patupu kwani baadhi ya wasanii hutumia lugha ya ishara na lugha ngumu katika ubunifu wa kazi zao (Tumaini, 2010).

### 1.5 Tamko la Tatizo la Utafiti

Mwendo wa ushairi ni kipengele cha kifani ambacho watunzi wanakitumia katika kazi zao ili kutimiza malengo ya kile walichokikusudia kukiwasilisha kwa hadhira zao, kwa mfano kuleta furaha au majonzi au vyote viwili. Kwa kawaida washairi wamekuwa na uelewa wa kipekee ambao umesababisha kuibua vipengele vipya katika kazi zao ili kuuboresha ushairi wa Kiswahili. Katika jitihada za kuibua vipengele kimeibuka kipengele kipya cha mwendo katika kazi zao. Hata hivyo, kipengele hiki cha mwendo bado hakijashughulikiwa kwa kina kwa upande wa ushairi hasa ikilinganishwa na riwaya na tamthiliya. Hii imedhihirika kwa baadhi ya watafiti walioandikia mwendo kwa upande wa riwaya na tamthiliya chambilecho (Tumaini, 2010; Sangili, 2014). Kutochunguzwa kwa mwendo wa ushairi kuna athari kubwa kwa wasomaji katika kujenga uelewa, na kujisomea kikasuku na kusababisha kushindwa kung’amua aina ya mwendo hasa unaohitajika kulingana na kisa husika. Katika kuziba pengo hilo mtafiti amechunguza mwendo wa ushairi wa Kiswahili kama unavyodhihirika katika vitabu vya *Wasakatonge* na *Kimbunga*, ili kuweka wazi mambo mbalimbali yanayohusiana na mwendo katika diwani hizo kwa kuonyesha vipengele vinavyojenga mwendo wa ushairi, dhima za mwendo na namna vinanvyoathiri usomaji na uelewa wa hadhira wa diwani teule.

### 1.6 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na malengo ya aina mbili, nayo ni lengo la jumla la utafiti na malengo mahususi ya utafiti.

#### 1.6.1 Lengo la Jumla

Lengo la jumla ni kuchunguza mdhihiriko wa mwendo wa mashairi katika ushairi wa Kiswahili kwa kutumia diwani teule za *Wasakatonge* na *Kimbunga*.

#### 1.6.2 Malengo Mahususi

Malengo yaliyotimizwa ni haya yafuatayo:

a) Kubainisha vipengele vinavyojenga mwendo katika mashairi ya *Wasakatonge* na *Kimbunga*.

*b)* Kufafanua dhima ya vipengele vinavyojenga mwendo katika mashairi *ya Wasakatonge* na *Kimbunga*.

*c)* Kutathmini athari za mwendo katika ushairi wa Kiswahili.

**1.7 Maswali ya Utafiti**

a) Je, ni vipengele vipi vinavyojenga mwendo wa mashairi katika ushairi wa Kiswahili?

b) Je, vipengele vinavyojenga mwendo katika mashairi ya *Wasakatonge* na *Kimbunga* vina dhima zipi?

c) Je, mwendo wa mashairi una athari zipi katika ushairi wa Kiswahili?

**1.8 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti ulikuwa na manufaa mbalimbali kama yafuatazo: Mosi, utajirishaji wa nadharia ya ushairi wa Kiswahili kwa kuongeza kipengele cha mwendo kama kigezo kimojawapo cha uhakiki wa ushairi.

Pili, utafiti huu utatumika kama rejeleo kwa wanataaluma na wahakiki wa ushairi, hasa ikizingatiwa kuwa marejeleo yanayohusu mwendo katika ushairi ni machache. Tatu, utafiti unaibua mijadala kadhaa ya kitaaluma ambayo itatoa hamasa kwa watafiti wengine kushajihika kutafiti mwendo wa ushairi. Nne, utafiti umekuza machapisho kadhaa yanayozungumzia mwendo wa ushairi na hivyo kukuza taaluma ya ushairi na washairi. Tano, kuutambulisha mwendo wa ushairi kwa baadhi ya waandishi na hadhira yao pamoja na wanafasihi wengine na jinsi unavyoathiri utunzi wao na kukuza ufahamu wa fasihi ya Kiswahili. Sita, kuwasaidia wasomaji wa kazi za fasihi kuufahamu mwendo uliomo ndani ya kazi za fasihi hususani ushairi ili kusoma kwa mujibu wa mwendo husika na kuweza kung'amua kwa wepesi maudhui yaliyokusudiwa

**1.9 Mawanda ya Utafiti**

Utafiti umechunguza mwendo wa ushairi kama ulivyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili. Lengo ni kuchunguza mwendo wa mashairi katika ushairi wa Kiswahili kwa kutumia diwani za *Wasakatonge* na *Kimbunga*. Mtafiti ametumia diwani alizozichagua kwa sababu ya upekee unaolingana na mada. Pia mtafiti amechunguza

msuko wa matukio kwa kuona kuwa umekidhi upatikanaji wa mwendo wa mashairi, ambayo ndio haja ya utafiti ikilinganishwa na diwani nyingine. Utafiti huu umechunguza mwendo wa mashairi katika diwani za *Wasakatonge* na *Kimbunga* tu na si nyingine isipokuwa kazi nyingine za fasihi kama vile riwaya na tamthiliya zimehusishwa kwa sehemu ndogo ili kuongeza uelewa tu.

### 1.10 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii imehusisha ufafanuzi wa vipengele vya usuli wa tatizo, kwa ufupi imeeleza tatizo lililomsukuma mtafiti kuamua kuichunguza mada hii na kuiundia malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mawanda ya utafiti. Sura inayofuata ni sura ya pili, ambayo inahusu mapitio ya maandiko tangulizi na kiunzi cha nadharia kilichotumika kuongoza utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura imeanza na maelezo mafupi ya historia za waandishi wa diwani teule. Vilevile sura iliangalia maandiko yanayohusu mwendo katika ushairi na ushairi wa Kiswahili. Sehemu inaangalia mwanya uliojitokeza kutokana na mapitio ya maandishi na mwisho imefafanua kiunzi cha nadharia iliyotumika katika kupata mawazo ambayo yamemsaidia mtafiti katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Sura imemalizia kwa muhtasari wa sura nzima

## 2.2 Historia ya Mwandishi Muhammed Seif Khatib

Utafiti umechunguza mdhihiriko wa mwendo katika ushairi wa Kiswahili na mtafiti ametumia *Wasakatonge* miongoni mwa diwani za mwandishi Khatib. Mtafiti ameona ni busara amueleze mwandishi huyu historia ya maisha yake kuanzia kuzaliwa kwake, elimu yake, nyadhifa zake serikalini na kazi zake za kisanaa. Msokile (1991) kupitia tahakiki na maelezo ya wachapishaji wa diwani za mashairi ya *Fungate ya Uhuru* (2007) *na Wasakatonge* (2012), anamuelezea kuwa Khatib alizaliwa mwaka wa 1951 katika kijiji cha Umbuji Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja. Khatib alibarikiwa kupata elimu ya msingi na sekondari. Khatibu alisomea Ualimu katika Chuo cha Ualimu kilichopo Nkrumah nje kidogo mwa mji wa Zanzibar. Baada ya kupata elimu hiyo, aliajiriwa kufundisha katika shule za msingi na sekondari na baadaye Chuo Cha Ualimu Nkrumah Zanzibar. Pia alifundisha katika Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar (1975).

Khatib aliamua kujiendeleza kielimu na alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuhitimu shahada ya kwanza ya (B.A. Ed) ya lugha ya Kiswahili na Fasihi (1978). Mwaka (1982) Khatib alihitimu shahada ya pili ya uzamili (M.A) Chuo Kikuu cha London (SOAS). Mwaka (2011) alitunukiwa shahada nyingine ya uzamivu Chuo Kikuu cha Dodoma.

Katika mawanda ya uandishi aliogolea uga wa ushairi ambapo aliandika kazi za mashairi kadhaa na kuchapishwa zikiwemo *Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar (1975), Pambazuko la Afrika (1982) na Taarab Zanzibar* (1992), *Fungate ya uhuru*

*(2007)*, na *Wasakatonge* (2003) ambayo ndiyo mtafiti ameichagua na kuifanyia kazi yake ya utafiti.

Mwandishi mbali ya kuwa malenga amewahi kushika nyadhifa kadhaa serikalini kama uwaziri, ubunge wa jimbo la Uzini Zanzibar na nyinginezo hadi sasa.

### 2.2.1 Historia Fupi ya Mwandishi Haji Gora Haji

Haji Gora Haji alizaliwa mwaka wa 1933 katika kisiwa kidogo cha Tumbatu kiitwacho Kokoni, Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Kaskazini (A) Unguja. Kisiwa kinakisiwa urefu wa kilomita saba kutoka kaskazini hadi kusini na upana unakadiriwa kilomita moja na nusu wenye mwinuko kiasi kutoka usawa wa bahari (Khamis na Omar, 1994). Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo na uvuvi. Gora alijishughulisha na mambo ya uvuvi, kufanya kazi majahazini, na ukuli. Tumbatu imegawika sehemu mbili, sehemu kusini na ya katikati. Sehemu ya upande wa kusini ambako kinapatikana kijiji cha Jongowe. Sehemu ya katikati kijiji cha Kichangani, chenye shehia mbili za Gomani na Uvivini.

Kwa upande wa familia, Gora alizaliwa shehia ya Gomani katika familia ya watoto sita wa mama na baba mmoja. Pia, anao ndugu wanne wa baba tu. Bw. Gora alipata elimu yake ya Qur-an Mjini Zanzibar katika chou cha Bi Mwana-darini kilichopo maeneo ya Vuga. Baadaye alirudi Tumbatu na kusoma kwa mwalimu Ibrahim Juma. Haji Gora hakuwahi kusoma skuli, lakini alijiendeleza hadi kufikia kiwango cha kujua kusoma na kuandika.

Kwa upande wa ndoa, Gora alioa miaka ya (50), na alibahatika kuoa wake watano, nao ni Bi Mrisho Pandu, Bi Bahati Makame, Bi Seoja Musa, Bi Miza Ngwali na Bi Patima Pandu. Wake wote amezaa nao, isipokuwa Bi Seoja Mussa. Haji Gora amefanikiwa kuzaa watoto kumi na saba. Wanawake sita na wanaume wanane. Wanawake shughuli zao kubwa ilikuwa kutunza nyumba, yaani mama wa nyumbani; wakati wanaume wanafanya kazi katika sekta tofauti za serikali pamoja na kumsaidia baba yao shughuli zake za uandishi.

Haji Gora alianza utungaji akiwa kijana mdogo huko kwao Tumbatu kwa kuanza na utungaji wa nyimbo katika kikundi maarufu cha ngoma kiitwacho Zige kwa wakati huo, na alitunga nyimbo za malumbano kwa kujibizana na waimbaji wenziwe

waliokuwa wakiimba katika vikundi vingine kama vile kaza roho. Mnamo mwaka (1957), Haji Gora alihama rasmiTumbatu na kwenda Mjini Unguja ambako alijiunga na vikundi vya taarabu asilia kama vile Klabu ya taarabu ya Mlandege, na Klabu ya Michezani.

## 2.3 Mapitio ya Maandiko

Katika mapitio ya maandiko tumemakinikia maandiko yanayohusiana na mada ya utafiti. Maandiko hayo ni yale yanayohusisha mwendo wa mashairi katika ushairi wa Kiswahili.Vilevile, tumebainisha mapengo yanayojitokeza kutoka katika maandiko hayo.

### 2.3.1 Maandiko Kuhusu Mwendo katika Ushairi

Ili kuweza kuuchambua mwendo katika mashairi hapana budi kuvizingatia baadhi ya vipengele kwa kina kama vile kiimbo, mapigo (*rhythm*) na mita (*metre*) ambavyo vitatoa mwanga kuhusu ufanyikaji wa mwendo katika mashairi kama vifuatavyo:

Massamba, na wenzake (2004), wanasema kuwa kiimbo ni mfumo wa sauti zinazotolewa kwa mpango maalum wa mpando na mshuko wa sauti wakati wa usemaji. Msemaji anaweza kupandisha sauti au kushusha kulingana na tukio husika, wanaendelea kusema kuwa kila lugha imejengwa utaratibu maalum wa upandaji na ushukaji wa sauti wakati wa utamkaji. Wakati huo huo dhana ya kiimbo hufuatana na dhana ya kidatu. Kidatu ni sauti inayotolewa wakati wa utamkaji wa juu, katikati, au wa chini unaosababishwa na namna mtu anavyokitamka kitu. Hivyo, anaweza kupandisha sauti, kiwango cha sauti anachokitaka kama kiwango cha juu, kati, au cha chini. Hii ina maana kwamba mpando na mshuko unafuatana na mahadhi yanayotolewa na mtu wakati wa utamkaji. Utamkaji huo hutafautiana baina ya mtu mmoja na mwingine kimwendo hivyo kila mtu huwa na mwendo wake wakati wa ughanaji wa shairi. Andiko hili limenufaisha utafiti kwani limempa uwezo wa kuelewa upandaji na ushukaji wa sauti, sauti huundiwa viwango (vya juu, kati na chini) ambavyo hutoa mahadhi yanayoonesha aina za mwendo zinazoweza kutofautisha baina ya mtu mmoja na mwingine wakati wa kusoma shairi na dhima za mwendo huo na kwa namna gani huathiri hadhira wakati wa kusikiliza shairi.

Mizani ni mpangilio maalum wa sauti zinazosisitizwa na zisizosisitizwa katika maneno yaliomo katika ubeti. Silabi zinazosisitizwa aghalabu huwa ndefu mfano neno angalizo (nga) hii ni silabi nzito yenye kusisitizwa na huwa ndefu, silabi isiyosisitizwa huwa laini na nyepesi katika kutamka kwa mfano neno wangapi silabi (wa) ni silabi isiosisitizwa (Ross, 1979). Mizani humsaidia mwandishi wa shairi kutunga shairi lenye kuimbika. Vilevile, andiko lilimsaidia kufahamu matumizi mapigo ya sauti za lugha kupitia mizani ambazo zilitumika kupima aina za mwendo na vipi mwendo unajitokeza kwa kupitia mkazo wa sauti za mizani.

Msokile (1993) anauona mwendo ni mapigo ya sauti za lugha zilizojengwa ili kuleta mapigo ya sauti fulani kwa lugha husika. Msokile anaamini kila lugha ina mapigo yake. Kwa mfano, mapigo ya lugha yakifuatanishwa vizuri hujenga mwendo ambao utatoa maana fulani yenye mvuto wakati wa kusomwa shairi. Msokile anaona kuwa mwendo katika ushairi unapatikana katika mapigo ya lugha (ridhimu) ambayo ndio yanayojenga uelewa wakati wa kusoma, kuimba au kughani. Hivyo, andiko hili limemnufaisha mtafiti kumpatia uelewa kuwa mwendo unaweza kujengwa na mapigo ya lugha kwa kupitia ridhimu ambazo ndizo zinazotoa aina ya mwendo, dhima na athari za mwendo huibuka kutokana na msomaji kumudu matumizi ya ridhimu ya shairi husika. Andiko limegusia vipengele vinavyojenga mwendo kwa mfano ridhimu (wizani), lugha na mapigo ya sauti lakini bado vipengele vingine vimeongezwa na utafiti huu.

Massamba (1983) anaona kuwa muunganiko wa vina au silabi ya kati na ya mwisho hutoa mapigo katika shairi. Mapigo hayo kazi yake kubwa ni kujenga urudiaji wa mshindio ambao msomaji anatakiwa kuupata ili kufikia ujumbe husika. Andiko hili limemsaidia mtafiti kujua aina ya mwendo, kipengele cha vina kinachojenga mwendo wa ushairi namna kinavyotumika wakati wa urudiaji wa vina hivyo, hujenga mwendo wa ushairi na kuonesha dhima ya kufikisha ujumbe. Athari hujichomoza wakati wa matumizi ya vina hivyo ambazo huathiri uelewa wa hadhira kwa hasi au chanya.

Kezilahabi (1975) amezungumzia mwendo kuwa ni mapigo (*rhythm*) katika shairi ijapokuwa si lazima mapigo yafanane kila mstari wa shairi. Lakini mapigo anayozungumzia Kezilahabi ni sauti ambayo huitwa mizani. Katika kuzungumzia

mwendo wa ushairi anasema shairi linalohusiana na msiba au huzuni mapigo ya mwendo wa shairi huwa yanawiana na tukio hilo. Kwa mfano shairi linalohusu mapenzi au furaha bila shaka mwendo wake utakuwa wa haraka na kinyume yake shairi linalohusu mauaji, ugomvi huwa na mwendo wa pole. Vilevile mapigo ya wizani hutumika kubainisha mpangilio wa silabi ambazo hujenga mstari wa shairi au hata shairi zima. Hivyo, andiko limemsaidia mtafiti kupata kufahamu kipengele cha mwendo (rhythm) na namna kilivyojenga mwendo wa ushairi kwa kupitia mapigo ya wizani na aina ya maudhui husika kwa kupata aina za mwendo kwa mfano mwendo wa polepole ambao hujengwa kwa dhamira za huzuni na majonzi hujengwa mizani nzito na mwendo wa kasi husanwa na mashairi ya mapenzi na furaha aghalabu huwa wizani laini.

Madumulla (2009) ameeleza kipengele cha mwendo kwa kukiingiza katika masimulizi. Masimulizi hueleza namna ambavyo usimulizi una~~vyo~~fanyika wakati wa kulieleza tukio katika kazi ya fasihi. Hivyo, msomaji hupata ujumbe unaokusudiwa wakati wa usomaji au usikilizaji wake. Masimulizi ndiyo yanayojumuisha uchomozi wa aina ya mwendo ndani yake, hasa msomaji au msikilizaji wakiwa na taaluma fulani kwa kile kinachohadithiwa. Andiko limeeleza usimulizi wa matukio kama kipengele cha kujenga mwendo kwani ili mwendo wa shairi uibuke lazima pawepo maandiko ya masimulizi. Usimulizi huu umemsaidia mtafiti kupata kipengele kinachojenga mwendo kwa mfano maudhui ya shairi (masimulizi), dhima za mwendo kufikisha ujumbe ingawaje katika ushairi usimulizi hauko kwa kiasi kikubwa lakini bado umempa mwanga mtafiti kupata kujua dhima na athari anazozipata msomaji wakati wa usomaji kwa kuhusisha na mwendo wa ushairi.

### 2.3.2 Mapitio ya Maandiko Kuhusu Ushairi wa Kiswahili

Mulokozi na Kahigi (1982) wanasema ushairi ni sanaa iliopamgwa kwa utaratibu maalum, ndani yake mkiwa na lugha za tamathali, ufasaha wa lugha, muwala na mtiririko wa lugha za picha na ishara. Mtunzi hutunga kazi yake ili kueleza wazo alilolikusudia kwa lengo la kufikisha ujumbe. Andiko hili limemnufaisha mtafiti katika kufahamu aina za mwendo. Kuwepo muala na matumizi ya lugha ufasaha, ishara na tamathali za semi hizi zimesaidia katika utafiti huu. Kwani vipengele kama lugha, taswira (ishara) vilitumika katika kuujenga mwendo wa shairi. Mtafiti

amegundua dhima ya ufikaji wa ujumbe kwa harakaharaka au polepole kulingana lugha na wazo alilolitumia mwandishi

Massamba (1983) anahusisha shairi kama nyimbo za kumliwaza msomaji au msikilizaji kwa kutumia mpangilio wa lugha fasaha, mapigo ya vina na mizani na lugha nzito hutumiwa ili kuwafanya wasomaji wasahau machungu na majaribu waliyokutana nayo na kujisikia wapo huru maishani. Andiko hili limemnufaisha mtafiti kupata kujua vipengele vya mwendo kama lugha, mizani na vina katika kufakisha malengo aliojiwekea katika kutambua vipengele hivyo. Pia mtafiti alifahamu dhima ya kumfikirisha msomaji na msikilizaji ili kusahau machungu na kujisikia yupo huru na athari zinazotokana na vipengele hivyo kufikisha ujumbe na burudani.

Wamitila (2010) anasema ushairi ni fani inayopangwa kwa kutumia utaratibu malum wa kishairi unaohusisha mdundo wa sauti, mpangilio wa mizani pamoja na matumizi mengine ya lugha. Ni mpangilio ambao mtunzi hupanga sentensi zenye vina vinavyotoa mdundo akimaanisha mwendo wa ushairi huku ukichanganya lugha ya mkato na ya mafumbo. Andiko limemnufaisha mtafiti kutumia mpangilio wa mdundo wa wizani, mafumbo, vifungu vya maneno na lugha ya mkato kama ni vipengele vinavyojenga aina ya mwendo wa ushairi na kutoa dhima ya kumsisimua msomaji au msikilizaji wakati wa kufikisha ujumbe vipi unavyomuathiri msomaji au msikilizaji kupitia vitu hivyo.

Abdillatif (1973) anaeleza ushairi kuwa ni mpangilio madhubuti uliosanwa kwa umbile la kishairi lenye matumizi mazuri ya ufasaha wa maneno yenye hekima yaliyounganishwa na lugha ya mkato inyomuwezesha mtumiaji kuitumia wakati wa utumbuizi. Vipengele ilivyotajwa hapo juu kwa mfano ufasaha wa maneno, lugha ya mkato ni vimetumika katika utafiti huu. Na vimemsaidia mtafiti kutambua  aina ya mwendo na kupima kasi ya mwendo katika ushairi na vipi huathiri uelewa kutokana na matumizi ya mahadhi hayo, pia aina za lugha aliyoitumia mfano lugha nzito, ya mkato na laini ni miongoni wa vipengele vinavojenga mwendo wa shairi.

## 2.4 Mwanya wa Utafiti Uliojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko

Ni wazi kwamba, maandiko tuliyoyachambua yamejikita katika maeneo maalum yanayohusiana kwa namna moja au nyingine na dhana ya mwendo. Kutokana na mpangilio wa malengo ya utafiti ni wazi kuwa yalijitosheleza kulingana na makusudio ya utafiti. Hata hivyo, mapitio ya maandiko hayo yamedhihirisha kuwa, dhana ya mwendo wa mashairi katika fasihi ya Kiswahili bado haijatafitiwa vya kutosha, mbali na dhana hii kutumiwa ndani ya ushairi na kuwaathiri wasomaji na wasikilizaji wa kazi za fasihi. Kutokana na hayo, wataalamu kadhaa wameandika kuhusu kipengele cha mwendo; kwa mfano Tumaini (2010) ambaye hata hivyo ameandika kwa uchache hasa kwa upande wa ushairi wa Kiswahili ukilinganisha na maandiko ya nathari. Hata hivyo, kutotambuliwa vizuri kwa mwendo wa ushairi hadi sasa, kumemfanya mtafiti kugundua mianya ifuatayo: Kwanza kutodhihirishwa wazi mwendo wa mashairi katika wigo wa ushairi. Kutofanyiwa tafiti za kutosha ili kufahamu dhima za mwendo, athari zake wakati wa uelewa wa mashairi na matumizi ya mwendo yanavyojichomoza katika ushairi wa Kiswahili. Hivyo mtafiti ameona ipo haja ya kufanya utafiti ili kuuchunguza mwendo katika ushairi ili kuziba mwanya uliojichomoza kwa kuchunguza yafuatayo: Mosi, mtafiti amefafanua vipengele vinavyojenga mwendo wa mashairi katika ushairi wa Kiswahili, pia aliainisha dhima mbalimbali ya mwendo wa mashairi katika ushairi wa Kiswahili na mwisho amefafanua athari za mwendo wa mashairi katika uelewekaji wa ushairi katika ushairi wa Kiswahili. Hivyo, mtafiti ameliziba pengo hili kwa kuchunguza mdhihiriko wa mwendo wa mashairi katika ushairi wa Kiswahili kwa kutumia mifano kutoka katika diwani za *Wasakatonge* na *Kimbunga*.

## 2.5 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti umeongozwa na mihimili ya Nadharia ya Upokezi, ambayo imetumika kama dira wakati wa ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wake.

Nadharia ya Upokezi inahusika na upokeaji wa matini za fasihi ambazo zinatoa muongozo kwa msomaji kupokea ujumbe uliomo ndani ya matini za fasihi, kwa lengo la kupata ujumbe husika (Njogu na wenzake, 1999). Wataalam hawa wanaendelea kueleza kuwa Nadharia hii pia imejikita katika kumchunguza msomaji vipi anapata maarifa ya kuzisoma kazi za fasihi. Nadharia hii iliasisiwa miaka ya

1960 hadi 1970. Watetezi wakuu wa nadharia hii ni Stanley Fish (1980), Jane Tompkins (1980) na Wolfgang Iser (1974) wote kutoka Ujerumani (Wamitila, 2002).

**Mihimili ya Nadharia ya Upokezi**

Waasisi wa nadharia ya upokezi waliona kuwa ili nadharia hii iweze kutumika vizuri mtafiti amepaswa kuzingatia hoja zifuatazo:

a) Je, Kuna aina yoyote ya mfanano wa kimaana kati ya kazi ya fasihi inayosomwa na inavyotafsiriwa na hadhira?
b) Je, kazi ya fasihi inatoa ujumbe kama ulivyokusudiwa na mtunzi kwa hadhira ?
c) Je, Kuna tofauti ya upokezi wa usomaji kati ya wasomaji wenye kusoma vizuri na wenye kusoma vibaya?
d) Je kuna vigezo maalum vinavyojulisha kuwa kazi fulani ya fasihi inafaa au haifai?

Baada ya kuzionaoja hizo wataalam mbalimbali walitoa fikra zao ambazo ndio mihimili ya nadharia hii. Kwa mfano Rosmarin (1991) anadai kuwa, usomaji haukamiliki mpaka kwa kuungwaungwa Hata hivyo, msomaji huikamilisha kazi ya fasihi kwa kijiuliza je amesoma vizuri au vibaya. Vilevile Fish (1980) aliunga mkono kuwa kazi ya fasihi haipimwi kwa jaribio la kisayansi, kwani jaribio la kisayansi huweka mipaka ya kimawazo kati ya msomaji na jaribio husika, kwani pasipo jaribio msomaji huweza kuzichambua vizuri kazi za fasihi. Fish aliendelea kusema kwamba kazi za fasihi hufungwafungwa kiasi ambacho hadhira hupaswa kuifungua na kubuni mawazo mapya kutoka katika matini chanzi, hii ni kutokana na msomaji kuwa na jukumu kubwa la kuusaka ujumbe, vilevile dai hili liliungwa mkono na (Wafula na Njogu, 2007).

Hata hivyo, waitifaki wa wanaupokezi wameona kuna haja ya kusoma kwa kuzingatia njia mbili muhimu kama zifuatazo;

a) Usomaji unaofafanua na kusisitiza mawazo ambayo msomaji binafsi anayakubali.
b) Kumchochea msomaji kurudia kusoma kazi ya fasihi ili kugundua mambo yaliyofumbwa na kutambua sauti zinazodhihirika katika kazi ya fasihi.

Nadharia ya Upokezi imemsaidia mtafiti kufikia malengo kama ifuatavyo: Mtafiti ameitumia baadhi ya misingi ya nadharia hii kubainisha mikabala ya kuibua vipengele na dhima za mwendo wa mashairi katika ushairi wa Kiswahili ambazo zilitumika kuudhihirisha mwendo wa ushairi. Nadharia imetumika katika kutathmini namna mwendo wa ushairi unavyoathiri uelewa kwa msomaji au msikilizaji. Mwisho nadharia imemsaidia mtafiti katika upatikanaji wa data, ufafanuzi wa data na utoaji wa matokeo ya utafiti huu.

## 2.6 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura imechambua baadhi ya maandiko muhimu yenye uhusiano na utafiti huu.Sura imeanza na maandiko yanayohusiana na dhana ya mwendo wa ushairi wa Kiswahili kwa jumla na maandiko yanayohusiana ushairi wa Kiswahili na kuunganishwa na historia ya waandishi vitabu teule Muhammed S. Khatib na Gora Haji Gora. Pia katika sura hii mtafiti ameichambua nadharia ya upokezi ambayo imetumika katika kufanikisha ukusanyaji na uchambuzi wa data pamoja na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Lengo la uchambuzi huo lilikuwa ni kuonesha mapengo ambayo yamezibwa kupitia utafiti huu. Sura inayofuata ni ya tatu ambayo imejikita katika kueleza methodolojia iliyotumika kukamilisha utafiti huu.

# SURA YA TATU
# METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imejadili mkabala wa utafiti, mbinu, na vifaa ambavyo vimetumika katika utafiti. Utafiti umetumia mkabala wa kitaaamuli (kimaelezo) katika kukusanya na kuzichambua data za utafiti huu. Kama wanavyoeleza (Kombo na Tromp, 2006), utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu hujazilizana na kukamilishana. Kwa maana hiyo, utafiti huu ulihusisha maelezo ya data na pia ulitumia nduni za utafiti wa kitakwimu. Hivyo, sura inajadili mbinu za utafiti na hatua zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data. Sura imehusisha usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, ukusanyaji wa data, njia na zana za kukusanyia data, mchakato wa ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, itikeli za utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti na utatuzi wake, na mwisho muhtasari wa sura ya tatu.

## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mfumo maalum unaoonyesha vipi utafiti umeendeshwa kuanzia mwanzo wa upatikanaji wa data, ufafanuzi wake na mwisho kuzitolea ufumbuzi (Kothari, 2008). Kothari anasisitiza kuwa utafiti ni utaratibu wa kuziweka taarifa pamoja na kuhakikisha zinakwenda sambamba na malengo na kuzitolea ufafanuzi wa kina na mwisho kutoa majibu. Hivyo, usanifu huu umekuwa wa kifafanuzi na umefanyika kwa njia ya maelezo, ambapo mtafiti amepata muda wa kutosha wa kuyaangalia mambo kwa kina na baadaye kuyatolea suluhisho muafaka katika upatikanaji wa data zake, ufafanuzi wake, na kuzitolea majibu. Utafiti umehusisha pia data za awali pamoja na za upili. Data za upili zimepatikana kwa uchunguzi wa nyaraka mbalimbali zilizotoa majibu ya mwendo wa mashairi zikilinganishwa na diwani teule zilizochaguliwa na mtafiti kama kiigizo muhimu cha utafiti huu. Data za awali zimepatikana kwa njia ya mahojiano na walengwa wa utafiti. Mahojiano hayo yamewahusisha watunzi wa vitabu teule, wataalam wa fasihi, wahadhiri na wanafunzi wa (M.A) na (Phd) Kiswahili huko (SUZA) Nkurumah na Vuga Mjini Zanzibar.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika Zanzibar maeneo ya Unguja Mjini. Sehemu zilizohusika na utafiti huu ni maktaba kuu ya Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na sehemu wanazoishi wataalam wa fasihi ya ushairi na watunzi wa diwani teule. Maeneo haya yamehusika katika ukusanyaji wa data za uwandani na zile za kimaktaba. Uteuzi wa maeneo haya umekuja, kutokana na kila sehemu ina umuhimu wake kama ifuatavyo. Mosi Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ni sehemu ambayo wanapatika wahadhiri, wanafunzi wa (M.A) na (Phd). Pia mtafiti amepata kutumia maktaba kwa ajili ya kuongeza maarifa ya kujisomea kuhusu mada na ametumia tasinifu mbalimbali kwa kuongeza maarifa. Pili sehemu wanazoishi na watunzi wa vitabu teule na wataalam wa fasihi hasa nyanja ya ushairi ambao wametoa mchango mkubwa kuhusiana na mada.Tatu maktaba kuu ya Zanzibar ambako mtafiti amepata baadhi ya vitabu vilivyochangia kuendeleza utafiti wake.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Omari (2006) anasema walengwa wa utafiti ni jumla ya vitu au watu wenye vigezo maalum vinavyokubaliwa na mtafiti kulingana na mada yake. Hivyo, walengwa wa utafiti huu waligawanywa katika makundi matatu, ambayo ni wango tafitiwa, mbinu ya usaplishaji na sampuli ya watafitiwa.

#### 3.4.1 Wango la Watafitiwa

Watafitiwa waliotumiwa ni wataalum wa fasihi, watunzi wa ushairi, wahadhiri na wanafunzi wa shahada ya pili (M.A) na ya tatu (Phd) wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), na maeneo wanamoishi wataalamu wa fasihi. Wango la watafitiwa linafafanua makundi yake kama yafuatayo:

i. Wahadhiri wanaofundisha fasihi ya Kiswahili wa Chuo Kikuu chaTaifa Zanzibar (SUZA), na wanafunzi wao. Watafitiwa hawa walichaguliwa kutokana na uzoefu wanaoupata wakati wa kujifunza kwa wanafunzi na ufundishaji kwa wakufunzi.

ii. Waandishi wa diwani teule. Hawa ni wazoefu wa utungaji wa mashairi.

**iii.** Wataalam wa fasihi hasa mashairi. Hawa walitoa uzoefu wao kuhusu mada ya utafiti na kutoa maelekezo kwa mtaalam mwingine ambako mtafiti alikwenda kupata taarifa zaidi kuhusu mada.

### 3.4.2 Mbinu ya Usampulishaji

Trochim (2000) anaona kuwa dhana ya usampulishaji ni utaratibu maalum wa kutafuta sehemu ndogo kati ya kundi kubwa la watafitiwa ili kumpatia mtafiti taarifa zinazotosheleza ambazo amezifanyia kazi na kutoa majumuisho yanayowakilisha kundi kubwa la watafitiwa. Katika utafiti lengwa mtafiti alitumia usamplishaji usio bahatishi.na mbinu ya usaplishaji lengwa. Usamplishaji lengwa umetoa nafasi kwa mtafiti kuchagua watafitiwa wanaoshiriki katika kutoa taarifa za utafiti zinazokwenda sambamba na malengo na upeo wa mahitaji ya utafiti wake (Enon, 1998). Utafiti umetumia usamplishaji lengwa wa aina mbili nazo ni usamplishaji lengwa wa kipekee na wa mpokezano. Usamplishaji lengwa wa kipekee, unahusu watafitiwa wenye sifa za kipekee kwa mfano wahadhiri na wanafunzi wa Chuo Kikuu (SUZA), mbinu ya usamplishaji lengwa ya mpokezano ilihusika na wataalam wa fasihi (ushairi), na watunzi wa vitabu teule, hapa ndipo mtafiti alipopata fursa ya mtafitiwa kumuelekeza kwa mtaalam mwingine mwenye sifa zinazolandana na mada na wapi anapatikana. Kutokana na mbinu hizi mtafiti alipata data zenye tija kwa utafiti wake. Idadi kamili ya watafitiwa ilikuwa ni watu kumi na sita (16) kutoka katika makundi yote pamoja na diwani mbili. Kwa hiyo sampuli ya utafiti huu ilikuwa katika mchanganuo kama ufuatao:

a) Wahadhiri wanne (4) wa somo la fasihi ya Kiswahili wenye kuzifahamu kazi teule ambao wanatoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).
b) Wanafunzi (4) wa shahada ya pili katika fasihi ya Kiswahili kutoka katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), wenye kuzifahamu diwani teule, na pia dhana ya mwendo wa ushairi.
c) Wanafunzi (4) wa shahada ya tatu wanaochukua kozi ya fasihi ya Kiswahili wenye kuzifahamu diwani teule katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).
d) Wataalam wa fasihi ya Kiswahili wawili (2) na watunzi wa diwani teule mashairi wawili (2) ambao mtafiti amewafuata katika maeneo yao wanayoishi.

## 3.5 Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii inahusu njia za ukusanyaji data pamoja na zana zake. Mtafiti alitumia njia mbili ambazo ni mahojiano na uchunguzi wa nyaraka. Njia hizi zilitumika ili kumpatia data sahihi na zenye uhakika. Patton (1990) anaunga mkono matumizi ya

mbinu katika tendo la ukusanyaji wa data yeye alidai kuwa ukusanyaji wa data humwezesha mtafiti kuelewa kinachohitajika na kinachoendelea wakati wa ukusanyaji wa data.

### 3.5.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data

Ikumbukwe kwamba utafiti ni kazi yenye hatua nyingi hadi kutoa matokeo, ili kufanikisha hatua hizo njia ya uchanganuzi wa nyaraka na mahojiano kwa ajili ya kupata data za awali toka kwa watafitiwa pamoja na data za upili kutoka maktabani zilitumika. Mtafiti pia alitumia zana mbalimbali kama kalamu, vijidaftari, karatasi, simu ya mkononi na vitu vyingine ambavyo vimesaidia katika kuendeleza mchakato mzima wa ukusanyaji data.

#### 3.5.1.1 Uchanganuzi wa matini

Uchanganuzi wa matini wa diwani teule umetumika kukusanyia data na yanayohusiana na mada hii ya utafiti. Uchambuzi wa maudhui yaliyomo kwenye matini hizo zilimuwezesha mtafiti kupata maarifa na data zinazoendana na mwendo wa mashairi ambazo alizihusisha kazi teule na kuuchambua mwendo wa ushairi kwa ujumla wake. Mtafiti alisoma maandiko ya hapo juu kutoka maktaba kuu ya Zanzibar na maktaba za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa lengo la upatikanaji wa data za kuridhisha kupitia maandiko hayo ambayo yamefanikisha kufikia lengo la utafiti huu.

#### 3.5.1.2 Mahojiano

Mahojiano ni mbinu ya kukusanyia data ambayo mhoji huwakaribia wahojiwa kwa kuwauliza maswali na kuandika majibu yao (Raj, 2005). Mahojiano hayo yalihusisha mpangilio wa maswali yaliyotoa majibu kutoka kwa watafitiwa kwa kutumia mdomo kwa kuwauliza maswali yaliyotayarishwa maalum yanayolenga mada husika. Mtafiti alitumia njia hii kwa kuwasiliana na watafitiwa kwa njia ya ana kwa ana au kwa njia ya mawasiliano ya simu, lengo likiwa kupata taarifa na mawazo yao kuhusu mwendo wa mashairi. Njia hii, imewalenga wataalam wa fasihi, wahadhiri, wanafunzi na watunzi wa diwani teule. Njia hii imetumia zana kama hojaji (maswali), simu ya mkononi kwa ajili ya kurikodi sauti na kuchukua picha kalamu na daftari kwa ajili ya kunukuu mambo muhimu yaliyopatikana katika mahojiano hayo. Mtafiti alichagua njia hii kutokana na faida zifuatazo: Moja, amepata ukaribu

na uaminifu kati yake na mtafitiwa na kusababisha kupata data nzuri. Pili, mtafiti alipata nafasi ya kuuliza maswali ya papo kwa papo ambayo yametoa nafasi kwa mhojiwa kueleza kwa kina kuhusu jambo lililokusudiwa. Tatu, mtafiti aliweza kuuliza maswali chomozi yanayohusu mada. Hii ilitokea pale ambapo mtafiti alikuwa anahitaji ufafanuzi zaidi wa mambo ambayo yalikuwa hajayafahamu wakati wa zoezi la mahojiano ya ukusanyaji wa data. Pia changamoto ya njia hii ni kwa baadhi ya watafitiwa kutokuijua mada kabisa na kutoa melelezo yasiyohusiana na mada. Kwa hiyo, mtafiti baada ya kuona kasoro hiyo aliona hapana budi kuongeza watafitiwa wenye ujuzi zaidi wa fasihi ya ushairi ili kupata usahihi wa data zinazohitajika.

### 3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data

Data za tasinifu hii zilikusanywa kwa kupitia uchunguzi wa nyaraka na kuwahoji watafitiwa. Katika uchunguzi wa data mtafiti alitumia njia ya usomaji nyaraka. Mtafiti amekusanya data kwa njia ya usaili. Mwongozo wa maswali ya usaili ulitumika kwa kuwahoji watafitiwa wake katika maeneo wanayopatikana. Mwongozo umelenga moja kwa moja kwenye malengo ya utafiti kwa kudadisi na kupata taarifa za mwendo wa ushairi kwa kuhusianisha vitabu teule vya *Wasakatonge* na *Kimbunga*. Wakati huohuo mtafiti alitumia vifaa vya ukusanyaji wa data kama vijidaftari, kalamu, simu ya kuchukulia picha na kunasa sauti. Data zilizokusanywa miezi miwili, mtafiti alihakikisha kwamba siku aliyochukua taarifa zilifanyiwa kazi ili kuepusha usahaulifu.

## 3.6 Uchanganuzi wa Data

Data zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia ufafanuzi wa maelezo kwani utafiti huu ni wa kitaamuli. Data zimechanganuliwa kwa mwegamo wa kimaudhui. Uchanganuzi huu umezingatia misingi ya Nadharia ya Upokezi. Hii imesaidia kuweka wazi mjadala wa kila lengo la utafiti. Katika uchanganuzi wa data mawazo ya msingi yaliyotolewa na watafitiwa lazima yazingatie malengo na maswali ya utafiti (Cresswell, 2012). Hata hivyo, kila lengo liliunda mada iliyokamilika ambayo ilikwenda sambamba na mada husika. Data zilichambuliwa na kutolewa matokeo kwa mbinu ya ufafanuzi. Mtafiti amebandika vielelezo na picha ili kuthibitisha ukweli wa data za utafiti.

### 3.7 Itikeli ya Utafiti

Mtafiti alizigatia maadili na miiko iliyomuongoza kuanzia uombaji wa kibali hadi kutoa majibu ya utafiti. Utafiti huu ulifuata miongozo na sheria zilizowekwa za kufanyia utafiti kama zifuatazo: Kwanza, mtafiti aliomba barua ya ruhusa kutoka kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambayo ilimsaidia mtafiti kuwa na ithibati ya kutambuliwa na kuaminika kuwa ni mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri. Pili, mtafiti aliwaomba watafitiwa wampe ushirikiano kwani aliwahakikishia kuwatunzia usalama wao kwa muda wote wa mchakato wa utafiti na baada ya utafiti huu. Mtafiti aliwaomba ridhaa watafitiwa ili wampe majibu ya maswali yake katika hatua ya ukusanyaji wa data.

### 3.8 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Kothari (2008) anasema kuwa ili matokeo yawe halali lazima uhalali utokane na utafiti wenye viwango maalum vinavyotakiwa kupimwa katika utafiti husika. Kwa upande wa uthabiti ni jinsi ya utafiti ulivyoweza kutoa matokeo yanayolingana hata kama utafiti kama huu umefanyika sehemu nyingine (Kothari, 2004). Kwa hivyo, uhalali na uthabiti wa matokeo ili yawe halali mtafiti amepaswa kuzingatia vigezo vifuatayo: Kwanza kuyafafanua kwa uwazi malengo ya utafiti husika. Hii ilimsaidia mtafiti kwenda sambamba na lengo hasa katika masuala ya upana wa mawanda na mipaka ya utafiti huu bila ya kuathiriwa na mambo yaliyo nje ya utafiti. Pili, mtafiti alitumia mbinu tofauti za kukusanyia data ambazo zilimsaidia mtafiti kupata data sahihi zenye viwango bila kutumia mawazo yake binafsi katika utafiti huu. Tatu, matumizi mazuri ya lugha yenye kueleweka wakati wote, hii ilisaidia kueleweka kwa watafitiwa na kupata majibu mazuri ya maswali ya utafiti huu.

### 3.10 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake

Utafiti umeleta mafanikio kadhaa yaliyopatikana. Hata hivyo, mtafiti alikumbana na baadhi ya changamoto wakati wa ukusanyaji wa data za maktabani na uwandani. Miongoni mwa changamoto hizo: Mosi, ugumu wa upatikanaji wa data kutoka kwa watafitiwa kuhusiana na upya wa dhana ya mwendo katika ushairi wa Kiswahili. Hii ni kutokana na dhana yenyewe ya mwendo wa mashairi kutojulikana kabisa kwa baadhi watafitiwa. Pili, watafitiwa wengi waliomba muda wa matayarisho na baadhi yao baaada ya muda kufika walishindwa kabisa. Baadhi ya watafitiwa walikosa hata muda wa kufanya mahojiano na mtafiti kutokana na kuzongwa na majukumu yao.

Mtafiti alizitatua changamoto kama ifuatavyo; Mosi, mtafiti alitumia busara na hekima katika kuwaelimisha watafitiwa kuhusiana dhana ya mwendo, kwa upande wa nathari na kuwataka kueleza kwa mawazo yaona jinsi wanavyo uwelewa mwendo katika mashairi. Mtafiti alikuwa na moyo wa subira kwa kuwapa muda na kwenda siku nyingine na huku akitafuta wataalam wengine ili kukamilisha taarifa za utafiti. Hizi ndizo baadhi ya changamoto na namna utatuzi wake ulivyofanyika.

### 3.11 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Katika sura hii mtafiti amefafanua methodolojia ya utafiti. Sura imeeleza namna ambavyo mtafiti alifanikisha suala la ukusanyaji wa data na uchambuzi wake. Mtafiti ameeleza kuwa utafiti huu ni wa kitaamuli ambao ulijiegemeza katika maelezo. Hivyo, data zilizokusanywa zimechambuliwa kwa kuzilinganisha data za uwandani na za maktabani na baadaye kuziwasilisha kwa njia ya maelezo. Katika sura hii sampuli ya utafiti iliyotumika katika tasinifu hii imeelezwa kuwa ni sampuli lengwa ikiwa na lengo la kupata taarifa maalum zilizohusiana na utafiti huu. Hata hivyo, sura imeangazia eneo lililotumika wakati wa utafiti huu. Pia sura hii imeeleza kuhusiana na itikeli na maadili muhimu yaliyozingatiwa wakati wa mchakato mzima wa kufanikisha utafiti huu, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti pamoja na mawanda ya utafiti. Na mwisho, zimeelezwa changamoto mbalimbali zilizoukumba utafiti huu pamoja na jinsi zilivyotatuliwa ili kuufanikisha. Sura inayofuata ni sura ya nne ambayo ilihusisha uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti huu kama ifuatavyo:

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utagulizi

Sura hii inawasilisha taarifa zilizokusanywa uwandani na maktabani. Sura hii imegawanyika sehemu tano. Mgawanyiko huu uko kama ifuatavyo: Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi wa sura nzima. Sehemu ya pili imehusisha vipengele vinavyojenga mwendo na ufafanuzi wake katika mashairi katika diwani teule. Sehemu ya tatu inafafanua dhima za vipengele vinavyojenga mwendo wa shairi katika diwani teule. Sehemu ya nne inahusisha kutathmini athari za mwendo katika ushairi wa Kiswahili. Sehemu ya tano imeeleza muhtasari wa yale yaliyojadiliwa katika sura nzima.

## 4.2 Vipengele Vinavyojenga Mwendo wa Mashairi katika Ushairi wa Kiswahili

Utafiti huu umefafanua vipengele vilivyotumika kuujenga mwendo katika ushairi wa Kiswahili. Pia umeonesha vipi waandishi wa vitabu teule vya *Wasakatonge* na *Kimbunga* walivyovisawiri vipengele hivyo. Kabla ya kujadili vipengele hivyo tunaanza kwa kutoa muhtasari wa diwani teule kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Muhtasari wa Diwani za Wasakatonge na Kimbunga

Kama tulivyodokeza hapo juu kuwa diwani zilizotumika ni *Wasakatonge* na *Kimbunga*. Hivyo, sehemu hii inaanza kwa kufafanua kwa muhtasari diwani ya *Wasakatonge* kama ifuatavyo:

#### 4.2.1.1 Muhtasari wa Diwani ya Wasakatonge

*Wasakatonge* ni diwani iliyoandikwa na Muhammed Seif Khatib ikiwa na matoleo mbalimbali kuanzia mwaka 2003, 2004, 2005, 2007, 2009, 2011 na 2012. *Wasakatonge* ni diwani inayolenga watu wanaofanya kazi duni za sulubu kwa ajili kupata maslahi katika jamii zao.

Kwa upande wa maudhui mwandishi anaonesha wavuja jasho wanavyohangaikia mlo wao wa kila siku huku wakidhulumiwa, kuteswa na kunyonywa na tabaka tawala. Mwandishi pia amebainisha migogoro kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa kutokana na tabaka hilo kuonewa na kunyanyaswa. Diwani imeonyesha uozo wa jamii na athari za uozo huo kwa wanyonge wa tabaka la chini. Mtunzi wa

diwani hakuacha kuwazindua wanajamii walioghilibiwa na kudanganywa kusudi waamke na kudai haki zao kwa wanasiasa madikteta wanaotumia nguvu za dola kuunyonya umma.

Kwa upande wa fani mwandishi ameibua utunzi wenye matumizi mengi ya tamathali za semi zikiwamo sitiari, tashbiha, tashhisi, tauria, mubalagha na nyingi nyinginezo. Aidha ametumia mafumbo, lugha ya picha na ishara kwa kiasi kikubwa. Katika diwani hii mtunzi ametumia mashairi ya kisasa na ya kimapokeo.

Diwani hii imetuwezesha kubaini aina za mwendo wa mashairi katika ushairi wa Kiswahili ambao tumeongelea sana kuanzia na vipengele vinavyoujenga mwendo, dhima na athari za mwendo huo kwa hadhira.

#### 4.2.1.2 Muhtasari wa Diwani ya Kimbunga

Diwani ya *Kimbunga* ilizinduliwa rasmi mnamo 1994 na mtunzi wake Bw. Gora Haji Gora na TUKI, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Diwani imetungwa kwa kujumuisha mashairi 51 yenye ubingwa wa fani na maudhui tofauti. Diwani imeitwa jina la *Kimbunga* kwa sababu ndani yake kuwemo shairi la *Kimbunga* ambalo linaonekana limebeba dhana nzima ya maudhui ya ukombozi katika diwani hiyo.

Kwa upande wa maudhui diwani ya *Kimbunga* inayozungumzia masuala ya kijamii yanayohusu maisha ya binadamu zikiwamo nasaha nzito kwa vijana vipi waishi ili wafanikiwe katika maisha yao. Aidha, inazungumzia suala la ujenzi wa jamii mpya ambalo mtunzi anaona kuwa linaweza kuleta mabadiliko na maendeleo ya haraka yamesababisha kuinua uchumi wa wananchi walio wengi wa tabaka la chini.

Katika kufikia azma hii, mwandishi ameonesha tungo zenye kugusa fikra na hisia za ndani za hadhira za kimapenzi na kisiasa kwa namna ya kipekee. Pia mtunzi amelezea vikwazo vinavyokwamisha ujenzi wa jamii mpya kama uongozi mbaya, ukoloni mamboleo,wizi uliokithiriwa mali za umma, rushwa, uongo wa viongozi na kadhalika.

Kwa upande wa fani mwandishi ametumia mbinu mbalimbali za kuwavuta wasomaji wake. Kwa mfano miundo tofauti ya mashairi, mtindo wa kimapokeo na matumizi mbalimbali ya lugha. Mwisho mwandishi amependekeza njia bora zitakazosaidia

ujenzi wa jamii mpya kwa mfano uongozi bora, kupiga vita rushwa, umuhimu wa elimu, kupinga ukoloni mamboleo na mengineyo

### 4.2.2 Vipengele Vinavyojenga Mwendo wa Mashairi

Sehemu hii inafafanua vipengele vinavyojenga mwendo wa mashairi na kuunganishwa mifano yake kutoka diwani teule. Miongoni mwa vipengele vilivyofafanuliwa ni lugha, muundo, vina, maudhui, uteuzi wa maneno, mandhari na wakati, lafudhi, maghani, taswira na kibwagizo navyo vimejadiliwa kama ifuatavyo:

#### 4.2.2.1 Lugha

Lugha ni mfumo maalumu wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii zenye utamaduni unaofanana ili waweze kuzitumia wakati wa kuwasiliana (TUKI, 1990). Katika kawasiliana huko watu hutumia njia tofauti ikiwamo sanaa ya mashairi. Sanaa hiyo ya mashairi huwasilishwa kwa kutumia lugha, na katika kuichambua lugha ya mashairi utafiti umebaini kuwa lugha ina nafasi kubwa katika kufanikisha utafiti huu. Wahojiwa wa utafiti huu wamebainisha lugha kama kipengele kimojawapo kinachojenga mwendo wa shairi. Zimeainishwa aina tatu za lugha ambazo ni lugha nzito/ngumu, lugha ya wastani na lugha nyepesi. Wahojiwa wamezieleza aina hizi na namna mwendo wa shairi unavyofanyika kwa kupitia kipengele cha lugha. Mhojiwa Daulat[1]anaanza kwa kueleza jinsi lugha ngumu ya shairi inavyojenga mwendo wa shairi kwa kusema:

> Lugha ngumu au ya huzuni; katika lugha hii mwendo wa shairi unakuwa wa polepole kutokana na kumfikirisha na kumpa msomaji hisia kali zilizomo ndani ya maudhui husika.

Mhojiwa aliendelea kueleza kwamba mara nyingi mwendo wa mashairi wa aina hii humfikirisha msomaji na msikilizaji kiasi kwamba huweza kujiinamia kwa kutafakari ujumbe anaopatikana kutoka ndani ya shairi hilo. Katika kuthibitisha nafasi ya lugha katika mwendo wa shairi, mhojiwa Ame[2] anaeleza kuwa:

---

[1] Bi Daulat Abdalla said ni mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na ni mwanafunzi wa shahada ya uzamivu Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) mahojiano na mtafiti yalifanyika ndani ya ofisi yake huko Nkuruma nje kidogo ya mji wa Zanzibar Juni 30 , 2020.

[2] Ame Malik ni Mwanafunzi wa shahada ya umahiri (M.A) Kiswahili Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA). Mahojiano yalifanyika katika skuli ya sekondari ya Al-Fallah Zanzibar.Julai, 10, 2020.

> “Lugha ngumu ndio inayoundiwa maudhui ya shairi na ndio inayoonesha aina ya mwendo wa shairi kutokana na namna lugha hiyo ilivyotumika ndani ya shairi husika”.

Hii ina maana kwamba lugha ngumu ndiyo inayobeba ujumbe unaotarajiwa kuwasilishwa na shairi ikilinganishwa na mahitaji husika ya shairi; umuhimu wake katika kulifanya shairi lieleweke kwa hadhira ni mkubwa zaidi ukilinganisha na vipengele vingine tajwa. Mhojiwa anatoa mfano wa lugha nzito kuwa husababusha mwendo wa polepole na kutoa maudhui mazito na hivyo mwendo wa shairi hufanywa kuwa wa taratibu mno. Akionekana kuunga mkono wazo hili, mhojiwa Hassan[3] alieleza kuwa;

> “…... Lugha ikiwa ngumu mwendo wa shairi utakuwa wa polepole na hivyo kuleta ugumu katika kufikisha ujumbe kwa baadhi ya hadhira”

Mawazo ya watafitiwa hawa kuhusu lugha ngumu inayokwenda sambamba na mwendo wa shairi wa polepole ambayo wakati mwingine humpandisha hadhi mtunzi na wasomaji wake kwa kubaini ujumbe uliokusudiwa ambao ni wa kufichwa  Haya yamethibitishwa na mwandishi wa diwani ya *Kimbunga*. Shairi la *Vitendawili* linaonyesha ugumu wa lugha unaokwenda sambamba na mwendo wa shairi wa polepole kama ifuatavyo:

*Kitandawili na tega, na tega kiteguweni*
*Tuguweni bila woga, na kutaja kwa lisani*
*Paa mayai kataga, katotoa wana nyani*
*Wateguzi tegueni, moja baada ya moja*

*Kuna yalozidimno, kuajabisha nyoyoni*
*Pana wakonge watano, wanashindana kwa fani*
*Wakata mawe kwa meno, na kujaza matumboni*
*Wateguzi teguweni, moja baada ya moja*

*Nasema kinaganaga, mengine sikilizeni*
*Farasi kula mizoga, na kufukua mavani*

---

[3] Mr. Hassan Hija ni Mhadhiri wa taaluma ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Pia Mwanafunzi wa shahada ya uzamivu Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Mahojiano na mtafiti yalifanyika Julai, 8, 2020. Katika ofisi yake huko Nkuruma.

*Kuna kijungu chapwaga, bila ya moto jikoni*
*Wateguzi tegueni moja baada ya moja (uk:13 )*

Beti za shairi hili zinaonyesha ugumu wa lugha inayofuatana na mwendo wa polepole kwani zinahitaji uelewa wa kutosha wa lugha na kutegua fumbo alilolikusudia mwandishi. Kwa mfano, maneno kama *Paa mayai kataga, katotoa wana nyani, Wakata mawe kwa meno, na kujaza matumboni, farasi kula mizoga, na kufukua mavani, kuna kijungu chapwaga, bila ya moto jikoni* si rahisi kueleweka maana iliyokusudiwa iwapo msomaji wa shairi hana umahiri wa kutosha wa lugha ya shairi, humfanya msomaji asome kwa kutafakari neno moja badala ya jingine na hivyo kufanya mwendo wa shairi hilo kuwa wa polepole.

Wakati huohuo, wahojiwa walipotakiwa na mtafiti kueleza nafasi ya lugha ya wastani inavyojenga mwendo wa shairi walitoa majibu ya kutofautiana. Hata hivyo, wengi walieleza kuwa lugha ya wastani hujenga mwendo wa wastani katika shairi. Katika kufafanua dhana hii, mhojiwa Ali[4]anasema kwamba:

> Lugha ya wastani husaidia kuchanganya maudhui ya furaha na tanzia katika mashairi hivyo utumikaji wake katika utanzu huu wa fasihi ni jambo lenye umuhimu mkubwa.

Kutokana na maelezo ya mhojiwa huyu, umuhimu wa utumiaji wa lugha ya wastani katika shairi unaweza kuonekana kutokana na ukweli kwamba msomaji wa shairi anaweza kupata huzuni fulani anaposoma kipande cha shairi fulani hata hivyo, anaweza kupata pia furaha fulani ya shairi hilohilo kabla kulimaliza kulisoma na ikawa ni faraja kwake, tofauti na lugha ngumu kupata huzuni pekee baada ya kusoma kipande fulani cha shairi na akamaliza na hali hiyohiyo. Hivyo, msikilizaji au msomaji hulazimika kulisoma kwa mwendo wa wastani kulingana na mchanganyiko wa huzuni na furaha na kufikia ujumbe alioukusudia. Lugha inayotumiwa katika mwendo wa wastani humfikirisha msomaji na msikilizaji wa shairi kwa kadri kutokana na maudhui ya shairi kutumia lugha ya nyepesi ya furaha na lugha nzito ya tanzia. Hoja hizo zinapata mashiko na kuunganishwa na mawazo ya diwani ya *Wasakatonge* shairi la *Wasomi* shairi lenye mwendo wa wastani linasema:

[4] Ali Haji Hassan ni Mwanafunzi wa shahada ya umahiri (M.A) Kiswahili Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA). Mahojiano yalifanyika katika chuoni kwao Vuga Zanzibar.Julai, 10, 2020.

Kuna wasomi,

Makasuku,
Wanaokariri,
Au kuhariri,
Hawana ‘thiori,
Fikira ‘tasa,

Kuna wasomi,
Wana siasa,
Wao huhubiri,
Katika viriri,
Kama mawaziri,
Kufata pesa.

*Kuna wasomi,*
*Wazalendo,*
*Wapendao umma,*
*Kuletea nema,*
*Nao kujituma,*
*Kipata fursa.*

*Kuna wasomi,*
*Wahakiki,*
*Waliomahiri,*
*Wanaofikiri,*
*Kubuni nadhari,*
*Inavyopasa* (uk: 40)

Beti mbili hizi za mwanzo za shairi tajwa hapo juu, zinaakisi huzuni ambayo msomaji anaweza kuipata baada ya kuzisoma. Hata hivyo, beti mbili zinazofuata zinaweza kuleta furaha kwa msomaji kutokana na kuonyesha hali chanya tofauti na ilivyoelezwa kwa beti za awali, huu ndio umuhimu mkubwa wa mwendo wa wastani katika shairi kama ulivyoelezwa na baadhi ya wahojiwa.

Katika kumalizia kuhusu umuhimu wa lugha katika kuamua mwendo wa shairi, mtafiti alitaka kujua umuhimu wa lugha nyepesi katika shairi. Wahojiwa wote walikubaliana kuwa lugha nyepesi inapelekea mwendo wa harakaharaka kwa msomaji wa shairi. Katika kufafanua dhana hii, mhojiwa Daulat (khj) alibainisha kwa kusema:

> Lugha ya nyepesi, kama ilivyo jina lake ni nyepesi na inafahamika.Waandishi wa mashairi huitumia lugha hii kwa kuwasilishia maudhui ya kuburudisha au matumaini ya jambo zuri

> ambayo hujenga mwendo wa harakaharaka. Msomaji hutiririka kwa taharuki kwa kujisikia raha kwa sababu anakipata kile anachokikusudia na kumfanya asome kwa mwendo wa harakaharaka bila ya kufikiri sana.

Mhojiwa huyu anatoa mfano wa mashairi ya mapenzi na ya ucheshi kwamba mara nyingi hutumia lugha nyepesi. Hata hivyo, ukweli kwamba wasikilizaji katika mwendo wa haraka wakati mwingine hupenda ladha ya mahadhi kutoka kwa msomaji na hisia za mapenzi kuliko kuchunguza ujumbe wa shairi  Hii ina maana kwamba utumiaji wa lugha nyepesi humfanya msomaji ua msikilizaji iliyepata ujumbe kwa haraka kutokana na kufahamu maana ya kila neno lililotumika katika shairi. Hali hii inasaidia hata kuokoa muda wake kwa vile hakuna haja ya kutafakari kwa muda mrefu au hata kutouliza maana ya maneno yaliyotumika katika shairi kwa watu wengine ambao ni wajuzi zaidi wa lugha ya fasihi kuliko yeye. Hii ni kutokana na mwendo wa harakaharaka watunzi wanakuwa hawazingatii sana utajaji wa kila kitu ni mwendo wa kurusharusha matukio,  kutokana na watumiaji wakubwa wa mashairi ya aina hii ni vijana ambapo  mambo yanayoelezwa yanawagusa sana katika maisha yao kama vile siasa na mapenzi.

Hoja hizi zinaelezea kipengele cha lugha nyepesi kinavyotumika kujenga mwendo wa shairi wa harakaharaka zinaungwa mkono kupitia diwani ya *Wasakatomge* shairi *Mahaba* linasema

*Kama mahaba mzigo, nitwike usinituwe*
*Lau ni pande la gogo, liache silipasuwe*
*Kama mahaba kipigo, niradhi kinisumbuwe*
*Unipe japo kidogo, mwenzio nijilimbuwe*

*Kama mahaba maudhi, nipe ili uenziwe*
*Hata madhila naridhi, wala usishutumiwe*
*Sitaki niombe radhi, sio kosa lako wewe*
*Kupenda ni faradhi, simtaki mwenginewe*

*Kama mahaba wazimu, sihitaji nitibiwe*
*Bora niwe chakaramu, nipigawe watu mawe*
*kuwa kwanga ahmumu, wewe isikusumbuwe*
*dawa yangusiyo ngumu, mimi nipendwe na wewe.(uk:1)*

Tukichunguza beti tatu hizi tunabaini kuwa maneno yaliyotumika ni ya Kiswahili cha kawaida ambacho kinamfanya kila mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili kuweza

kupata ujumbe wa shairi hilo kirahisi na hivyo kuibua mwendo wa harakaharaka. Kutokana na kutumika lugha nyepesi katika ubeti wa kwanza inaweza kupelekea taharuki kwa msomaji.Hatimaye kukosa subira na kufanya harakaharaka kujitolea muhanga kwa lolote na liwe lakini apate penzi. Beti ya pili inazidi kuonyesha mwendo wa harakaharaka zaidi pale mhusika kuwa yupo tayari kutii chochote kinachotaka mpenzi wake.Ubeti wa tatu mhusika yupo tayari hata apatwe na maradhi ya wazimu na yuko radhi asitibiwe lakini penzi alipate. Kwa msomaji wa beti hizi humuongezea taharukimsomaji kutaka kujua mwisho wa tukio na kuzidisha kasi ya mwendowa usomaji.

#### 4.2.2.2 Muundo wa Mashairi

Muundo ni mpangilio maalumu wa beti na mishororo yake uliopangwa na msanii kwa nia ya kufikisha maudhui mbalimbali kwa hadhira iliyokusudiwa na mtunzi (Njogu na Chimerah, 1999). Katika kuangalia muundo wa shairi tumeangazia muundo wa mishororo ndani ya beti na idadi ya beti za shairi husika. Watafitiwa waliojibu walibaini kuwa muundo wa shairi ni miongoni mwa vipengele vya mwendo wa shairi; na walieleza namna vinavyojenga mwendo wa shairi, kama Bi Daulat (khj) anavyosema:

> Muundo wa shairi likiwa na mistari mingi kwa kila ubeti bila shaka mwendo wa shairi utapungua na kuwa wa polepole ukilinganisha na ubeti wenye mistari michache kama miwili au mitatu hata kama maudhui ni mamoja, mwendo utakuwa wa harakaharaka.

Hapa ana maana kwamba kwa muundo wa shairi lenye mistari mfano 10 na kuendelea msomaji itambidi kutumia mwendo wa polepole kwa sababu inambidi kufanya tafakuri ya maudhui kutoka mstari wa mwanzo hadi wa mwisho. Wakati huo huo likiwa na mistari miwili au mitatu mwendo utakuwa wa harakaharaka hata kama maudhui yanafanana. Hii ina maana kwamba muundo wa beti zenye mishororo mingi ujumbe wake hukawia kufika na kupelekea mwendo wa polepole kwa kuwa msomaji na msikilizaji hupatwa na wakati mgumu wa kufikiri ili kupata dhana ya ubeti mzima. Kinyume chake shairi lenye beti zenye mishororo michache kama 3 hadi 4 mara nyingi ujumbe wake hupatikana kwa haraka na kufanya mwendo kuwa wa harakaharaka.

Hoja ya beti zenye muundo wa mishororo mingi ambayo inaibua mwendo wa polepole inathibitika wazi katika diwani ya *Wasakatonge* kwenye shairi la *Nahodha.*Vilevile shairi la *Warambanyayo* linathibitisha kuwa mistari michacheya shairi msomaji huweza kulisoma kwa mwendo wa harahaharaka ukilinganisha na shairi la *Nahodha* lenye mistari mingi. Shairi linasema:

*Nahodha*
*Wang'ang'ania sukani,*
*Na jahazi, lenda mramamrama,*
*Mrama, na kupasuka mataruma,*
*Mataruma, mkuku umeachana,*
*Meachana, tangalimo kudatama,*
*Kudatama, foromaliyainama,*
*Yainama, chombo sasa kitazama,*
*Nahodha tosa nanga!*
*Nahodha,*

*Wang'ang'niasukani,*
*Abiria, sote tunasikitika,*
*Teseka, kulewa na kutapika,*
*Kutapika, na ngama inatoka,*
*Inatoka, vikonge vyasulubika,*
*Yayatika, vitoto vyataabika,*
*Nahoza tosa nanga!(uk:42)*

Shairi *Waramba Nyayo* linasema:

*Waramba nyayo,*
*Waionea fahari,*
*Kazi hiyo.*

*Walifanya hayo,*
*Na bila yakufikiri,*
*Wana moyo.*

Beti zote zina maudhui ya aina moja ya siasa lakini beti mbili za mwanzo muundo wa mashairi yake ni mistari mingi hivyo hujenga mwendo wa polepole kutokana na kufanya tafakuri kila mstari kutafuta ujumbe kwa hiyo inakuwa vigumu kufanya tafakuri ya beti nzima. Na beti mbili za mwisho zina idadi ndogo ya mistari kuzisoma na kuzingatia kila mstari ni rahisi kupata ujumbe. Hivyo, mwendo wa beti mbili za chini utakuwa wa harakaharaka. Pia mhojiwa Daulat (khj) anaendelea kuongezea kuwa:

> Muundo wa beti mbili zenye mistari sawa mitatu au minne lilikiwa linazungumzia furaha litakuwana mwendo wa harakaharaka, na vilevile muundo wa shairi lenye mistari mitatu au minne likiwa linazungumzia tanzia litakuwa na mwendo wa polepole.

Hapa mhojiwa anazingatia tofauti ya kimaudhui kila shairi litakuwa na mwendo wake kwa mujibu wa maudhui ya kila shairi hata kama lina mistari sawa, mistari ya furaha mwendo wake wa harakaharaka na tanzia wake wa polepole. Hoja inathibitika kwa kupitia diwani ya *Kimbunga* shairi la *Punda* na *Wasakatonge* shairi la *Pendo Tamu*. Hili la pili linasema:

*Pendo tamu kama hili, hakuna mfano wake,*
*Halina yake mithili, duniani liko pweke,*
*Ladha yashinda asali huko kufanana kwake,*
*Pendo tamu kama letu, duniani hulikuti.(uk:35)*

Na katika diwani ya *Kimbunga* shairi linasema:

*Hasa akiwa kirongwe, limezidi kerolake*
*Si kinda wala mkongwe, ukaidi ndiyo wake*
*Pindi miguu igongwe, bendi mpaka atake*
*Kuchunga akikushinda, mwachiye ende zake (uk:22).*

Ubeti wa kwanza una muundo wa mistari minne na shairi lina maudhui ya furaha na kufanya mwendo wa harakaharaka. Katika ubeti wa pili kuna muundo wa mistari minne lakini shairi lina maudhui ya tanzia na linahitaji uteguzi wa fumbo la 'punda huyu punda gani'? Ubeti huu basi, husomwa kwa mwendo wa polepole. Hivyo, idadi ya mistari inaweza kuwa sawa lakini kila ubeti ukawa na mwendo wake.

Akiunga mkono kuwa suala la muundo ni kipengele kinachojenga mwendo wa shairi, mhojiwa Salma[5] anasema:

> Muundo wa beti za mashairi mara nyingi huwa kidogo ambazo kukusanya mambo mengi ukilinganisha na utanzu mwingine wa nathari, mwendo utakuwa wa harakaharaka kwenye mashairi.

Hapa mhojiwa ameuchukulia mwendo wa shairi hupatikana kwa mtunzi kusana kazi yake kwa kuingiza mambo mengo ndani ya beti chache na hutumia lugha ya mkato

[5] Dr.Salma Omar Hamad ni mhadhiri wa Taaluma ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria Zanzibar Kampas ya Nkurumah. Mahojiano na mtafiti, Julai 3, 2020 ofisini kwake Nkurumah.

na uteuzi wa maneno ni mambo yanayopelekea mwendo wa harakaharaka ukilinganisha na nathari. Kwani matukio ya kinathari huwa na uchambuzi mkubwa wa matukio na kufanya mwendo wa polepole. Kwa upande wa ushairi hili linathibitika katika diwani ya *Kimbunga* kwa kupitia katika shairi la *Vielelezo:*

*Ukimwi vielelezo, vyakevinoendeleza*
*Mtu hasa ni wa mwanzo, yulleasojituliza*
*Hupata maanbukizo, wengine kuanbukiza*
*Hiyo njia moja wapo inosambaza ukimwi*

*Damu nazo huchangia, pasi na kuichunguza*
*Vyenye vidudu vibaya, mwengine kumuongeza*
*Kuona wsaidia kumbe waangamiza*
*Na hilo ni moja wapo linosambaza ukimwi (uk:3)*

Shairi zima lilikuwa na beti nne. Beti mbili hizi ndizo hasa zilizoeleza tabia ya shairi ya kukusanya mambo mengi. Kwa mfano njia za kuuepusha na kusambaza kwa UKIMWI ni kama *sindano*, *damu* isiyochunguzwa. Mwisho wa shairi ametoa tahadhari kwa waganga kuwa ni ugonjwa hatari na wanajamii wafuate ushauri wa waganga ili kujiepusha na janga hili hatari.

#### 4.2.2.3 Ujenzi wa Vina

Massamba (1983) anasema vina ni zile silabi au mapigo yaliyomo ndani ya mistari ya ubeti, mapigo haya huwa kati na mwisho wa kila mstari katika shairi la Kiswahili. Hapa ana maana kwamba mapigo ya vina yanapelekea kuimbika kwa shairi kwa ajili ya kufikisha ujumbe kwa haraka. Katika utafiti huu vina vinaonesha umuhimu mkubwa katika kusaidia ujenzi wa mwendo wa shairi, kwani kazi yake kubwa ni kutoa msisitizo wa ujumbe ambao mtunzi anataka kuufikisha kwa jamii, kwa kuwa imebainika kuwa sehemu kubwa ya umbo la shairi ni vina. Wanamapokeo wanaamini kuwa vina ni msingi wa utunzi wa mashairi, na dhima yake kubwa ikiwa ni kutoa sauti na kulifanya shairi liimbike na kuweza kutofautika na kazi nyingine za fasihi. Daulat (khj) anaifafanua hoja hii kwa kusema:

> "Vina hasa vya mwisho vinaonesha aina ya mwendo kwa kutegemea msomaji atasoma kwa kutumia gani ya mahadhi wakati wa kughani shairi……"

Mhojiwa anaonesha kuwa vina vya mwisho ndivyo vinavyotoa mwendo wa shairi wa polepole, wastani au harakaharaka, hii ni kwa mujibu wa msomaji anavyoweza

kughani shairi kwa mujibu wa mwendo anaoutaka. Kwa mfano msomaji anaposoma shairi la mwendo wa harakaharaka na kuvikata vina vya mwisho katika kusoma kwake, na kuufanya mwendo wa shairi kuwa wa harakaharaka, au atapolisoma kwa kuvikata vina kwa kiasi mwendo utakuwa wa wastani na mwendo utakuwa wa pole baada ya msomaji kurefusha na kusoma kwa utulivu mkubwa na sauti ya upole. Vilevile katika kuliunga mkono suala la vina Vuai[6] alisema:

> Vina ndio shairi ili liwe shairi na liimbike hapana budi liwe na vina ambavyo hutoa mdundo unaovuta hisia za msikilizaji kuwa karibu na kusikiliza hata kama haelewi maana ya shairi linalosomwa, Hivyo msikilizaji huibua mwendo kulingana na kumsikiliza msomaji.

Hii ina maana kwamba ili shairi liimbike lazima litumie vina, vina ambavyo vinavyoweza kuvuta hisia za msomaji na msikilizaji, mara nyingi msikilizaji huvutwa na mapigo ya vina na kuchukuliwa mawazo yake. Msomaji husikiliza shairi hata kama haelewi maana yake. Kwa hiyo, mwendo wa shairi kwa mazingira haya humilikiwa na msomaji. Kwa mfano msomaji anaposoma shairi kwa kasi na msikilizaji hukimbizwa kwa mwendo wa haraka na mara nyingine hata kukosa ujumbe ili kwenda sambamba na msomaji wake. Mwendo wa polepole kwa msomaji kuna wakati humchosha msikilizaji wake. Kwa mwendo wa wastani msomaji na msikilizaji huwa wanakwenda sambamba katika kupata ujumbe. Kwa shairi lenye mwendo wa harakaharaka kutoka diwani ya *Kimbunga* shairi *Nakusabilia* linalosema:

*Nakusabiliya, pendo lote lako*
*Litaseleleya, litabaki kwako,*
*Sitaliachiya, kwenda kwa mwenzako,*

*Tuliya utuwe, poa moyo wako,*
*Fahamu ujuwe, wewe peke yako,*
*Hilo sitafanya, kuleta vicheko (uk: 23)*

Beti hizi zinasomeka kwa kutumia urari wa vina na mizani. Katika kuzisoma beti hizi msomaji ndiye muamuzi azisome kwa mwendo ili kwenda sambamba na msikilizaji wake. Hata hivyo, msomaji wa beti hizi anaweza kumchosha msikilizaji

[6] Bw. Vuai Saburi Muya ni mwanafunzi washahada ya uzamili Chuo Kikuu Huria tawi la Zanzibar (SUZA) Pia Ni mratibu wa kituo cha waalimu Dunga Zanzibar Mahojiano na mtafiti yalifanyika Julai, 8, 2020. Katika ofisi yake huko Dunga Zanzibar.

kwa mwendo wa pole au kumkimbiza kwa mwendo wa haraka kutokana na ufundi wa matumizi ya vina na aina ya mahadhi anayotumia msomaji.

Mtafiti amebaini kuwa kasiya shairi inaweza kupungua kutokana na mpangilio tofauti wa vina ndani ya ubeti mmoja na kupelekea ugumu wa mahadhi na kukosa mapigo ya vina. Hivyo ubeti unaweza kusomwa taratibu kwa kuyaridhia mapigo ya vina yaliyotofauti na kufanya mwendo wa polepole au wa wastani. Hoja inathibitika katika diwani ya *Wasakatonge* shairi la *Madikteta* linalosema:

*Madikteta*
*Katika,*
*Dunia hii ya tatu,*
*Na hasa Afrika yetu,*
*Itele "Mungu watu",*
*Bokasa, Iddi, mobutu,*
*Mizinga nayo mitutu,*
*Haitowi risasi,*
*Huto maraisi*
*Walio madikteta (uk:21)*

Ubeti unaonyesha kipengele cha vina kinavyojenga mwendo wa polepole kwa sababu ya matumizi ya aina tofauti za vina hufanya msomaji kupata ugumu wakati wa kusoma shairi. Kwa mfano katika ubeti mmoja mwandishi ametumia *ta, ka, tu* na *si* mbali na ugumu wake pia vinasababisha ugumu wa kukosa mapigo ambayo yanatoa mahadhi na pia inategemea maudhui ya shairi ya kiwa magumu huibua mwendo wa polepole.

Kwa kumalizia mtafiti amegundua kuwa vina huwa na sifa ya kutumbuiza kwa kutoa burudani kwa wasikilizaji mashairi. Burudani hii huambatana na mwendo ambao msomaji ameuchagua wakati wa tumbuizo. Mara nyingi mwendo huwa wa wastani kutokana na kuwa msomaji na msikilizaji huwa wapo katika hisia za furaha na utulivu. Beti zinazotumiwa katika tumbuizo mara nyingi huwa refu kiasi kwamba mapigo ya vina yaweze kumvuta msikilizaji. Sharif (1988) akizungumzia tubuizo la vina alisema

> Utumbuizo huweza kuwa wa kina kimoja tu au zaidi ya kimoja ambavyo hutumia vina zaidi ya kimoja kwa madhumuni ya kumsisimua na kumvuta hadhira.

Sharif ana maana kwamba usomaji kama huu wa utulivu, hivyo, msomaji hutumia mwendo wa wastani ambao utatumia sauti moja ya mapigo ya vina ambayo yatamfanya msikilizaji kuliwazika na kufikia ujumbe wa tumbuizi husika Hoja inathibitika kwa kuonesha tumbuizi lenye kina zaidi ya kimoja ambalo husomwa kwa mwendo wa wastani ilikutimiza haja ya wasikilizaji kutii kiu zao. Shairi kutoka diwani ya *Wasakatonge* shairi la *Sili Nikashiba* linalosema

*Mpenzi muhibu, menisusuika,*
*Umenighilibu, na kunigeuka,*
*Unanipa tabu, na mengi mashaka,*

*Sili nikashiba, nikikumbuka,*
*Hula habahaba, na kushikashika,*
*Ninjozi za huba, kweli nasumbuka.*
*Kiitikio*
*Njoo mahbubu, upoze mtima,*
*Tamu lako huba, ndo wangu uzima (uk:17)*

Beti mbili hizi zinaonesha vipi vina vya shairi vinavyoweza kubeba dhima ya kumtumbuiza msikilizaji kwa mwendo wa wastani wa shairi kwa kutumia mahadhi laini yenye mapigo ya sauti ya ***bu*** kwa kati ya mshororo na ***ba*** ili kuonesha vipi msikilizaji analiwazika.

#### 4.2.2.4 Mjengeko wa Wizani

TUKI (2003) wanasema kuwa wizani ni idadi ya silabi zinazopatikana katika mishororo ya ubeti. Kazi kubwa ya silabi ni kutoa mdundo utakaomwezesha msomaji au msikilizaji kupata msisitizo utakaowawezesha kulipata wazo la mwandishi. Wizani wakati mwingine hujulikana kama ridhimu. Matumizi mazuri ya wizani katika shairi humuwezesha msomaji kulisoma shairi kwa mahadhi mazuri na hata kumvuta msikilizaji wake katika kufikia ujumbe. Mhojiwa Vuai (khj) alichangia hili kwa kusema:

> Muundo wa shairi kwa upande wa kimapokeo wizani ni kitu cha msingi, kwa kuwa humuwezesha msomaji kuwa na uwiano sahihi wa mapigo katika kila mshororo ambayo hufuatanishwa na ujumbe wa shairi. Katika mapigo ya wizani ndimo mnamoibuliwa aina za mwendo wa shairi.

Maelezo hayo yanatufahamisha kuwa kila mtunzi ana ujuzi katika usanaji wake wa wizani, wapo wanaotumia idadi sawa kwa kila mshororo au kipande cha mshororo na

wengine hutumia wizani tofauti katika mistari ya beti zao. Lengo ni kutoa mapigo yatakayowawezesha wasomaji wa mashairi kwenda sambamba na wazo la shairi. Wamitila (2008) anasisitiza kuwa wizani ina sifa ya kujirudiarudia kwa mrudio unaoakisi mwendo wa shairi. Wamitila ana maana shairi limetungwa kwa ajili ya kuimbika ili liimbike vizuri hapana budi wizani za shairi zijirudie kwa kuzingatia wazo la mtunzi analokusudia kulifikisha kwa hadhira. Kwa mfano shairi limetungwa kwa wizani zenye mawazo mazito msomaji husoma kwa mwendo wa polepole na ikiwa shairi limetunga kutumia wizani zenye mawazo mchanganyiko bila shaka mwendo utakuwa wa wastani. Vilevile wizani za shairi zikiwa zinajirejea kwa mawazo ya furaha mwendo utakuwa wa harakaharaka. Hoja inathibitika kwani mara nyingi katika mashairi urudiaji wa mapigo ya wizani ni jambo la msingi sana urudiaji huu unaweza kufanywa mwanzoni mwa mstari, kati, au mwishoni mwa mshororo kwa lengo kuruhusu kuimbika. Kwa mfano katika diwani ya *Wasakatonge* shairi la *Tonge la Ugali* linalosema

*Wanasemana*
*Wanasutana*
*Wanakanyana*
*Kwatonge la ugali*

*Wanapigana*
*Wanaumizana*
*Wanauwana*
*Kwa tonge la ugali (uk:21)*

Beti hizi zinaonesha urudiaji wa wizani za mwanzo ***wana*** nawizani ya mwisho ***na*** ambapo urudiaji huu humfanya msomaji kuwa na mazoea katika matamshi ***wana*** na ***na*** kupelekea kulisoma shairi kwa mwendo wa harakaharaka na hasa ukizingatia wazo la shairi hilo si zito.

#### 4.2.2.5 Ujenzi wa Maudhui

Maudhui ni mambo yote yanayowasilishwa na mwandishi katika kazi ya fasihi na hujumuisha vipengele vyote vya maudhui (Wamitila, 2008). Mtafiti amebaini kuwa sifa kubwa ya maudhui ni kuweka wazi wazo au mawazo ya mwandishi pamoja na mtazamo wake na mafunzo ambayo humsukuma mwandishi kuitunga kazi ya fasihi na kuifikisha kwa hadhira yake. Hadhira huwa na kazi ya kuyahakiki maudhui kama

mazito kwao au mepesi. Ujenzi wa maudhui unaweza kuamua namna gani mwendo wa shairi husika uwe Ali[7]:

> Maudhui yakijengwa kwa hisia za woga hujenga mwendo wa polepole, kwa sababu maudhui hujengwa kwa hisia nzito zenye kuibua huzuni, uzito unaozungumzwa hapa ni uzito wa lile analolizungumzia mwandishi kwa mfano dhulma, unafiki na unyanyasaji.

Mtafiti amepata maana kwamba mtunzi wa shairi hubuni maudhui ambayo humfannya hadhira kuibua hisia zitakazomfanya msomaji kumuamsha kifikira na kusoma kwa kuzingatia uzito wa maudhui hasa ikiwa ya tanzia, huzuni au majonzi yaliyotumika. Maudhui haya huibua hisia za woga msomaji anaweza kulihusisha tatizo analolisoma na yeye kwa muda huo. Hivyo msomaji husoma taratibu kutokana na hisia. Hoja hii inathibitika kwa kupitia diwani ya *Kimbunga*, katika shairi la *Hili Mnatutakiya* linalosema:

*Wakijua una pesa, nyumbani watakujiya*
*Usiku wa saa tisa, ndani kukuingilia*
*Mara wakakukabasa, na vyako kuangamiya*
*Hukuna watendewalo, ndipo wakapamba moto.*

*Umekuwawasiwasi, kupita katika njyia,*
*Wezi wenda kwa vikosi, wapitao kuviziya*
*Yoyote hawatohisi, ghafla humvamiya*
*Hukuna watendewalo, ndipo wakapamba moto (uk:18-19)*

Beti mbili zinaelezea tanzia ya janga la wezi wanaowaibia watu, janga hili huibua mwendo wa polepole kutokana na kufanya hisia za hofu kwa msomaji. Msomaji huibua hisia za woga pale anapojenga picha ya wezi kuvamiwa majumbani na kuiba, kundi la wezi wenye kuvizia watu na kuvichukua vitu vya watu.

Utafiti umebaini kuwa maudhui ya furaha kwa kawaida huwa yanaibua mwendo wa shairi wa harakaharaka kutokana na wepesi wa maudhui kufahamika na mwandishi kutia taharuki baina ya tukio la kwanza na la pili. Msomaji au msikilizaji huvutiwa

[7] Mwalimu Ali Mwalim ni mhadhiri wa taaluma ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na mahojiano na mtafiti yalifanyika ndani ya ofisi yake huko Nkuruma nje kidogo ya mji wa Zanzibar julai 4, 2020.

na kujenga taharuki inayompelekea kupata ujumbe. Hoja inathibitika katika diwaniya *Kimbunga* shairi la *Mpendwa Hapokonyeki* linalosema:

> *Mola ndiye atowaye, akampa mahulukun*
> *Humpa amtakaye, ambae humbariki*
> *Na kila amnyimaye, kupata hatodiriki*
> *Mpewa hapokonyeki aliye pewa kapewa (uk: 35)*

Ubeti unafafanua namna maudhui yaliyoundwa kwa lugha nyepesi na ya kawaida yanavyojenga mwendo wa harakaharaka kutokana na kutumika tukio la wasia wa *Mpendwa Hapokonyeki* tukio lenye ukweli ambao unafikisha ujumbe kwa jamii kubwa. Wakati Salma (khj) anakubaliana na mawazo kama hayo anasema:

> Maudhui shairi mwandishi ameyafumba sana kwa lugha nzito yenye tamathali za semi au taswira zenye visa na matukio mazito ya tanzia bila shaka mwendo wa shairi utakuwa wa polepole.

Mhojiwa ana maana kwamba mtunzi hutunga kazi yake kwa kuifumba kwa kuonesha ubingwa au kuichangamsha hadhira yake. Kwa mfano katika Nadharia ya Upokezi Wafula na Njongu (2007) wakiunga mkono mawazo ya Fish (1980) wanasema kazi za fasihi hufungwafungwa kiasi ambacho hadhira hupaswa kuifungua na kubuni mawazo mapya kutoka katika matini chanzi, hii ni kutokana na msomaji kuwa na jukumu kubwa la kuusaka ujumbe. Hivyo msomaji na msikilizaji inambidi kusoma na kusikiliza kwa kutafakari maudhui ya shairi kwa kina na kufanya uchambuzi wa maudhui kwani waandishi hutumia lugha ya ishara na mbinu nyingine za kisanaa zenye kuhitaji ufafanuzi ili kuufikia ujumbe. Ushahidi wa dai hili unaonekana wazi katika diwani *Kimbunga* ya kwenye shairi la *Vitendwili* linalosema:

> *Kitandawili na tega, natega kiteguweni*
> *Tuguweni bila woga, na kutaja kwa lisani*
> *Paa mayai kataga, katotoa wana nyani*
> *Wateguzi tegueni, moja baada ya moja*
>
> *Kuna yalozidi mno, kuajabisha nyoyoni*
> *Pana wakonge watano, wanashindana kwa fani*
> *Wakata mawe kwa meno, na kujaza matumboni*
> *Wateguzi teguweni, moja baada ya moja (uk:13*

Beti zimeundwa kwa lugha ya ishara iliyounganishwa na maudhui ya taswira ya fumbo msomaji inabidi kuchukua muda kilifumbua kutokana na matukio ya tanzia na

ya ajabu yanayooneshwa katika beti hizo mfano *Paa mayai kataga, katotoa wana nyani, Pana wakonge watano, wanashindana kwa fani* na *Wakata mawe kwa meno, na kujaza matumboni* msomaji anahitaji muda wa kuyafumbua mafumbo hayo, kitendo cha kuchukua muda kufumbua shairi hujenga mwendo wa polepole kwa msomaji na msikilizaji.

#### 4.2.2.6 Uteuzi wa Maneno

Uteuzi wa maneno ni uchaguzi maalumu wa maneno anayoyatumia mtunzi kwa lengo la kutosheleza katika kazi yake anayoitunga na kuifanya yenye kuvutia. Ili shairi likamilike lazima liwe na wingi wa msamiati, uteuzi wa maneno unaotumia maneno ya ishara na taswira ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa (Mulokozi, 2017). Katika kukamilika kwa shairi inategemea uwezo wa mwandishi wa upangaji, uchambuzi, na uchaguzi wa neno au maneno ambayo yanaleta mvuto na hisi wakati wa kufikisha ujumbe alioukusudia. Kutokana na maelezo hayo mhojiwa Masoud[8] anaifafanua hoja ya uteuzi wa maneno kwa kusema:

> Katika uteuzi wa maneno mtunzi wa mashairi huteuwa neno au maneno, kwa mfano mtunzi anapotaka kujenga mwendo wa huzuni hubuni maneno yanayojenga huzuni ili yaweze kutoa huzuni kama anavyotaka, wakati mwengine watunzi huyakata maneno au kuyapunguza kwani ushairi unaruhusu kufanya hivyo na kuunda maneno mengine mapya ili kupata mwendo wa shairi anaoukusudia kwa kutengeneza neno lenye mantiki nzuri ya matumizi katika shairi lake.

Hii ina maana kwamba mtunzi wa shairi huwa na uhuru wa kuamua atumie neno au maneno ambayo yatakamilisha kazi yake ikiwa neno la fumbo au la furaha. Vilevile mtunzi wa mashairi ana uwezo wa kuliunda neno ambalo humfanya msomaji kuchukua muda kulitatua lengo kazi yake iwe na mvuto na hisia za kishairi. Kwa kulishadidia hili Njongu na Chimera (1999) wanasema uteuzi wa maneno humfanya mtunzi kufikiri maneno ambayo yanauwiano na lile wazo analolitaka kuliwasilisha. Kwa mfano mtunzi akiamua uteuzi wa neno au maneno uwe wa mwendo wa polepole, hapana shaka hutumia neno au maneno yanayokubaliana na mwendo huo ili kuvuta hisia za hadhira wake.

---

[8] Dr.Masoud N. Mohammad ni mhadhiri wa Taaluma ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) alifanya mahojiano na mtafiti, Juni 30, 2020 ofisini kwake Nkurumah.

Hapa mtunzi wakati mwingine humwacha msomaji wa shairi kuamua aina ya mwendo kwa mujibu wa uteuzi wake wa maneno anaokutana nao wakati wa kusoma shairi, kama ataamua mwendo wa polepole, wastani au wa harakaharaka. Hoja inathibitishwa kwa kupitia katika diwani ya *Wasakatonge* mwandishi anaonesha uteuzi wa maneno kwa kuliteuwa neno mfano *mtemea mate mbingu,* hoja inathibitika kupitia shairi lifuatalo:

> *Nimeona maajabu, mambo yaliotendeka,*
> *Nikashindwa kuwa bubu, kuamua kutamka,*
> *Tena bila ya aibu, maovu yalifanyika*
>
> *Kutemea mate mbingu, na uso ukainuka,*
> *Na kutumia mizungu, na mikakati kuweka,*
> *Hayavuki hata wingu, chini yataporomoka.*
>
> *Atafute mtefule, kohozi limemshika,*
> *Aujaze mate tele, na mengine kufurika,*
> *Hatapigiwa kelele, hilo linaeleweka (uk:31 )*

Beti hizi zinaonyesha uteuzi wa maneno ambapo mwandishi ameteua neno *mtemea mate mbingu*. Neno ambalo limebeba taswira ya shairi zima na kumfanya msomaji atumie muda wa kufikiri ambayo hufanya mwendo wa shairi kuwa wa polepole. Katika beti hizi mwandishi ametumia lugha ya fumbo yenye maneno mfano, *mtefute,*[9] *mpingo,*[10] *mizungu*[11]. Uteuzi huu wa maneno umepelekea kuibua mwendo wa shairi wa polepole.

Hata hivyo Vuai (khj) kwa upande wake amesisitiza umuhimu wa uteuzi wa maneno kwa kusema:

> Uteuzi wa maneno ni jambo la lazima, mtunzi anapoteua maneno huteuwa kwa mujibu wa maudhui ya tukio lake analolilenga kulifikisha kwa hadhira. Kwa mfano tukio la furaha huliteua neno la furaha na mwendo wa shairi ukawa harakaharaka na maneno aliyoyateuwa yakiwa ya huzuni mwendo utakuwa wa polepole. Kazi ya mtunzi ni kuyavunjavunja maneno ili kupata anachokikusudia na ndani ya uteuzi wake huibua aina ya mwendo wa mashairi kama wa haraka, wastani au polepole.

---

[9] Mtefute ni chombo maalum cha shaba au dhahabu kinachotumika kutemea mate.
[10] Mpingo maana yake ni mti mgumu wenye kiini cheusi hutumika kutengenezea samani.
[11] Ni kiini macho  kinchofanywa ugangani.

Ni dhahiri kuwa katika mashairi uteuzi wa maneno ni jambo lisiloepukika hii ni kutokana na mtunzi kuyatumia maneno hayo katika kuunda maudhui ya shairi. Uteuzi huu hufanywa kwa mujibu wa uzito au wepesi wa maudhui na tukio analolitaka mtunzi kuliwasilisha. Hapa mtunzi anaweza kubadili sarufi ya lugha, kupunguza au kuzidisha maneno ili kuunda neno au maneno na kujenga maudhui anayoyataka. Ushahidi wa hoja hii unaonekana katika diwani ya *Kimbunga* katika shairi la *Punda* linalosema:

*Punda kakosa thamani, sababu vitimbi vyake*
*Milele akawa duni, wala asiheshimikez*
*Wa wake umaluuni, kuvunjiwa hadhi yake*
*Ndivyo tabia ya punda, kurusharusha mateke*
*Kuchunga akikushinda, muwachiye ende zake*

*Punda hakumbuki wema, hata kwa mchunga wake*
*Humpa mwingi mtama, na maji anufaike*
*Katu haiwi salama, shukurani zake mateke*
*Ndiyo tabia ya punda, kurusharusha mateke*
*Kuchunga akikushinda, mwachiliye aende zake (uk:21)*

Beti hizi zinaonyesha uteuzi wa neno *Punda* unavyojenga mwendo wa pole wa shairi kutokana na kutumia neno lenye taswira ya mnyama kufananishwa na binadamu asiyekuwa na fadhila. Hivyo, msomaji ili kufikia ujumbe hutumia mwendo wa pole kutafakari huyu ni punda au kiumbe mwingine asiyefadhilika mwenye vitimbi kama hivi.

#### 4.2.2.7 Mandhari na Wakati

Mandhari ni sehemu au hali ya maumbile yaliyomzunguka mwanadamu na historia yake (Holman, 1986). Katika kazi za fasihi, mandhari zimegawanyika katika makundi mawili: mandhari halisi na ya kubuni. Katika fani ya ushairi, mandhari hutumika kujenga na kuchunga masimulizi ya tukio ambalo mwandishi anataka kulifikisha kwa hadhira yake. Lengo kuu la mandhari ni kuibua hisia za msomaji wakati wa kusoma kwa kumtajia maeneo kama vile miji, vijiji, tarafa, kata, mabonde, milima miti na vinginevyo, lengo la kumuunganisha msomaji au msikilizaji na vitu

hivyo ni kupata urahisi wa kuelewa ujumbe wa mwandishi. Mhojiwa Mberwa[12] anasema kuhusu mandhari:

> Mtunzi huyatumia mandhari kama kiunganishi cha maudhui ya kazi yake na mazingira ya hadhira kwa kumjengea uwezo mzuri wa kufikiri na kupata ujumbe. Mandhari hutumika kuonyesha mwendo wa shairi kwa namna gani mtunzi amekusudia kulifikisha tukio lake kwa harakaharaka au kwa mwendo wa polepole.

Katika kulifafanua hili kazi kubwa ya mandhari ni kusaidia kufahamika kwa maudhui ya kazi ya fasihi. Hivyo mtunzi ana uhuru wa kuyatumia mandhari kwa mujibu wa kazi yake kama alivyokusudia, ikiwa kwa kuyataja tu au kueleza kwa uwazi ili kufikia ujumbe alioukusudia. Kwa mfano mwandishi wa shairi anapotaka kufikisha maudhui yake katika eneo kubwa lenye mazingira yanayofanana (ya pwani) na lake hutumia mwendo wa harakaharaka ili kulibana eneo kwa kumvuta msomaji wa mbali kuwaweka karibu. Kwa mfano katika diwani ya *Kimbunga* mwandishi ametumia mandhari ya visiwani Zanzibar, Dar es Salam na Mikoa mingine ya Tanzania na hata Afrika ya Mashariki. Wasomaji wote hawa wanaposoma hujisikia kama wapo katika sehemu ndogo ya mtunzi. Dai linadhihirika kupitia diwani *ya kimbunga* shairi *Kasa* linasema:

*Zuberi na daruweshi, malinga wa visiwani*
*Hili linanitabishi, nijile kukwambieni*
*Kateni utatanishi, nitoke matatizoni*
*Nataka uweleweshi,mnyama au samaki.*

*Tanga na darisalama, rufiji hata barani*
*Kwa majina nisosema, kwa kuwa siwajuwini*
*Mniondolee dhima, nyote kwa zenu hisani*

*Wenzangu vipi mwasema, mnya au samaki (uk:14-15)*

Beti hizi zinachambua ufundi wa mtunzi wa kuyasana mandhari kwa kuyafumbata na kuonekana kama sehemu ndogo ili kumjengea hisi msomaji wake popote alipo kulisoma shairi kwa mwendo wa kasi kwani msomaji hujihisi kama yupo karibu na

[12] Bw. Mberwa ni Mwanafunzi wa taaluma ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) anasoma ngazi ya shahada ya uzamivu Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Mahojiano na mtafiti yalifanyika Julai, 11, 2020. Katika ofisi yao huko Vuga Mjini Zanzibar.

mtunzi. Mfano ubeti wa pili alipotaja tu sehemu kama Tanga, Dar es Salaam, Rufiji, Bara na asikokujua mtunzi ndani na nje ya Afrika.

Kwa upande mwingine mtafiti alibaini kuwa mara nyingi kipengele cha mazingira hufuatana na wakati hasa wakati wa kutunga kazi za mashairi, hata hivyo mtafiti alibainisha wakati kama ifuatavyo:

Wakati ni muda maalum uliomo ndani ya mazingira ya binadamu unaotumika katika kupangilia utaratibu wake wa maisha na kujenga historia yake. Katika mashairi mtunzi hutumia wakati kwa kuonesha tukio linapoanza, linapoendelea, na hata linapomalizika. Lengo kuu katika kazi ya fasihi ni kutumia wakati kumvuta msomaji kwenda sambamba na tukio analoliwasilisha ili kupata ujumbe. Kutokana na mawazo hayo mhojiwa Mberwa (khj) aliendelea kubainisha wakati kwa kusema:

> Wakati katika mashairi mara nyingi huwakilisha aina ya mwendo wa harakaharaka hii ni kutokana nn sababu kadhaa zikiwemo mashairi hukusanya mambo mengi wakati mmoja, uteuzi wa neno au maneno wenye kutumia lugha ya mkato hii husababisha ukataji wa matukio na kuyafanya kwa ufupi mno.

Mawazo haya yanasisitiza kuwa kipengele cha wakati huchukua jukumu la kuufafanua mwendo wa shairi kuanzia usanaji wa matukio kuelezwa kwa uwazi kwa kutaja kila kitu kuhusiana na tukio na kufanya mwendo wa polepole au kutaja baadhi mambo kwa ufupi huhusisha mwendo wa harakaharaka, utumiaji wa kuoneshwa kwa uwazi wakati husika kwa kueleza mambo kwa uwazi na mpangilio maalumu huibua mwendo wa polepole na kutaja baadhi tu ya mambo husababisha mwendo wa harakaharaka, matendo ya wahusika kuoneshwa harakaharaka hufanya mwendo wa haraka au matendo ya wahusika yakiwa ya kwenda polepole mno mwendo utakuwa wa polepole. Dai hili linaonesha kwa kuchukua mfano wa shairi la *Mwanamke* kupitia diwani ya *Wasakatomge* shairi linalosema:

*Namuona yu shambani,*
*Na jenmbe mikononi,*
*Analima,*
*Mwana mama,*
*Mavuno si yake,*
*Ni ya mume wake*

*Namuna yu nyumbani,*

*Mpishi yu jikoni,*
*Yaya yeye,*
*Dobi yeye,*
*Huna malipo,*
*Likizo haipo,*

*Namuona kitandani,*
*Yu uchi maungoni,*
*Ni mrembo,*
*Kama chombo,*
*Chenye ushawishi,*
*Mzima utashi. (uk: 16)*

Beti hizi zinaonyesha mkusanyiko wa matukio mengi kwa wakati mmoja yanayoonesha ufinyu wa wakati. Kwa mfano mwandishi amechorwa kiwakati kwa kutumia mwendo wa harakaharaka kwa kumchora mwanamke yupo shambani, mara viwandani wakati huohuo yupo kitandani uchi punde yupo mkekani anazaa na tukiendelea yupo pweke anavunjiwa heshima. Kila tukio kati ya yaliyotajwa hapo juu linachukua muda mfupi bila kuelezwa kwa uwazi na linaanza tukio jingine. Hivyo, msomaji hana budi kusoma kwa mwendo wa harakaharaka kulinga na kukimbizwa na mwandishi kwa kigezo cha wakati.

#### 4.2.2.8 Lafudhi

Massamba (2009) anasema lafudhi ni sauti za matamshi ya msemaji wa lugha fulani kutoka jamii moja ambayo huwa kama kitambulisho cha kuijulisha jamii hiyo kutokana na athari za kimazingira. Hapa ikumbukwe kwamba lafudhi inatambulika kuwa ni kipengele kinachojenga mwendo wa mashairi kwa kutofautisha kati ya msemaji wa lafudhi ya sehemu moja na lafudhi ya sehemu nyingine kutumia lafudhi tofauti kimatamshi. Daulati (khj) alisema:

> Lafudhi inatokana na matamshi ambayo kwa muda wote hutokana na usemaji wa lugha mama ya mtu na huwa kama kitambulisho chake. Mkazo wa lafudhi unatokana na lahaja inayotegemea mazingira ya uzawa lugha iliyotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha kazi yake.

Katika kuifafanua lafudhi msomaji mmoja hutofautiana na msomaji mwingine. Nadharia ya upokezi inatwambia kunaweza kutokea hata tofauti za kimaana kutokana na neno linavyotamkwa. Katika kuangalia mwendo wa mashairi unaojengeka kwa kupitia lafudhi huwa kama shairi moja linaposomwa na watu

wawili wenye lafudhi mbili tofauti, kila msomaji husoma kwa mwendo wake. Msomaji aliyetumia muda mchache kusoma shairi lafudhi yake itakuwa ya lugha rasmi na kuufanya mwendo wa shairi kuwa wa harakaharaka na msomaji wa pili aliyelisoma shairi kwa muda mkubwa lugha ya shairi itakuwa ya pili kutokana athari za kimatamshi msomaji huyo ametumia mwendo wa shairi wa polepole.Tukichukua mfano shairi la *Sivui Maji Mafu* kutoka diwani ya *Wasakatonge* linaeleza mkazo wa lafudhi inayotegemea mazingira ya uzawa na lugha iliyotumiwa na mwandishi:

*Uvuvi wa maji mafu, hauna hata tijara*
*Samaki wake hafifu, hawana ila hasara,*
*Ni kazi ya usumbufu, wavuvi mnatukera,*

*Kuvua pono na tasi,na kauzu toratora,*
*Vikolekole vepesi,ni kitoweo uchwara,*
*Vijipweza na vingisi, kwangu si vyakula bora.*
*Kiitikio*
*Sijavua maji mafu,kwa kitoweo nilacho,*
*Bahari kuu si hofu, kufata nikitakacho.(uk:33)*

Beti hizi zinaonyesha mazingira ya pwani kwa wakazi wa mazingira ya pwani, msomaji wa mashairi wa mwambao wa Afrika ya Mashariki anaweza akalisoma kwa mwendo wa harakaharaka kwa kutumia muda mfupi kutokana na uzoefu wa mazingira ya uvuvi na kuwa na lafudhi za matamshi zenye kuruhusu mwendo wa shairi wa harakaharaka. Lakini kwa mtu wa nje ya mazingira ya mwambao akitakiwa alisome shairi kama alivyolisoma mtu wa mwambao kwa muda uleule hushindwa kutokana na athari za kimatamshi, ni vigumu kulimaliza kwa wakati na mwendo wake utakuwa wa polepole kwake.

#### 4.2.2.9 Maghani

Maghani ni kipera cha ushairi kinachotumiwa kughana shairi kwa kutumia kalima ya maneno badala ya kuimbwa. Maghani hutumia lugha ya kishairi wakati wa kuwasilishwa kwake. Msomaji wa shairi ughanaji wake ndio unaotoa kalima ya maghani ya shairi. Maghani yanaweza kufuatanisha maghani na ala za muziki au kughani kwa mdomo mtupu (Wamitila, 2003). Hii ina maana kwamba katika kusoma mashairi kughani ni jambo la msingi kwani maghani hutoa hisi za kishairi ambazohumvuta msikilizaji kufikia ujumbe wa shairi. Maghani kazi yake ni

kuboresha shairi hasa akipatikana mghani mzuri wa shairi. Kipengele hiki kimedhihirishwa na mahojiano yaliyofanywa na mtafitiwa Omar[13]:

> Msomaji wa shairi wakati wa kughanihuonesha tofauti kubwa kati ya msomaji mmoja na msomaji mwingine hata kama maudhui ya shairi yatakuwa sawa na beti sawa, hii ni kutokana na kigezo cha muda na sauti kila mmoja atachukuwa muda wake wa kughani.

Katika maelezo haya Omar ana maana kuwa kughani kunategemea kipaji cha msomaji na taaluma ya mwendo. Mara nyingi katika kiimbo na maghani mwendo wa shairi hupimwa kwa kutumia sauti za wasomaji si mara nyingi wasikilizaji kuzingatia ujumbe wa shairi husika Msomaji hutumia sauti yake kughani shairi kwa aina zote za mwendo. Katika kuunga mkono jambo hili Nadharia ya Upokezi inadokeza kuwa "….kuna tofauti za upokezi katika usomaji kwani wapo wasomaji wanaosoma vizuri na wanaosoma vibaya" (Jane Tomkins, 1980). Hapa ana maana kuwa hakuna uwiano wa moja kwa moja katika usomaji, tofauti hii husababisha kuibuka kwa watu wawili katika shairi moja kulighani kwa mwendo tofauti. Hii ni kutokana na msomaji ana dhima ya kuamua aina ya mwendo wakati wa kuliwasilisha shairi kulingana na uwezo wake.

Aidha, Momanyi na Maitaria (2013) Kwa kutilia mkazo wazo hili wamesema

> Shairi lenye mpangilio maalum wa maneno huweza kughanwa kwa kutumia mahadhi yaliyounganishwa na ridhimu za aina tofauti ambazo matokeo yake shairi hilo husomwa kwa kutumia mapigo ya muziki.

Wataalam wana maana kwamba umbile la shairi limeumba maalum kwa ajili ya kuimbwa katika kufikisha ujumbe. Juhudi za waandishi katika upangaji wa sauti hupelekea mapigo ya kimuziki ambayo huibua aina za mwendo kwa kutegemea uwezo mzuri wa msomaji au mghanaji wa shairi na aina ya wazo la furaha au tanzia. Haya yanadhihirika katika kuonesha tofauti ya ughanaji katika diwani ya *Wasakatonge* shairi la *Tutabaki Wawili* linalosema:

*Nakupenda peke yako, humukatika dunia,*
*Mwingine tena hayuko, mapenzi kukufikia,*
*Pendo langu liko kwako, daima litabakia,*

[13] Dr. Omar Salum Mohamed ni mhadhiri wa Taaluma ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) alifanya mahojiano na mtafiti, Julai 13, 2020 ofisini kwake Nkurumah Zanzibar.

*Hakuna wa kulizima, pendo langu kufifia,*
*Litabakia daima, na kwako kusehelea,*
*Hadi siku ya kiyama, pendo litaendelea,*
*Kiitikio*
*Dua yetu ya manani, twaomba iwe kubuli,*
*Dunia nyingine haiko, ili tubaki wawili(uk: 26)*

Beti hizi zinaonyesha maghani namna yanavyojenga mwendo wa shairi, maghani hujenga aina ya mwendo kwa mujibu wa kipaji cha msomaji anataka azisome beti hizo kwa mwendo wa pole wastani au harakaharaka kutokana na shairi kubeba mahadhi ya aina zote. Kwa kuongezea mtafiti baada ya mahojiano, mhojiwa alibainisha kuwa maghani hayana tofauti kubwa na kiimbo. Katika mahojiano hayo mhojiwa Nadhra[14] alisema:

> Kiimbo kinategemea cha msomaji kutumia mawimbi ya sauti wakati wa kusoma shairi huwa anaweza kupandisha na kushusha ili kutafuta mahadhi yatakayo mliwaza msikilizaji wake na kufikia ujumbe. Hapa kinachozingatiwa ni mahadhi na sauti ya msomaji.

Hapa mhojiwa alikuwa na maana kwamba msomaji wa shairi anapaswa kutumia viimbo kwa kuhusisha mwendo wa shairi, na kwamba viimbo hutumika kwa kupandisha sauti na kushusha kwa kutumia mahadhi yanayokwenda sambamba na shairi ili kufikia ujumbe. Kwa mfano mwendo wa harakaharaka msomaji hutumia sauti yake kuipandisha na kuishusha kwa kasi wakati wa kusoma shairi. Mwendo wa wastani msomaji huipandisha sauti kwa kiasi na kuishusha kwa kiasi kidogo ukilinganisha na mwendo wa harakaharaka. Mwisho katika mwendo wa pole msomaji hupandisha sauti na kuishusha kwa utaratibu mno. Hii itambulike kwamba katika matumizi haya kiimbo katika mashairi ya Kiswahili yapo lakini kwa mashairi hayo yanasomwa kwa shughuli gani. Hoja inathibitishwa kupitia katika diwani ya *Kimbunga* tukichukua shairi la *Vijana wa Zanzibar* linalosema:

*Sikiyeni nawambiya, vijana wa Zanzibar*

*Mambo mnojifanyia, wazazi twatahayari*
*Mabangi kujivutia, yanaondoa nadhari*
*Mila zetu za fahari, wacheni kuzipotosha*

[14] Nadhra Haji Ussi ni mwalimu wa skuli ya sekondari Vikokotoni mjini Zanzibar, ni mtaalamu wa fasihi ya Kiswahili. Mahojiano yalifanyika nyumbani kwake tarehe Julai, 14, 2020.

*Mwawachayenu ya hapa, ambayo yalo mazuri*
*Kutii na kuogopa, mwaona hakuna kheri*
*Mwayavamia kwa pupa, kwakedi na ujeuri*
*Mila zetu za fahari, wacheni kuzipotosha. (uk: 25)*

Beti hizi zinaonyesha kiimbo kinavyojenga mwendo wa mashairi. Mwendo kupitia kiimbo msomaji husoma kwa kupandisha sauti na kuishusha wa sauti ili kutimiza lengo la kusoma kwake. Ikumbukwe kuwa katika beti hizi msomaji mmoja kwa kutumia viimbo anaweza kutoa aina zote za mwendo, kinachozingatiwa ni uzoefu wa msomaji tu.

### 4.2.2.10 Taswira

Taswira ni aina ya lugha inayotumika kuchora picha za vitu, wazo au mazingira ya mahali kwa kutumia ishara maalum. Taswira kazi yake kubwa ni kumfanya hadhira apate hisi zilizomo ndani ya kazi ya fasihi kwa kutumia viungo vya hisia (Senkoro, 1982). Neno au maneno ya taswira hupangwa kwa utaratibu maalum na kuundiwa picha ya kitu kwa kutumia lugha ya ishara fulani itakayomfikirisha msomaji katika kufikia ujumbe. Katika mahojiano yaliyofanywa kati ya mtafiti na mtafitiwa Vuai (khj) alisema

> Taswira inaweza kujenga mwendo wa shairi, kwanza taswira ni picha ya ghaibu (iliyofichikana) ili kuiweka wazi inahitaji tafakuri ya kutosha. Katika kufikiri huku hujenga dhana ya aina ya mwendo aidha wa polepole au wastani.

Maelezo hayo yanamaanisha kuwa taswira ni fumbo linalohitaji ufumbuzi, katika kufanya ufumbuzi msomaji au msikilizaji hubuni picha akilini ambayo itawiana na maelezo ya mtunzi, hivyo, msomaji au msikilizaji huweza kuibua aina ya mwendo wa shairi kutokana na tafakuri nzito, mara nyingi mwendo huwa wa polepole hii ni kutokana na sifa ya taswira kumfikirisha mtu na mara chache hujitokeza mwendo wa wastani taswira inapokuwa si funge sana.. Haya yanadhihirika wazi katika kitabu cha *Wasakatonge* katika neno Ging'ingi ambayo ni dhana ya kufikirika tu kwa hiyo msomaji wa mashairi inambidi kulimakinikia ili kupata maana husika. Dai hililinathibitika katika diwani ya *Kimbunga* katika shairi la *Uchawini (*uk:11) linalosema:

*Nilipokwenda Ging'ingi, hukoniliyoyaona*

*Kuna watu moja rangi, sura zashabihiana*
*Bali hayana msingi, wanayofanyiziana*
*Haweshi kusokotana, kila moja ni yeye*

*Wakaao mkumbizo, hujigambandio ana,*
*Na walo mkokotezo, hudai ndio vinana*
*Inavuruga mawazo, ukifikiria sana*
*Haweshi kusokotana, kila moja ni yeye*

*Yalio huko na huko, yametafautiana*
*Milele kuna usiku, hakuingii mchana*
*Ng'ombe humwita kuku, kwa huku lake jina*
*Haweshi kusokotana, kila moja ni yeye (uk:1)*

Beti hizi zimejenga taswira ya *Ging'ingi* hivyo msomaji wa shairi inambidi kujiuliza maswali mengi kuhusiana na neno *Ging'ingi* kwa mfano *Ging'ingi* ni nini? iko wapi? nani wahusika wake?, kwanini haionekani? na mengineyo ambayo baadaye anaweza kugundua. Hivyo msomaji inambidi kufikiri ili kupata picha kamili, na kujenga mwendo wa polepole wa shairi na ikiwa amebobea kifasihi huweza kulifumbua fumbo la *Ging'ingi* kwa mwendo wa wastani.

#### 4.2.2.11 Kibwagizo

Kibwagizo ni mstari unaokaa mwisho wa ubeti wa shairi na wakati mwingine hurudiwarudiwa kila ubeti kwa lengo la kusisitiza ujumbe (Masinde, 2007). Utafiti umegundua kuwa kibwagizo hutumika, hasa katika ujenzi wa takriri kwani usomaji wa kibwaizo ni tofauti na usomaji wa mishororo ya juu ya shairi ambayo kwa mkabala huu wa usomaji tofauti wa kibwagizo ndio hutumika kuonyesha mwendo wa mashairi katika kibwagizo. Kazi kubwa ya kibwagizo hutumika kama kiitikio ambacho hufichua fumbo la mwandishi la huzuni au furaha kwa hiyo msomaji huonesha hisia tofauti ya usomaji wake ili kufikia ujumbe. Nadhra (khj) anasema kuwa kibwagizo hubeba dhima ya mwendo wa shairi kwa kutegemea hisia za msomaji wa shairi. Kibwagizo cha huzuni kinajenga mwendo wa polepole na atakisoma kwa sauti iliyojaa huzuni. Mahadhi ya kibwagizo mara nyingi huonesha upole unaongozwa na sauti za huzuni.

Wakithibitisha hili Momanyi na Maitaria (2013) wanasema msomaji wa shairi hulisoma shairi kwa mwendo wa polepole kuanzia mistari ya juu hadi kwenye mstari wa kibwagizoanapofika mstari wa kibwagizo huonesha msisitizo wa toni za hisia za

huzuni. Wataalamu hawa wanaona kuwa ni muhimu kwa msomaji anapokisoma kibwagizo kuonesha hisia ambazo zitalingana na wazo la shairi likiwa la huzuni kibwagizo kitabeba hisia za mwendo wa huzuni. Madai haya yanaonekana katika shairi la "Kimbunga" kupitia kibwagizo cha 'nyoyo zimefadhaika" (uk: 1) linadhihirisha hoja hii:

Kunakikonge ajuza, viumbe kinawateka
Hicho kina miujiza, kila rangihugeuka,
Watakao kiendekeza, hilaki zitawafika
Nyoyo zilifadhaika

Katika ubeti huu mstari wa mwisho uliopigiwa mstari ni kibwagizo, kibwagizo huonyesha mwendo wa shairi wa polepole kwa hapa. Msomaji anapomalizia huonyesha kwa kuishia kwa sauti ya hisia za upole. Hapa hupatika na mwendo wa polepole kutokana na huzuni katika maudhui aliyoyapata msomaji wakati wa kusoma mishororo ya juu ya ubeti. Msomaji wakati anafika katika kibwagizo humalizia kwa kuashiria hisia za furaha na raha na kukata sauti za vina kwa kuonyesha mwendo wa harakaharaka. Akionesha kuunga mkono mawazo haya Momanyi na Maitaria (2013) wanasema kibwagizo ni muhimu kwa kuwa ndicho kinachobeba hisia za msomaji na msikilizaji wakati wa kukisoma ua kukisikiliza. Kwa mfano maudhui ya shairi yanayowasilishwa yakiwa ya furaha, msomaji wa shairi atasoma mishororo ya juu kwa mwendo wa kasi hadi mshororo wa mwisho hapa msomaji hupata hisia za furaha. Haya yanaonekana wazi katika mfano katika diwani ya *Wasakatonge* shairi la *Tutabaki Wawili* kibwagizo kinachosema:

*Nakupenda peke yako, humukatika dunia,*
*Mwingine tena hayuko, mapenzi kukufikia*
*Pendo langu liko kwako, daima litabakia,*

*Hakuna wa kulizima, pendo langu kufifia,*
*Litabakia daima, na kwako kusehelea,*
*Hadi siku ya kiyama, pendo litaendelea,*
***Kiitikio***
*Dua yetu ya manani, twaomba iwe kubuli,*
*Dunia nyingine haiko, ili tubaki wawili.(uk: 26)*

Katika beti mbili hizi mistari miwili ya chini iliyopigiwa mistari ndio kibwagizo, beti zinazungumzia maudhui ya furaha kwa msomaji anapomalizia kwa kuonyesha furaha, hivyo mtindo wa usomaji wa kibwagizo hiki unaibua mwendo wa

harakaharaka kutokana na msomaji kuwa na hisia za furaha kwa kuamini kuwa hakuna wa kulizima pendo lao.

### 4.3 Dhima za Vipengele Vinavyojenga Mwendo wa Shairi

Sehemu hii inafafanua dhima za vipengele vinavyojenga mwendo wa shairi. Mjadala umefanyika na kuibua dhima mbalimbali zikiwamo kutia hamasa za usomaji, kuibua hisia kwa wasomaji, kupendezesha mtu kusikiliza, kumpa uhuru mtunzi, kudhihirisha matumizi ya takriri, kujenga uwezo wa kufikiri, kuibua taharuki, chanzo cha kuibua maudhui, kuweka wazi nafasi ya mahadhi, kuonyesha upekee wa mwandishi, mwendo kama kipengele cha kifani. Utafiti umebaini dhima hizo na kuonyesha ufafanuzi wa kila dhima na aina ya mwendo wa shairi unavyofanyika kwa kila dhima kama ifuatavyo:

#### 4.3.1 Kufikisha Ujumbe

Ujumbe ni maono ya mwandishi ambayo hupatikana baada ya kusoma kazi ya fasihi (Jilala, 2016). Kwa ufupi kila kazi ya fasihi huwa na ujumbe ambao amemlenga hadhira kuupata kama alivyokusudia mwandishi. Nadharia ya upokezi kwa kulisisitiza wazo la ujumbe wanasema "…kazi ya fasihi inatoa ujumbe kama inavyoichukulia hadhira na kwenda sambamba na lengo la mwandishi (Senkoro, 1999) Tukumbuke kuwa msingi mkuu wa kazi ya fasihi ni kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Hata hivyo kitu muhimu kinachojenga ujumbe ni fani na maudhui vinapouunganishwa na dhamira kuu na dhamira ndogo ambavyo hujenga ujumbe. Katika kuufafanua ujumbe mhojiwa Masoud[15] anasema:

> Mashairi ni maneno mazito yanayogonga nyoyo za hadhira. Kwa hiyo, dhima yake kubwa ni kufikisha lile alilonalo mwandishi. Mwendo wa shairi utamuelekeza hadhira kule anakokutaka mwandishi aifikishe hadhira yake kwa nguvu, kasi, uzito na namna ile ile aliyokusudia mwandishi kuifikisha kwa hadhira hiyo. Mwandishi anapotaka kutia hamasa, tanzia, jazba, au furaha mwendo wa shairi utamsaidia mwandishi kuyafikisha mambo hayo kama anavyokusudia kwa kila moja kulifikisha kwa msomaji wake kwa mwendo anaoukusudia.

[15] Dkt. Masoud N. Mohammad ni mhadhiri wa Taaluma ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) alifanya mahojiano na mtafiti, Juni 30, 2020 ofisini kwake Nkurumah.

Maelezo haya yanamaanisha kuwa watunzi wa mashairi hujitahidi katika uteuzi wa maneno ili kuunda hisia tofauti zinakazowafanya wasomaji na wasikilizaji kuibua hisia za tanzia, jazba au hata furaha, mwendo wa shairi ndio unaotumika kufikisha ujumbe huo kwa hadhira yake. Kwa mfano mwandishi wa diwani ya *Kimbunga* anakusudia kufikisha ujumbe kwa kutoa nasaha kwa umma walipe madeni yao. Nasaha zimetolewa kwa mwendo wa harakaharaka kutokana na lugha iliyotumika na uzoefu wa tukio linalosumbua jamii kubwa. Hoja inathibitika katika diwani ya *Kimbunga* katika shairi la *Dawa ya Deni Kulipa* linalosema:

*Deni lipa kwa hiari, upate kuaminiwa*
*Usijifanye ayari, hivyowajitia dowa*
*Lazima utafakari, hakuzozi kuzidiwa*
*Huwezi kuaminiwa, kama hukujiamini (uk:32)*

Ubeti huu unazungumzia jazba, hamasa, za kumfaya msomaji au msikilizaji kufanya hima ya kulipa deni. Kutokulipa madeni ni tatizo la watu wengi, kutolipa deni ni kujitia doa na kutoaminika maishani. Hivyo, msomaji anaweza kusoma shairi kwa kutumia mwendo wa harakaharaka kutokana na uzoefu wa tukio na lugha iliyotumika ni nyepesi. Vilevile Ali (khj) alishadidia hili kwa kusema:

> Mwendo wa shairi una dhima ya kumpa uhuru mtunzi pale anapotunga kazi yake, kuitunga kwa uhakika na kujua atumie mwendo wa aina gani katika shairi lake. Kwa mfano mwandishi akitaka kufumba hutumia maneno ya mafumbo na kumfaya msomaji kupata ujumbe kwa mwendo wa polepole.

Maelezo haya yana maana kwamba, ili kufikisha ujumbe kwa hadhira, mtunzi lazima awe na uhuru wa kutosha katika kutunga kazi yake. Uhuru humpelekea kuamua kuifumba kazi yake kwa kuzingatia uwezo wa hadhira kwa kutumia lugha nzito, mara nyingi ujumbe utakawia kufika kutokana na uzito wa maudhui hayo. Ili ujumbe uweze kufika inategemea muumano wa lugha na tukio linalozungumzwa pia jamii wanalipokeaje tukio hilo. Tukiangalia shairi ambalo mtunzi amekusudia kufikisha ujumbe kwa haraka katika diwani ya *Kimbunga* shairi la *Bahati* linalosema:

*Kama nitahiyarishwa, penye viwili teuwa*
*Mali nikiamrishwa, au bahati chukuwa*
*Sitongoja kuonyeshwa, bahatinita nyakuwa*
*Bahati ni kitu bora, kiumbe akijaaliwa*
*Ijapokuwa fukara, yake hwenda kwa muruwa (uk: 36)*

Ubeti huuunachambua namna mwendo unavyofikisha ujumbe kwa haraka. Hii ni kutokana na kwamba ubeti huu, umetumia lugha nyepesi na tukio linalozungumzwa linapelekea kuzusha mjadala wa kipi bora mali au bahati. Msomaji anapolisoma huwa tayari ameshakaa upande mmoja hiyo hupelekea taharuki ya kujua kitu gani ni bora. Katika muktadha huu ujumbe hufikishwa kwa maneno ya mtunzi na namna ya msomaji anavyolisoma shairi hulazimika kulisoma kwa mwendo aliokusudia mwandishi na mhakiki kuweza kukipa haki kila kitu anachokiona ndani ya maandishi. Mhakiki anavyoweza kivihakiki vitendo kama kukunja uso, kulia, kucheka, kuigiza ndivyo na mwendo unavyofanyika harakaharaka au polepole. Hoja hii inadhihirika wazi katika diwani *ya Wasakatonge* katika shairi la *Wafadhiliwa* shairi linasema:

*Nisera kunakamishwa,*
*Umma wote kuatilishwa*
*Shida na dhiki kuvilishwa*
*Taabani (uk: 39)*

Ubeti huu unaonesha utendaji wa kuigiza matendo yaliyomondani ya ubeti huo,kwa mfano neno *kunakamishwa* msomaji atafunga mikono yake kwa alama ya kuonesha hakuna kitu. Pia neno *umma wote* huifanya mikono ya duara, *shida na dhiki* huonesha kukunja uso au hata kuliana neno *taabani* msomaji huweka mkono wake kidevuni na kuonesha kuonewa. Hivyo, msomaji wa shairi hufanya vitendo vyote hivi na bila shaka mwendo wa shairi utakuwa wa polepole au wastani.

Sambamba na hilo mtafiti amebaini kuwa, ujumbe mara nyingi hufika kutokana na taharuki ya msomaji na msikilizaji kukipenda kile anachosikiliza au anachokisoma kiwe kinawiana na utashi wake, kikiwa kinaendana hukisoma kwa mwendo wa harakaharaka kutokana na hisi alizozipata wakati wa kusoma shairi. Kwa mfano msomaji anaposema shairi *itowe kauli yako* hukumbuka sauti ya *muhibu*[16] wake na kumsukuma kusoma kwa haraka. Dai hili linathibitika kwa kupitia diwani ya *Wasakatonge* katika shairi *Itowe kauli yako* linasema:

*Itowe yako sauti, kama kweli wanipenda,*
*Niweze kujizatiti moyo uondke funda*
*Nazidi kukuzibiti sikuachi hata nyanda*

[16] Muhibu ni mpenzi anayependwa ndani ya roho ya mpendaji

*Itoweyako kauli itamke bila inda*
*Itekeleze miadi bila ya kufanya inda*
*Na mola awe shahidiyakuwa utajilinda (uk:27)*

Beti hizi zinachambua taharuki ya kupenda kile anachokisoma na kusoma kwa haraka ili kufikisha ujumbe, hapa ujumbe utafika kwa mwendo wa harakaharaka kwa sababu ya hisi alizozipata msomaji zinamsukuma kusoma kwa haraka wakati wa kusoma shairi.

### 4.3.2 Kutoa Hamasa katika Usomaji

Msomaji kwa kawaida hupata hamasa ya usomaji kutoka na kile anachokisoma na anahisi kitampatia ujumbe utakayomnufaisha katika maisha yake. Kitu kinachomtia hamasa msomaji na msikilizaji ni vionjo vya kifani kama vile tamathaliza semi, taswira, semi na vinginevyo, ambavyo huvitumia ili kuichapuza kazi yake na kumfanya msomaji kuwa na hamu ya kuendelea kusoma hadi kupata ujumbe. Katika kumpa hamasa msomaji mwandishi anapaswa kuzingatia namna anavyomhamasisha kwa kutumia mwendo wa shairi unaolingana na maudhui anayoiwasilisha. Bi Aminia (khj) anasema:

> Msomaji atapofuata mwendo wa shairi kama alivyokusudiwa mwandishi kwa uzito au wepesi wa aina ya mwendo wa shairi alioukusudia mwandishi husaidia kupata hamasa na hamu ya kuendelea kusoma hadi mwisho wa shairi na kuibua ujumbe.

Hapa mhojiwa ana maana kwamba kufanikiwa kwa msomaji kwa kufanana mawazo yake na maudhui anayoyafahamu mwendo wake mara nyingi hufanya bidii na pupa katika usomaji ya kufukuzia mwisho wa kisa ili kufikia ujumbe, hivyo usomaji wake utakuwa harakaharaka. Vilevile msomaji huwa na hamasa ya kusoma kazi nyingine zenye mwendo tofauti kwa kuamini kuwa watamudu kupata ujumbe kama ulivyoksudiwa na mwandishi. Msomaji huingia hamasa wakati mwingine kwa kukiona tu kichwa cha shairi mfano *Nilikesha* katika mawazo yake hubuni aina ya mwendo wa shairi na kujiuliza kwanini akeshe? Msomaji anapofanikiwa kwenda sawa na mwendo alioukusudia akilini kabla hamasa huongezeka na kuzidisha kasi ya usomaji zaidi. Dai hili linathibitika katika diwani ya *Wasakatonge* katika shairi *Nilikesha*, shairi hili ni la mwendo wa harakaharaka. Shairi linamtia jazba msomaji kusoma kwa kasi kujua kwanini mwandishi alikesha? Shairi linalosema

*Nilikesha ,*
*Kwa usiku uliorefuka*
*Kihesabu kila dakika,*
*Mapigo ya moyo kusikika,*
*Usiku wa maruirui,*
*Sababu mliwaza wangu,*
*Niklikesha*
*Kusubiri yetu miadi,*
*Uwe usiku wa kufaidi,*
*Kwa kuitekeleza ahadi,*
*Nikakusubiri kwa hamu,*
*Kwa shauku na tabasamu (uk: 23)*

Beti zinaonyesha hamasa kwa msomaji baada ya kuona tu kichwa cha shairi na akaweza kabaini ukweli kama alivyofikiria hamasa za mwendo wa kasi zitaongezeka kwa kusaka sababu za kwanini akeshe? na ilikuwaje baada ya kukesha? katika kufikia ujumbe.

### 4.3.3 Kuibua Hisia kwa Wasomaji

Ili shairi liwe na uzito kisanaa lazima liwe uwezo wa kugusa hisia za hadhira ndani ya nyoyo zao wakati wanapolisikiliza shairi na litoe maana yenye mvuto. Kama Abdulltif abdalla (1983) anavyomalizia maana yake mwisho kwa kusema "...shairi lazima liathiri masikio kwa kusikia na lenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ulivyokusudiwa". Msikilizaji huibua hisia za mwendo wa shairi pale anapoguswa na tukio fulani liwe la furaha au la huzuni na kufanya mwendo wa harakaharaka kwa tukio la furaha na mwendo wa polepole kwa tukio la huzuni. Ali (khj) anasema:

> Wasomaji wa mashairi hupatwa na hisi za ndani wakati wa kusoma shairi pale atapoufuata mwendo wa mshairi uliomo ndani ya maudhui ipasavyo. Hisia hujengeka kwa kuufahamu mwendo wa shairi na kuhusianisha na taaluma ya msomaji.

Hii ni kusema kila aina ya mwendo hutoa hisia ambazo humsukuma msomaji kufuata kwa mujibu wa taaluma yake, maelezo yanafafanua maana kwamba maudhui mazito ya kisiasa hugusa hisia za uzalendo huling'ang'anua shairi kwa mwendo wa polepole kwa kulirudiarudia hadi kuifikia maana. Kama Nadharia ya Upokezi inasema "…kurudia kusoma kazi ya fasihi humuezesha msomaji kugundua mambo yaliofichikana…" Mara nyingi ili msomaji au msikilizaji aweze kufahamu vizuri wazo la mtunzi inambidi arudie tena na tena. Hoja hii inathibitika katika shairi la

*Vinyonga* linahitaji kufikiri na kuvuta hisia za uzalendo katika diwani ya *Wasakatonge* linasema:

*Mlipuko,*
*Umetukumba,*
*Vimeleya vinyonga,*
*Kama vile vimeleya,*
*Hatari kwa jumuiya,*
*Itakuja angamiya,*
*Hatuaispochukulwa,*
*Maangamizi (uk: 49)*

Beti inazungumzia masuala mazito ya kisiasa kwa mwendo wa polepole wenye kuhitaji tafakuri katika kuibua hisia zilizomo ndani ya ubeti. Hivyo, msomaji baada ya kuguswa na maudhui yaliyomo ndani ya shairi huibua hisia ambazo zitamfanya aibue mwendo, mfano hisia za tanzia mwendo utapungua na kuwa wa polepole na hisia za furaha mwendo utakuwa wa harakaharaka kwani msomaji huwa na haraka ya kufukuzia mwisho itakuwa vipi. Hoja inadhihirika katika shairi la *Si Wewe*. Msomaji hujisikia kama yeye na humfanya asome kwa harakaharaka mno. Shairi linalosema:

*Nilipokutupia mshipi,*
*Ukashindwa kujizuia,*
*Nikakuchmbuza,*
*Ukanifuata*
*Kwa makeke na vishindo,*
*Si wewe.?*

*Umeshapwelewa nchi kavu,*
*Wako werevu umekwisha,*
*Sasa unatweta,*
*U taabani,*
*Ni wewe ulo mlafi*
*Si wewe? (uk: 21)*

Beti mbili hizi zinaelezea dhima ya mwendo katika kuvuta hisia za msomaji, msomaji anaposoma beti za aina kama hii huibua hisia za ndani zitakazo msukuma msomaji kusoma kwa mwendo wa harakaharaka na kwa furaha na kujisikia ni mshindi baada ya kuguswa maudhui husika. Katika kazi ya fasihi mtunzi jambo analoliangalia kwa karibu ni hisia za msomaji wake kwani msomaji ndie muamuzi au mlengwa anaefikishiwa hisia hizo kwa ajili ya kufanya mabadiliko. Hata hivyo, hisia

katika mashairi mtunzi hujengwa kwa uteuzi maalum wa maneno, kuangalia jamii inataka nini kwa wakati huu atafanya haya kwa mujibu wa maudhui na mwendo gani wa shairi ili zifike kama alivyokusudia. Kwa mfano wa hisia za furaha, tanzia, majonzi na hisia sauti, kila aina kati ya hizi huzifuatanisha na hisia za mwendo wake.

Tukichukulia mfano haya mambo yaliyoingia siku hizi wa kubakwa wanawake na watoto ni matukio ya kitanzia mwendo wa shairi utaibua hisia kali za kusisimua na kuufanya msomaji kusoma kwa mwendo polepole hasa kama amefanyiwa jamaa yake wa karibu. Dai linnaonekana katika diwani ya *Wasakatonge* katika shairi la *Unyama* linalosema:

*Binadamu hana aibu,*
*Ni kawaida kubaka,*
*Wasichana kunajisi*
*Wavulana kulawiti,*
*Muflis wa maadili*

*Binaadamu mmiliki,*
*Anefuga majini,*
*Kuyatukia mahsetani*
*Kuongea mizimun*
*Na kuwazuru (uk: 47)*

Beti zinaonyesha mjonzi ya balaa la kubakwa kwa wanawake na watoto wa kiume kulawitiwa. Binadamu huyu pia mrogaji na ushirikina bila ya aibu. Msomaji huibua hisia kali za majonzi na kumfanya asome kwa mwendo wa polepole hasa kama matukio haya yamemkuta au kuwakuta jamaa zake wa karibu.

#### 4.3.4 Kumpendezesha Mtu Kulisikiliza au Kusoma

Mtu hupendezwa na shairi kutokana na maudhui au sauti ya msomaji anayoipata wakati wa kusikiliza. Katika kusikiliza mashairi msikilizaji hupendezwa na mengi, mfano sauti ya anayeghani shairi, vitendo anavyovifanya msomaji, namna ya usomaji wake wa shairi, ujumbe anaopatikana ndani ya shairi na megineyo. Omar (khj) anaeleza kuwa:

> Mwendo una dhima kubwa ya kumpendezesha mtu kulisikiliza shairi. Msomaji wa shairi, hasa akiwa mweledi wa kusoma mashairi humvuta msikilizaji na kumfanya awe makini kimwili na kiakili. Ukikosekana mwendo mzuri wa shairi msomaji au msikilizaji

> hulitupia mbali shairi. Pia msikilizaji hupendezwa na aina ya mwendo wa shairi na aina ya mahadhi mahadhi. Kwa mfano kama wasikilizaji wao wanapenda mwendo wa haraka lisomwe shairi limalizike na wengine wanapenda mwendo wa shairi wa polepole kwa sababu katika kupenda mwendo wa shairi kunategemea sampuli ya mtu au watu wa mashairi au si mtu wa mashairi. Ikiwa si mtu wa mashiri huona kila kitu sawa lakini mtu wa mashairi huwa mchaguzi wa aina ya mwendo.

Hata hivyo hisia za mtu kupendezwa zinakuja kulinga na wazo linalotumbuizwa kwa kupitia msomaji aliyebobea kusoma mashairi vizuri, lafudhi nzuri za kishairi, na pia mahadhi yenye kupendeza. Haya humfanya msikilizaji kuwa makini hasa akiwa mweledi wa mashairi.Tukiangalia katika diwani ya *Wasakatonge* shairi linalokusudia kumpendezesha mtu ni Shairi la *Nilichelewa kupenda* (uk:41), linasema:

*Yeye siye mwanagenzi, kila kila kitu atambuwa,*
*Kwa mizungu ni mjunzi, mhaba anayajuwa,*
*Raha itowayo chozi, ndio kwake nangunduwa*
*Kiitikio ,*
*Kupendwa nilichelewa,na wanaojua kupenda,*
*Wengi walinizinguwa, pendo walilivurunda. (Uk:3)*

Ubeti huu unazungumzia mwendo wa shairi katika kumburudisha, msomaji au msikilizaji huburudika kutokana uteuzi wa maneno unaokwenda na mwendo wa shairi ambao msomaji humvutiwa na maneno ya ubeti kama vile mahaba, mjuzi wa mapenzi hujiwa hisia na kuusoma kwa mwendo wa harakaharaka. Kuhusu kupendezeshwa kwa njia ya burudani mhojiwa Ame alisema kwamba mtunzi wa mashairi anapoamua kutunga shairi, kwanza hufanya uteuzi wa maneno yanayokwenda na wakati. Hali kadhalika yanayokwenda jamii anayoitungia ili kumfanya msomaji au msikilizaji kupata burudani ya kutosha. Ufafanuzi ni kwamba mwendo ni sehemu ya burudani kwa kuwa mashairi mengi yaliyotungwa kwa ajili ya burudani hutumia ya mwendo wa harakaharaka kutokana na matukio yake mengi huwa ya kufurahisha. Hivyo, waandishi wanapotunga kazi zao hutumia maudhui na lugha rahisi nyenye kutoa hisi za furaha ambazo humfikia msomaji au msikilizaji wa shairi. Kutokana na maelezo hayo mwendo wa shairi wa burudani mara nyingi huwa wa harakaharaka ili kukidhi haja ya wasikilizaji kupata taharuki na kuufikia ujumbe. Kwa mfano wa shairi lenye mahadhi ya mwendo wa harakaharaka linaonekana wazi katika diwani ya *Kimbunga* shairi la *Mpewa Hapokonyeki* linalosema:

*Aliyepewa kapewa, naapa hapokonyeki*
*Kwa alicho jaaliwa, wallahi hapokonyeki*
*Ukimlia ngowa, unjipatia dhiki*
*Mpewa hapokonyeki, aliyepewa kapewa*

*Mola ndiye atowae, akawapa mahuluki*
*Humpa amtakae, ambaye humbariki*
*Na kila amnyimae, kupata hatodiriki*
*Mpewa hapokonyeki, aliyepewa kapewa (uk: 35)*

Beti hizi mbili zinaonyesha mwendo wa harakaharaka kutokana na ushahidi wa maudhui na lugha nyepesi inayopelekea kufikisha ujumbe kwa kupitia burudani. Utaiti umebaini katika beti hizo kuwa mwendo unaoibuka ni wa harakaharaka hutoa burudani kwa asilimia kubwa. Kwa mfano beti hizo zinachambua msomaji au msikilizaji kwamba waache tamaa na kukinai wanachokipata na wasione choyo kwa mtu aliyepewa wakumbuke Mola ndiye mtoaji na kumpatia amtakae.

### 4.3.5 Mwendo Unampa Uhuru Mtunzi

Uhuru wa mtunzi ni uwezo wa mtu binafsi kujiendeshea mambo yake mwenyewe kujiitathmini kujijua na kufanya maamuzi ya busara nini afanye na nini asifanye (Kezilahabi, 1993). Siri kubwa ya uhuru wa mwandishi ni utashi yaani kujitolea na kuondosha hofu. Kiungo muhimu kinachompa sifa ya kuwa na uhuru wake ni lugha, na lugha ndio inayojenga mwendo wa shairi, hivyo, akiweza kuitumia vizuri bila woga kila kitu kitatengenea. Salma (khj) anathibitisha kwa kusema:

> Uhuru wa mtunzi huupata pale anapokuwa na uwezo wa kuamua katika kazi yake atumie aina gani ya mwendo. Mfano akitaka mwendo wa pole shairi lake ana uhuru kulifumba anavyotaka na kulifanya beti chache, kwa upande wa mwendo wa wastani au harakaharaka mtunzi basi ama huzifanya beti zake kuwa nyingi na tukio mara nyingi huwa moja.

Maelezo haya yanashadadia hoja hii kwa kumwezesha mtunzi kuifumba kazi yake kwa kutumia lugha ngumu na wingi wa taswira kwa lengo la kuibua mwendo wa polepole na anapoamua mwendo wa wastani na harakaharaka hutumia matukio ya kufurahisha kutumia kwa lugha nyepesi. Hoja hii inadhihirika kwa kuonyesha uhuru wa mtunzi kutunga anavyotaka. Kwa mfano katika diwani ya *Kimbunga* shairi la *Mnapata Kitu gani?* pale mtunzi alipowapa nasaha wavutaji sigara kwa kusema:

*Wavutaji wa sigara, nauliza nijibuni*
*Ni ipi yake tijara, mwapata faida gani*
*Nipeni jawabu bara, ambayo ya kuamini,*
*Ni ipi tijara yake, niambieni mvutao.*

*Sigara zapumbaza, wavutao duniani*
*Wengie zikawakohoza, kuwacha hawatamani*
*Japo zinawaumiza, hawajali hawaoni*
*Mnapata kitu gani, nambieni mvutao (uk:26 -27)*

Beti hizi zinaonyesha uhuru wa mtunzi kwa kutumia lugha kwa mujibu wa mwendo anaoutaka. Beti hizi zinonyesha mwendo wa harakaharaka kwa sababu mtunzi ana lengo la kutoa wosia kwa vijana wadogo wanaovuta au kujifundisha kuvuta sigara. Hivyo, ameutumia mwendo huo kwa mujibu wa uwezo wao wa kumfahamu na kupata ujumbe alioukusudia kwa njia ya swali *mnapata kitu gani?* Lengo hapa ni kufikisha ujumbe uliokusudiwa.

### 4.3.6 Kudhihirisha Matumizi ya Takriri

Takriri ni mbinu inayoshirikisha matumizi ya kurudiwa rudiwa kwa maneno, silabi, vina, herufi, au kipande cha mstari wa shairi, hali hii hufanya msomaji na msikilizaji wa shairi kuweza kuyafahamu maudhui ya shairi vizuri (Senkoro, 1988). Hii ina maana kwamba mara zote takriri ya neno au maneno humfanya msomaji na msikilizaji kuwa na uzingativu katika kukumbushwa, kusisitizwa na kuunganishwa mawazo ya kile alichokisoma katika beti zilizotangulia ili kifikia ujumbe. Takriri hudhihirishwa kwa kutumia mwendo wa shairi kwa mujibu wa maudhui na lugha aliyotumia mwandishi lakini mara nyingi huwa kwa mwendo wa harakaharaka. Kwa mfano katika diwani ya *Kimbunga* mtunzi amerudia shairi zima lenye beti 8 neno *kujitawala,* hivyo humfanya msomaji kuwa na mazoea nalo na kusoma kwa harakaharaka. Hoja hii inathibitika katika diwani ya *Kumbunga* shairi la *Kujitawala* linalosema:

*Kujitawala sikwema, kuliko kutawaliwa*
*Kujitawala ni umma, kila yao kuamua*
*Kijitawala si kama, ulanguzi na rushwav*

*Kujitawala khatamu, na umma kushikilia*
*Kujitawala hukumu, makosa kushitakiwa*
*Kujitawala si sumu, mara kwa mara kuuwa (uk:7)*

Beti hizi zinaonyesha kusomeka kwa mwendo wa harakaharaka, msomaji na msikilizaji tayari wamekwishalizoea neno *kujitawala*. Kwa upande mwingine takriri pia huweza kuonesha mwendo wa shairi wa wastani kulinga na maudhui ya dhuluma na kuonewa. Katika diwani ya *Wasakatonge* shairi la *Hatukubali* mwandishi ameonyosha takriri ya maneno ya takriri mstari mzima; maneno *hatukubali tena* kwa kila ubeti kati ya beti 6, na maneno mengine yamerudiwa rudiwa kila beti kuonyesha msisitizo wa huzuni ya kudhulumiwa na kuchoka kila beti ni *hatukubali tena.* Shairi linasema:

*Hatukubali tena,*
*Kuja tena lili kuonewa,*
*Kuja tena kudharauliwa,*
*Kuja tena na kutawaliwa,*
*Hatukubali katu,*
*Ndani ya nchi yetu,*
*Ilio huru (.uk:30)*

Ubeti unasomeka kwa mwendo wa wastani kwa sababu ni matukio ya huzuni ya kutawaliwa na wakoloni na lugha ilyotumika ni ya wastani kumfanya msomaji kupata ujumbe kirahisi, urahisi huu unatoka na kurudiwa kwa maneno kwa mfano *kuja tena*, *kuja tena* yamepelekea kupunguza ugumu wa shairi na kulifanya kuwa la mwendo wa wastani

### 4.3.7 Chanzo cha Kuibua Maudhui

Maudhui ni wazo ua mawazo ya mwandishi anayoyaweka katika kazi yake ambayo lengo lake ni kufikisha ujumbe kwa hadhira yake. Katika maudhui hayo ndimo mnamoibuliwa mwendo wa shairi. Aminia (khj) anasema:

> Maudhui ni uti wa mgongo wa kazi ya fasihi, mwandishi ili aweze kufikisha ujumbe lazima pawe na wazo la jumla nandani ya wazo ndimo mnamopatikana dhamira za mtunzi, ndani ya dhamira mnapatikana mwendo wa shairi wa kuifikisha hiyo dhamira kwa hadhira. Mtunzi wa mashairi hutumia mwendo unaokwenda sambamba na maudhui ili jamii inufaike na ujumbe anaotaka kuufikisha.

Maelezo haya yana maana kuwa, mtunzi wa shairi anapotumia mwendo wa shairi unaolingana na dhamira yake ni rahisi kwa mwendo kuyabainisha maudhui yatakayo wiana na mwendo huo. Nadhari ya upokezi inabainisha kuwa kazi ya fasihi itaibua

ujumbe kama anavyouchukulia hadhira. Kwa mfano dhamira yake inahusu mambo ya tanzia msomaji wa shairi hulisoma shairi kwa mwendo wa polepole kwa lengo kufahamu kile alichokusudia mwandishi kwa sababu maudhui ya tanzia yana lengo la kumfikirisha msomaji kutokana na hisi za majonzi zilizomo ndani ya shairi. Kwa hiyo mwendo wa polepole umeibua maudhui ya tanzia. Madai haya yanadhihirika kupitia diwani ya *Wasakatonge* katika shairi la *Kwa heri* linalosema:

*Ingawa umenuna, vishavu vyako kutuna,*
*Kunapambazuka, jua linatoka,*
*Bado kunakucha*
*Kwa heri*

*Ingawa mekasirika, na uso kusawijika*
*Zinavuma pepo hata kama hupo,*
*Kusi matlai,*
*Kwa heri*

*Ingawamenisusia, kujipa kunigomea*
*Mvua zanyesha, masika hukesha*
*Hakuna ukame*
*Kwa heri (uk:29)*

Beti hizi zinasomeka kwa mwendo wa polepole kutokana na ujumbe wa mwandishi kuonesha mapenzi ya upande mmoja, ambapo mtu mmoja kuwa na mapenzi na mwingine kumdharau mwenziwe. Hii inaonesha kwamba beti hizi zimeibua maudhui ya tanzia na kusababisha mwendo wa polepole kutokana na kuwapo kwa matukio ya dharau na kejeli ya mtu mmoja kudharau mtu mwingine. Hivyo maudhui humfanya msomaji kutumia mwendo wa polepole hasa kama hilo jambo limekuta au mtu wake wa karibu, hivyo utaratibu katika usomaji unahitajika ili kufikia ujumbe.

Hata hivyo, msomaji anapotumia mwendo wa harakaharaka bila shaka msikilizaji anaweza kugundua aina ya maudhui yaliyotumika ikiwa ni mepesi hupata ujumbe kwa urahisi au hata wakati mwingine kile kinachozungumzwa katika maudhui kikawa cha kufurahisha msikilizaji. Shairi huweza kuibua maudhui yaliyokusudiwa na mtunzi harakaharaka kutokana na jinsi mtunzi alivyoyaweka wazi maudhui kwa kupitia lugha iliyoitumia. Hoja hii inadhihirika katika diwani ya *Kimbunga* shairi la *Madereva:*

*Madereva nawambia, wawe nayo tahadhari*

*Mwendo wa kupindukia, ni kiini cha hatari*
*Waweze kuzingatia, kama silo jambo zuri*
*Mwendo uwe wa salama (uk:41)*

Katika ubeti huu unaonyesha lugha na maudhui ni mepesi na yenye kufahamika. Hivyo msomaji au msikilizaji huweza kupata ujumbe haraka kutokana na aina ya maudhui yaliyotumika hivyo, ujumbe hupatikana kwa urahisi bila ya kufikiri sana na kufanya mwendo wa shairi kuwa wa harakaharaka kwa sababu ya maudhui yaliyotumika katika ubeti huo.

### 4.3.8 Kuonyesha Upekee wa Mwandishi

Upekee ni utofauti wa vitu au watu kwa kuwa na sifa za pekee ambazo kitu au watu wingine hawana. Tasinifu hii imebaini kuwa, vipengele vilivyotumika kujenga mwendo katika ushairi husaidia zaidi katika kuwafanya watunzi kuwa wakipekee tofauti na watunzi wengine. Katika kushadadia hoja hii, Nadhra (khj) anasema kuwa:

> Mwandishi Gora Haji Gora ametumia maudhui yenye hali ya upole kwa kutoa wasia mfano *Vielezo*, *Usimpige mkeo*, *Hongera*, *Sivema*, *Ulezi kazi*, *Vijana wa Zanzibari*, *Dawa ya deni*, *Mpewa hapokonyeki*, *Sifa ya mke*, *Wasia* na mengi mengineyo.Hivyo kufanya mwendo wa harakaharaka.

Hii ilitokana na mambo kama jamii aliyoitungia ilikuwa ya watu wa kawaida, na wakati huo wa utunzi yake. Hivyo, alitumia nyepesi ambayo kwa asilimia kubwa inaeleweka kirahisi. Dai hili linalodhihirika kwa kupitia katika diwani ya *Kimbunga* Shairi la *Wasia* linalosema:

*Wasia wangu nakupa, mwanakwetu zingatiya*
*Siingilie kwa pupa, ina hatari duniya*
*Itakuja kukutupa, usipopakusudiya*
*Kaa kwa kuiyogopa, katu haina shujaa.(uk: 30)*

Ubeti huu unaonyesha uhalisia wa mtunzi Gora kuwa mashairi yake kwa silimia kubwa ni ya mwendo wa harakaharaka kutokana na misingi ya historia yake na yakijamii aliyoitungia. Wakati Mohammed Seif Khatib mashairi yake mengi yanakwenda na wakati, hivyo kifasihi anayafumba kulingana na uwezo wake wa elimu na hadhira aliyoikusudia. Mwandishi huyu mashairi yake mengi ameyatunga kwa kutumia taswira nzito kwa mfano mashairi ya *Vinyoga*, *Bundi*, *Miamba*, *Fahali la dunia*, *Buzi lisilochunika*, *Nahodha*, *Mtemea Mate Mbingu*, *Usikuwa kiza*, *Kansa*

*na mengineyo*. Haya ni miongoni mwa mashairi yanayoonesha mwendo wa polepole. Hivyo, msomaji inambidi kwanza afumbue fumbo ndipo afikie ujumbe. Nadharia ya Upokezi inalisisitiza hilo kwa kusema "… ili msomaji apate maana inambidi agundue mambo yaliyofumbwa na mtunzi…" (Fish, 1980). Endapo msomaji akitumia muda mkubwa kugundua mwandishi anataka nini, usomaji huu ni dhahiri ni wa mwendo wa polepole.

Khatibu kutokana na mashairi yake mengi yanayozungumzia siasa kwa kuyafumba kwa mwendo wa wastani bado yapo ya furaha yanayozungumza mapenzi ambayo yanadhihirisha kutumia mwendo wa harakaharaka. Katika kuthibitisha hoja hii tasinifu imebainisha shairi lenye mwendo wa polepole lililotungwa kwa fumbo na lenye kuhitaji jawabu katika diwani ya *Wasakatonge* shairi la *Asali ilipotoja* linalosema:

*Aina ya mizinga*
*Mingi tuliochonga*
*Mitini tukapanga*
*Nyuki wakatuzonga*
*Misumari kitunga*
*Tukavumilia*

*Mili ikatuvimba*
*Ila hatukuyumba*
*Tukabakia shamba*
*Kutumaini kwamba*
*Faida Itawamba*
*Heri itafika (uk:37)*

Beti hizi mbili zinaonesha upekee wa mwandishi Mohammed Seif Khatib, ambaye umahiri wake katika utunzi wa mashairi. Mashairi yake mengi amezungumzia siasa, hivyo, ufumbaji wa wastani ametumia. Kwa mfano matumizi lugha ya ishara ambayo inahitaji ufafanuzi wa kina ili kupata ujumbe. Hivyo, msomaji na msikilizaji hana budi kufanya tafakuri na kufanya shairi lisomeke kwa mwendo wa pole.

### 4.3.9 Mwendo kama Kipengele cha Kisanaa

Tasnifu hii imebaini kuwa mwendo katika ushairi hutumika kama kipengele cha kisanaa sawa na vipengele vingine vya kisanaa. Imebainika kuwa mara nyingi kipengele cha mwendo ni dhana ambayo bado haijafanyiwa tafiti za kina hasa katika

uga wa ushairi wa Kiswahili, hivyo kuonekana kama kitu kigeni. Salma (khj) anasema kuwa:

> Kipengele cha kisana kama kilivyo kipengele chengine cha kisanaa. Hii ni kutokana na kipengele cha mwendo wa shairi kuwa na dhima sawa na vipengele vingine vya fani. Dhima yake kubwa ya kipengele hiki ni kulifanya shairi kuwa namvuto zaidi na kwenda sambamba na maudhui ya kazi husika, na kwamba, mwendo humuongoza mtunzi kujua shairi lake anataka alitunge kwa kutumia kasi gani. Mfano, kama mtunzi anataka shairi liwe na mwendo wa harakaharaka kuna mambo ya kuzingatia kama lugha nyepesi, matukio ya furaha na kuzingatia aina ya hadhira anaowatungia na uwezo wao kifasihi.

Tasinifu hii imebainisha kuwa mwendo wa shairi unamuongezea uhuru mtunzi wa kutafakari ni mwendo gani atumie katika shairi lake na mambo gani ayazingatie ili kufikia lengo. Kwa, kupitia Nadharia ya Upokezi tumeweza kubaini kuwa uwezo wa hadhira katika kufikia ujumbe hupimwa kimawazo kati ya msomaji na wazo analolisoma (Fish, 1980). Hii ni kusema kuwa uwezo wa hadhira kama wazo litakuwa wazi atamudu kuichambua kazi ya fasihi kwa haraka na kupelekea mwendo wa harakaharaka. Hoja hii inaonekana katika shairi la *Kimbunga* katika diwani ya *Kimbunga*:

*Tumia sanaa yako, kwa juhudiulionayo*
*Kufunza jamii yako, wala usiwe na choyo*
*Kwani ni wajibu wako,sikia nikwambiayo*
*Lazima tujuwe hayo, ni yepi tunayotunga.(uk. 23-24)*

Ubeti huu unaonyesha dhima ya mwendo kama kipengele cha kisanaa kwa sababu mwandishi ametumia lugha nyepesi, tukio la kawaida la furaha na pia amezingatia aina ya hadhira kwa kuwa shairi linaweza kusomwa na kila mtu katika jamii.

### 4.3.10 Kujenga Uwezo wa kufikiri

Wahojiwa walihusisha dhana ya mwendo na kujenga uwezo wa kufikiri kwa msomaji na msikilizaji wa shairi. Walibainisha kuwa kazi ya fasihi zote zinahitaji ubingwa wa uandishi ambao utamfanya msomaji na msikilizaji apate tafakuri wakati wa usomaji na usikilizaji katika kusaka ujumbe. Bila ya kufikiri kazi hiyo itakuwa ina mapungufu. Katika kuweka wazi dai hili, Mberwa (khj) alisema:

> Katika kuwasilisha maudhui ya shairi, mtunzi hubuni maudhui ya mwendo wa shairi unaohitajika ili kumfikirisha msomaji na msikilizaji juu ya kile anachokisoma au kukisikiliza ilikupata ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Kwa mfano mwendo wa pole humfikirisha zaidi msomaji kutokana na kuambatana na lugha nzito, tanzia, matendo ya kutisha, taswira, wingi wa tamathali za semi na mengineyo.

Maelezo ya wahojiwa hawa yanaonesha kwamba ili ujumbe wa shairi upatikane msomaji au msikilizaji lazima afanye tafakuri ya kutosha, kitendo cha kufikiri kinapunguza kasi ya mwendo wa mashairi na kufanya mwendo wa polepole. Ukweli huu unadhihirika katika diwani ya *Wasakatonge s*hairi la *Nalitote* (uk:15) kama ifuatavyo:

*Nalitote, mbao tugawane,*
*Kwa vyovyote isivyowezekana,*
*Iwe pute*[17]*, mali tugawane,*
*Nalitote.*

*Nalitote, wimbi liwe ndani,*
*Nakisete, chombo mkondoni,*
*Tukifate, bila usukani,*
*Nalitote. (uk:15)*

Ili msomaji au msikilizaji apate ujumbe inambidi afanye tafakuri ya kutosha, hasa juu ya maana ya maneno kama *mkondoni*[18]*, kiyoyome*[19]*,mbao, usukani, wimbi* na *nalitote* kwa kuwa yanaonekana kubeba dhima muhimu katika kupatikana kwa ujumbe uliokusudiwa. Kazi ya kupata ujumbe kusudiwa kwa usahihi inaweza kuwa rahisi zaidi iwapo msomaji au msikilizaji ataelewa zaidi jamii iliyokusudiwa. Hata hivyo, Ame (khj) alidokeza kuwa:

> Katika kujenga tafakuri ya msomaji au msikilizaji wa shairi, suala la uteuzi wa maneno katika shairi ni jambo linalofaa kuzingatiwa na mtunzi kwa kuwa hubuni lugha namna kwa namna ili kupata neno litakalomridhi katika kazi yake. Neno gani atumie katika utunzi wake au alitumie vipi ili rahisi kufikisha ujumbe au asitumie neno hili kwani ujumbe wake utachelewa kufika kwa hadhira. Maamuzi haya ya mtunzi ndiyo yanayomfanya atumie maneno gani ambayo yatakwenda sambamba na mwendo wa shairi anaoutaka.

[17] Pute maana yake piga kumbo kitu, angusha
[18] Mkondoni maana yake njia ya maji ilioko baharini
[19] Kiyoyome maana yake kiangamie kiondoke duniani

Hii ina maana kwamba mwandishi anapokitumia kipengele cha mwendo wa shairi kitamsaidia katika kufanya uchaguzi wa maneno ya kutumia katika kazi yake. Mtunzi hupata nafasi ya kufikiri na kujiuliza atumia neno gani kwa mwendo ninaotumia ili ujumbe wake ufike kwa haraka kwa hadhira. Kwa mfano nikitumia neno hili ujumbe huenda usifike kwa haraka. Hoja hii inathibitika katika diwani ya *Wasakatonge,* shairi la *Kansa* kama ifuatavyo:

> *Jamii imeoza, imeoza yanuka,*
> *Uchafu wachomoza, wachomoza wafoka,*
> *Inatoa mafuza mafanza, yanamwagika*
> *Imetunga usaha, usaha usokwisha,*
> *yazidi karaha, karaha yatapisha,*
> *Yahatarisha siha siha inadhofika. (uk:4)*

Katika beti hizi neno *kansa* limetumika kuashiria uozo uliopo katika jamii kuhusu mmonyonyoko wa maadili unaopelekea kuibuka kwa maovu mengi yenye athari kwa jamii. Maovu hayo ni kama vile ulevi, uongozi mbaya, ubakaji na mengineyo.

### 4.3.11 Kuibua taharuki

Mbinu ya taharuki ni mbinu ya pekee katika kumchunga usomaji na msikilizaji wa shairi kubaini ujumbe wa shairi. Utafiti huu umebaini kuwa taharuki katika utafiti huu umebaini kuwa hamu inayomfanya msomaji au msikilizaji wa shairi kuwa na hamu ya kutaka kujua tukio elezwa linahusiana na nini na litaishiaje. Kwa kuongezea mawazo ya hapo juu mtaalamu Madumula (2009) anasema:

> Msanii aliyebobea katika sanaa ya utunzi ni yule anayeitunga kazi yake kwa kutumia ufundi wa kutumia tukio moja likaweza kusababisha tukio jingine ambalo humfanya msomaji kuwa na hamu ya kuendelea kusoma kwa lengo la kutaka kufahamu nini kitatokea mwisho wa tukio.

Hii ina maana kwamba taharuki hujengwa na tukio ambalo litamfanya msomaji au msikilazaji kuendelea na kusoma kwa haraka kufukuzia mwishoni mwa tukio. Matukio hayo humfanya msomaji kupata taharuki na kuibua mwendo ulitokana na taharuki. Taharuki hupatikana kwa wasomaji hasa wanaojua mwendo wa shairi ukoje yaani ujuzi wa kitaaluma na kwa wasikilizaji hupata kuusikiliza na kuufanyia kazi kwa makini ili kupata ujumbe uliokusudiwa.

Wapo wasomaji wa shairi ambao hawana habari na mwendo wa shairi lakini wanapata taharuki kupitia maudhui ya shairi wanalolisoma au kulisikiliza. Wakati mwingine taharuki wanaipata kwa kusikia sauti ya msomaji wa shairi humvuta na kumuweka karibu kwa lengo la kupata ujumbe. Kwa mfano katika diwani ya *Kimbunga* shairi la *Vielezeo* liantoa mwendo wa taharuki kama ifuatavyo:

*Ukimwi vielelezo, vyake vinoendeleza*
*Mtu hasa ni wa mwanzo, yule asojituliza*
*Hupata maambukizo, wengine kuwarukiza*
*Hiyo njia moja wapo, inosambaza ukimwi (uk: 3)*

Ubeti huuunaibua taharuki kwa msomaji taharuki inayopatikana hapa kwa kusikia au kusoma huu UKIMWI neno hili hurusha taharuki na kumfanya msomaji kusoma kwa mwendo wastani ili kupata nafasi uufikiria ugonjwa huu.

### 4.4 Athari chanya za Mwendo katika Ushairi wa Kiswahili

Athari chanya ni athari zinazopatikana katika mwendo wa shairi katika ushairi wa Kiswahili. Athari chanya za mwendo wa shairi hizo ni hizi zifuatazo:

#### 4.4.1 Kufikisha Ujumbe

Lengo kuu la kazi ya fasihi ni kufikisha ujumbe kwa hadhira. Ili ujumbe ufike lazima kuwe na muumano mzuri wa fani na maudhui ambavyo ni njia ya kufikia ujumbe aliokusudia mwandishi. Kwa ujumla wahojiwa wamebainisha kuwa mwendo hutoa mchango mkubwa katika kufikisha ujumbe kipitia mashairi. Mmoja wa wahojiwa hao aliweka wazi kuwa:

> “Mwendo wa polepole ndio unaoifanya hadhira kuufikia ujumbe ipasavyo na hivyo kupelekea lengo la fasihi kutimia…….”

Hata hivyo, mtafitiwa huyu alifafanua kuwa mwendo wa pole huambatana na mambo mengi kumpatia msomaji muda wa kuchambua kwa umakini mambo hayo. Aliendelea kusema kuwa:

> Faida ya mwendo wa pole ni kuwa na mambo mengi ambayo msomaji hupata muda wa kutosha kutafakari kila kitu kama vile lugha nzito au nyepesi, matukio ya kuogofya na kuhuzunisha, matumizi ya mafumbo na mengineyo.

Maelezo ya mtafitiwa huyu yanathibitisha kuwa msomaji au msikilizaji wa shairi anakosa muda wa kutosha wa kutafakari kwa kina mambo anuwai yanayotumiwa na mtunzi wa shairi ili kufikisha ujumbe kwa jamii anayokusudia iwapo mwendo wa pole haukutumika katika ujenzi wa shairi hilo. Hali hiyo inaweza kusababisha kupatikana kwa ujumbe ambao haukukusudiwa na mtunzi wa shairi na hivyo kuviza lengo la ushairi kwa jamii. Madai haya yanadhihirika wazi katika diwani ya *Wasakatonge* katika shairi la *Bundi* linalosema:

> *Jogoo la kwanza liliwika,*
> *Tuliolala tukaamuka,*
> *Tulizani kumepambazuka,*
>
> *Kaniki nyongani*
> *Panga mkononi,*
> *Ni kwenda shambani,*
> *Hakujacha (uk:43)*

Kupitia beti hizi inaonekana wazi kuwa kupatikana kwa ujumbe si jambo rahisi kutokana na kutumika kwa lugha isiyorahisi kwa kila mtu. Hii inatokana na maneno kama vile *jogoo, tuliolala, tuliamka, kaniki, panga* na *shambani* kutumika kimafumbo zaidi ya maana zao za kawaida na hivyo kuibua mwendo wa pole.

Kinyume na mtafitiwa huyu, mhojiwa mwingine pamoja na kuunga mkono imani kwamba mwendo ni nyenzo muhimu katika kufikisha ujumbe, yeye anadhani kwamba mwendo wa harakaharaka ndio njia bora ya kufikisha ujumbe kwa kuwa huwa unambatana na matumizi ya lugha nyepesi katika shairi ambayo ni rahisi kueleweka anasema:

> Mimi ninadhani kuwa mwendo ni silaha muhimu katika kufikisha ujumbe hasa pale ambapo mwendo wa haraka umetumika katika shairi kwa vile unarahisisha ujumbe kufika kwa walengwa bila mtu kuwa na taaluma kubwa ya ushairi ua lugha ya Kiswahili.

Jambo hili linadhihirika katika diwani ya *Kimbunga* katika shairi la *Sifa ya Mke* linalosema:

> *Awe kama malaika, mzuri kupindukiya*
> *Tabia zikipotoka, si vizuri kusogeya*
> *Utakuja fedheheka, tahsdhari nakwambiya*
> *Sura njema ni kipambo, sifaya mke tabia*

Ubeti huu unadhihirisha namna ambavyo mwendo katika ushairi unavyoweza kuathiri katika kufikisha ujumbe lengwa wa mtunzi. Mtunzi akitumia mwendo wa harakaharaka ni mwendo bora ingawa msomaji hapati muda wa kulitafakari shairi, ila wepesi wa lugha inayotumiwa humfanya kupata ujumbe kwa kina zaidi.

#### 4.4.1.1 Huleta Mvuto kwa Hadhira

Kwa kwaida msomaji au msikilizaji wa shairi huweza kuvutiwa na vionjo tofauti vinavyo jumuishwa katika utunzi wa shairi husika.Mtunzi huvitumia vionjo kama vile tamathali za semi, matumizi ya semi na mbinu nyingine za kisanaa.Sio tu kwa ajili ya kupamba kazi zao bali pia kuweza kuvuta hisia za wasomaji au wasikilizaji wa mashairi yao. Omar (khj) katika maelezo yake alidokeza kuwa:

> Katika kuwagawa hadhira wapo wanaopenda mwendo wa kasi na wapo wanaopenda mwendo wa polepole na kundi la mwisho wanaopenda mwendo wa wastani. Wakati mwengine burudani ya mvuto inaweza kupanda kutegemea kiwango cha mwendo wa shairi anaoutaka msomaji au msikilizaji.

Katika ufafanuzi wake, mhojiwa huyu alitoa mfano wa kundi la vijana kuwa mara nyingi hupendelea mwendo wa haraka kutoka katika mashairi ya mapenzi na siasa kwa sababu ujumbe wake hupatikana haraka kutokana na lugha nyepesi inayotumika katika mashairi hayo. Dai la mvuto wa mwendo tuliangalie katika diwani ya *Wasakatonge* shairi la *Nilikesha* linalosema:

Nilikesha,
Siyo kwa ngoma au shakawa
Siyo kwa ngoma amatakuwa

Ila kwa hamu na nyingi hawa
Ikawa hakupambazuki
Ni mtekwa wa huba zako (uk:23)

Muundo wa maneno katika ubeti huu na shairi zima umejengwa katika namna ambayo huivuta hadhira katika kusoma na kulifurahia. Kuvutiwa kwa hadhira kunatokana na wepesi wa maneno na namna ambavyo maneno yameundwa na kuumana kiufundi. Mvuto huo pia unatokana na kasi au mwendo katika usomaji wa shairi hili. Hivyo, kwa kiasi kikubwa hadhira hupata burudiko na tulizo la nafsi inapokutana na mashairi yenye hadhi hii.

#### 4.4.1.2 Kuleta Msisimko kwa Washairi

Sengo (1988) anaeleza kuwa ushairi wa Kiswahili uliimbwa kwa lengo la kutoa burudani na kuiliwaza jamii husika baada ya kazi zao za mchana kutwa kwa lengo kuleta msisimko na kuwaondoshea uchovu. Ushairi uliotumika awali kwa kiasi kikubwa ulikuwa katika fasihi simulizi, yaani fasihi ya awali ambayo ilikuwa haijaandikwa. Ushairi ulijidhihirisha kupitia nyimbo mbalimbali ambazo zilitumika katika kuchapuza kazi au kutoa burudani baada ya kazi. Mwendo wa nyimbo hizo za awali ulikuwa katika mwendo wa harakaharaka kwa kuwa, mwendo huo huwa na sifa ya kutoa burudani au kufanya hadhira ichangamke hasa wanapofanya kazi. Katika ushairi wa kipindi hiki, hadhira kwa kiasi kikubwa hupenda miondoko ambayo itaifanya ichangamke. Hoja hii inadhihirika kwa kupitia shairi la *Kazi* kutoka diwani ya *Wasakatonge* shairi linalosema

*Pesa huletwa na kazi, ni njia zipitiayo*
*Hupata matumizi, iwapo kazi hunayo*
*Pesa njaa hukuliza, uvivu ni amgamizo*
*Uwache uvivu wako*

*Mapema toka na jembe, ukalime mbiyo mbiyo*
*Ardhi ukaichimbe, panda mbegu ifaayo*
*Yailahi umuombe, akupe matarajio*
*Uwache uvivu wako. (uk:17-18).*

Beti hizi zinaleta msisimko kwa hadhira hasa wapenzi wa mshairi ambao wengi wanaupata msisimko kwa kupenda mahadhi tu ya shairi, wengine msisimko wao kama maliwazo kwa kazi za mchana kutwa. Hivyo msikilizaji husikiliza kwa mwendo wa harakaharaka kwani wasikilizaji hao kidogo wanaotafuta ujumbe wa shairi. Wataalamu wa ushairi wao wako kinyume na wapenzi wengi wa ushairi kimtazamo. Mhojiwa Daulat (khj) anasema:

> Washairi waliokomaa kifasihi mara nyingi hupenda mashairi ya mwendo wa polepole yaliyotungwa kwalugha nzito na yenye mafumbo. Hii ni kwa sababu kwao mashairi hayo hutoa msisimko wakati wa kuyachambua mpaka kufikia ujumbe kwani uwezo wao wa kitaaluma unawaruhusu kufanya hivyo.

Anashadidia kwa kusema kuwa wasomi hao na wataalamu huyaona mashairi yenye mwendo wa harakaharaka kuwa ni chapwa kwa kuwa wanayaona kuwa ni mashairi yenye msisimko mdogo wakati wa kutoa ujumbe kwa hadhira kutokana na uwezo

wa taaluma yao. Wasomi hawa hupenda mashairi yenye tafakuri nzito kama ya shairi linalofuata hapo chini. Dai linathibitika kwa kuongozwa na diwani ya *Kimbunga* katika shairi la *Vitendwili* linalosema:

> *Nasema kinaga naga, mengine sikilizeni*
> *Farasi kula mizoga, na kufukua mavani*
> *Kuna kijungu cha pwaga, bila ya moto jikoni*
> *Wateguzi tegueni, moja baada ya moja*
>
> *Kuna yalozidi mno, kuajabisha nyoyoni*
> *Pana wakonge watano, wanashindana kwa fani*
> *Wakata mawe kwa meno, na kujaza matumboni*
> *Wateguzi teguweni, moja baada ya moja*
>
> *Kigarawa cha ukumbi, kipakia watu ndani*
> *Wavuvi wa mkunumbi, idadi yao tisini*
> *Kinayakata mawimbi, meli zinazama chini*
> *Wateguzi tegueni moja baada ya moja (uk:13-14)*

Beti hizi zimetungwa kwa lugha ya mafumbo, kwa hinyo, mtaalamu wa kufumbua lugha za mafumbo hupata msisimko wa kufikiri na kufanya uchambuzi wa kina kutokana na taaluma yake, na kusababisha usomaji wa kuwa wa mwendo wa polepole. Hivyo washairi waliokomaa kifasihi humuona mtunzi kama ~~huyu~~ ndiye aliyekamilika kwa utunzi wa mashairi kwa kuwa huweza kuzichemsha akili zao wakati wa kuzichambua beti ilikufikia ujumbe.

Akiongozea mhojiwa tajwa hapo juu aliendelea kwa kueleza kuhusu mwendo wa wastani na wa harakaharaka kwa kusema:

> Kundi la washairi huwa ni mchanganiko wa baadhi ya wasomi na wapenzi wa mashairi, hawa mara nyingi hupenda mwendo wa harakaharaka au wa wastani. Kwa sababu msisimko wanaoupata kwao ni kama maliwazo na burudani hawana uchambuzi mkubwa wa kutafuta ujumbe na wakati mwingine hata hawazingatii ujumbe husika, wanachozingatia ni msisimko wa sauti ya msomaji na aina ya mahadhi tu.

Kinyume na mawazo ya mwendo wa polepole hadhira ilyokusudiwa hapa ni mchanganyiko ambao wapo wanaopenda mwendo wa wastani kulingana na uwezo wao wa kufikia ujumbe na pia wapo wenye uwezo hafifu kwa mwendo wa wastani ambao mapenzi yao makubwa ni kupata burudani ya mahadhi au sauti ya msomaji

kwa ajili ya kupata maliwazo wakati wa mapumziko yao. Madai yanadhihirika kwa kujumuisha makundi ya wanaopenda mwendo wa wastani na wa harakaharaka kutoka diwani ya *Wasakatonge* katika shairi la *Mcheza Hawi Kiwete* linalosema

> *Ngoma yataka matao, huchezwa kwa kudemka,*
> *Kwa maringo na pumbao, mwili wote kunyumbuka,*
> *Haichezwi kama bao, komwe zako kupangika,*
> *Mcheza hawi kiwete, ngoma yataka matao*
>
> *Ngoma hutaka madaha, ya bashasha na kucheka,*
> *Nyuso hubeba furaha, haiba kuongezeka,*
> *Na nyimbo za ufasaha, si kupayukapayuka,*
> *Mcheza hawi kewete, ngoma yataka matao.*

Beti hizi zinatowa changamoto wa mwendo wa wastani kwa kumtaka msomaji na msikilizaji kufumbua fumbo la kujua hii ni ngoma gani? Lakini kwa upande mwingine beti zinatoa burudani kwa msomaji na msikilizaji baada ya kuyasikia maneno kwa mfano *mwili wote kunyumbuka, madaha, maringo, bashasha, furaha na nyinmbo za ufasaha.* Haya humfanya msikilizaji kusahau machofu na kuzitafsiri beti kwa mwendo wa harakaharaka.

**4.4.1.3 Kuchochea kwa Ukuaji wa Lugha ya Kishairi**

Lugha ya kishairi ni lugha maalum inayojitofautisha na lugha ya nathari, utofauti huu unapelekea ukuaji wa lugha ya kishairi mara kwa mara. Mayoka (1993) anasema ushairi una hazina kubwa ya maneno kutokanana unyumbufu wa fani ya ushairi. Mtunzi amepewa uhuru wa kufupisha au kurefusha bila ya kukiuka misingi ya utunzi. Kutokana na maelezo hayo ni wazi kwamba kuongezeka kwa kipengele cha mwendo wa mashairi kitapelekea ukuwaji wa lugha baada ya watunzi kudhihirisha uteuzi wa maneno yanayowiana matumizi ya mwendo wa shairi. Katika kufanya mahojiano kuhusu ukuaji wa lugha, Ali (khj) alisema:

> Mtunzi wa mashairi ana uhuru mkubwa wa uteuzi wa maneno, katika uteuzi wake mtunzi inambidi ongeze kasi kutokana na kuibuka kwa kipengele cha mwendo ambacho ufanyaji kazi wake anahusisha matumizi ya lugha kwa kiasi kikubwa.

Maelezo haya yanaonesha kuwa, endapo watunzi wa mashairi watapokielewa vema kipengele cha mwendo bila shaka ongezeko la ukuaji wa lugha ya kishairi itaongozeka kutokana na ukweli kwamba kipengele cha mwendo kinajihusisha na

matumizi ya lugha kwa kiasi kikubwa katika kidhihirisha umuhimu wake katika shairi. Katika kuyaweka wazi maelezo haya tunayanganisha na diwani ya *Kimbunga* katika shairi la *Chui* linalosema:

*Karine zilizopita, tangu kuanza duniya*
*Epigwa vikali vita, ambavyo vyaendelea*
*Lakini utamkuta, viumbe awarukia*
*Huyo ndiye chuwi gani,*

*Haingiwi namabomu, hilo nawakataliya*
*Naataetakadamu, silaha kumpigiya*
*Hamuoni asilani, alivyo kushabihiya*
*Huyo ndiye chui gani. (uk: 42)*

Beti hizi zinashajihisha kwamba baada ya mwendo wa mashairi huzoeleka, watunzi wa mashairi huwa na ubunifu mkubwa wa uteuzi wa maneno. Hili limethibitika katika beti hizo mbili zimetungwa kwa ubingwa wa hali ya juu katika uteuzi wa maneno ambapo lugha ya mafumbo kumfumbia Chui asiekufa imetumika na kuibua mwendo wa polepole wa shairi.

### 4.4.2 Athari Hasi za Mwendo katika Ushairi wa Kiswahili katika Diwani Teule

Sehemu inayofuata inabainisha athari hasi za mwendo katika ushairi wa Kiswahili. Athari hizi ni changamoto ambazo zikifanyiwa kazi na zinaweza kuinua hadhi ya mwendo wa mashiri na ushairi kwa ujumla miongoni mwa athari hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:

#### 4.4.2.1 Taaluma Ndogo ya Mwendo kwa Hadhira ya Shairi

Taaluma ni kitu cha kwanza katika uelewa ujumbe wa shairi endapo taaluma hiyo ikiwa ndogo bila shaka uelewa utakuwa hafifu. Kwani swali la msingi katika shairi ni kumudu kulitafsiri na kupata ujumbe kama Masoud (khj) anavyosema:

> Wasomaji huenda asilimia kubwa hawana habari na mwendo wa shairi. Wanachokijua ni kusoma mashairi na kufurahi au kupata ujumbe tu, vilevile katika akili zao hawazingati suala la mwendo labda shairi hili lina mwendo gani au shairi hili lina mwendo gani hiyo hakuna. Wanaozingatia haya ni wasomi wachache na wale wanaosoma kwa lengo la kutafuta kitu fulani. Kwa maoni yangu siku ukiwambia kuna mwendo wa mashairi utawachanganya kwani anachokijua shairi hili linaonya, hili linaburudisha.

Mtafitiwa ana maana kwamba taaluma ya mwendo wa shairi bado haijaingia vichwani mwa wanamashairi. Hivyo, wanalolijua wao ni kusoma au kusikiliza ili kupata ujumbe. Mhojiwa akingozea katika uhaba wa taaluma ya mwendo anaona si kwa wasomaji na wasikilizaji lakini pia kwa waandishi wa mashairi kwa kueleza

> Waandishi wa fasihi si wengi wanayoijua taaluma ya mwendo wa mashairi kwa sababu waandishi hawa wamegawika katika makundi mawili kuna waandishi wa fasihi na waandishi wa Kiswahili. Hivyo watunzi wa fasihi hasa mashairi katika akili zao hawana kama kuna kitu kinachoitwa mwendo wa shairi lakini kwa mbali swali hili wanalolijua ni wahakiki wa mambo ya fasihi na pengine ni chanzo cha kuleta mtafaruku kwa waandishi.

Waandishi wa mashairi ni mhimili mzuri kati yao na hadhira anayoiandikia katika kuutafsiri na kuufahamu ujumbe ulioukusudia. Hivyo mwandishi anatakiwa kuwa na taaluma ya mwendo wa shairi ambayo itayomwezesha kufikisha ujumbe, bila kujua dhana ya mwendo wa shairi litawachosha hadhira yake.

#### 4.4.2.2 Msomaji Kuichosha Hadhira yake

Msomaji wakati mwingine huwa ndio dira ya kufikisha ujumbe kwa jamii. Msomaji wa shairi hubeba dhamana ya kuwafikishia ujumbe hadhira yake kwa kutumia mbinu mbalimbali. Endapo akishindwa kujua uwezo wa hadhira yake matokeo yake ni kuichosha kutokana na kuibebesha mwendo si mahala pake na kutofikiwa kwa ujumbe. Salma (khj) kuhusu hili anasema:

> Mwandishi kama imeitunga kazi yake kwa tukio la huzuni na lugha ngumu ya mafumbo msomaji wa shairi akaliwasilisha kwa mwendo wa harakaharaka, hapa inategemea aina ya hadhra ikiwa hadhira imepikika kifasihi uelewa utapatikana lakini kwa hali halisi si rahisi kwa hadhira iliyokubwa. Vile vile shairi likitungwa kwa lugha nyepesi au wastani kwa tukio la furaha, msomaji akiliwasilisha shairi kwa mwendo wa polepole mno bila shaka hadhira itachoka.

Hapa imebainika ipo haja ya wasomaji wa mashairi kuyasoma kwa mujibu wa mtiririkowa visa na kuzingatia ugumu au wepesi wa lugha wakati wa kusoma ilikwenda sambamba na anachokiwasilisha kwa mujibu wa mwendo husika, wasipofanya hivyo, hadhira iliyokubwa hukosa ujumbe. Madai haya yanadhihirika katika diwani ya *Wasakatonge*, katika shairi la *Pepo Bila Kifo,* shairi limefumbwa

lakini lugha inafahamika msomaji kama si mweledi atapoteza uelewa. Shairi linasema:

*Nataka niifikie pepo,*
*Nizipate raha zilipo,*
*Na kila kizuri kilichopo,*
*Nifaidike.*

*Niyanywe maziwa ya uzima,*
*Na maji baridi ya kisima,*
*Niuridhiye wangu mtima,*
*Niburudika*

*Nichote mito yenye asali,*
*Niyale matunda mbali mbali,*
*Na vyakula vilivyo anzali,*
*Niridhike (uk:24)*

Beti zinaeleza vipi ataifikia pepo bila ya kifo? Ni fumbo kwani hakuna pepo ya duniani yenye raha tupu. Hivyo msomaji atakapoziwasilisha beti hizi kwa mwendo wa harakaharaka hadhira inayowasilishiwa bila shaka watakosa kuzifahamu kutokana na kufumbwa kwa beti hizi na kuziachilia mbali na kukosa ujumbe.

#### 4.4.2.3 Kupoteza Taharuki kwa Wasikilizaji

Senkoro (2011) anasema taharuki hujengwa kwa kutumia taswira ambazo msanii huziwasilisha kwa hadhira kwa lengo la kufikisha ujumbe. Katika muktadha huu msomaji wa shairi ndiye anayebeba dhima kwa msikilizaji wake kumfikishia ujumbe. Endapo msomaji akishindwa kuiwasilisha kazi yakekama maudhui ya shairi kama yalivyokusudiwa atapoteza taharuki ambayo alitakiwa aijenge ndani ya akili za wasikilizaji wake. Mhojiwa Ali (khj) alisema

> Wasikilizaji mara zote huwa na shauku na hamu ya kile anachokiwasilisha msomaji kiwe na manufaa na mafuzo ili kupata mabadiliko. Kinyume chake ikiwa msikilizaji hakupata chochote katika kusikiliza kwake, kutokana ugumu wa kazi au msomaji kuisoma kazi kwa mwendo usiolingana na maudhui matokeo yake msikilizaji kupoteza taharuki.

Mhojiwa ana maana kwamba msomaji lazima awena ujuzi wa kujua wasikilizaji wake wana sifa gani na vipi awasilishe shairi vyinginevyo atawachosha kama atatumia mwendo usiolingana uwezo wao na maudhui husika, matokeo yake

kupoteza na kukosa hamu na kupelekea kukosa ujumbe. Kwa mfano mazingira ya uwasilishwaji wa mashairi anapowasilisha kazi kwa mwendo wa polepole mno na kazi hiyo ikiwa yenye kuonyesha misiba, mauwaji, masuala ya madhara ya shiriki na dhulma za waziwazi. Muasilishaji au msikilizaji ikiwa yamemkuta miongoni mwa maafa hayo tajwa hapo juu, na msomaji anasoma kwa mwendo wa taratibu mno matokeo yake ataongoza msiba na kupoteza hamu ya kuendelea kusoma. Vile vile mwendo wa shairi ukiwa harakaharaka mno bila shaka kuna mambo msomaji atayaruka au atayabania. Kwani, mambo hayo yakiwa yanamhusu msikilizaji ile hamu au shauku hupotea. Haya yanathibitika katika diwani ya *Wasakatonge* shairi la *Unyama linalosema:*

*Binaadamu mmiliki,*
*Anefuga majini,*
*Kuyatukia mashetani*
*Kuongea mizimuni*
*Na kuwazuru (uk: 47)*

Beti ni ya tanzia inaelezea unyama wa binadamu anaefugamajini ili adhura watu. Hivyo, msomaji akiisoma kwa mwendo wa polepole mno msikilizaji hisia zitamzidi hata kulia kupoteza taharuki ya kutaka kujua kinachoendelea mbele.

### 4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura imeanza na muhtasari wa vitabu teule vya *Wasakatoge* na *Kimbunga.* Sura imejumuishana uwasilishaji wa taarifa kwa kuongozwa na Nadharia ya Upokezi. Data zilizojadiliwa, kuchanganuliwa na kuwasilishwa data hizo zilitoka maktabani na uwandani. Mahojiano yalifanyika ipasavyo kati ya mtafiti na watafitiwa wake. Shughuli za udurusu wa maandiko umefanyika kwa kujumuisha vitabu, majarida mbalimbali, makala na tasnifu. Mjadala huu umeganywa katika sehemu tatu kuu kulingana na malengo ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza imebainisha vipengele vinavyojenga mwendo wa shairi katika ushairi Kiswahili. Sehemu ya pili imebainisha kwa uwazi dhima za mwendo wa shairi. Sehemu ya tatu imejadili na ubainisha tathmini ya athari zinazotokana na mwendo wa mashairi. Sehemu inayofuata ni hitimisho la tasnifu, maoni na mapendekezo ya tasinifu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura inafafanua muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Sehemu ya kwanza itawasilisha muhtasari wa tasnifu hii. Sehemu ya pili ni hitimisho na sehemu ya mwisho imewasilisha mapendekezo kwa munufaa ya tafiti zinazokuja.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti ulilenga kuchunguza mdhihiriko wa mwendo katika ushairi wa Kiswahili ambapo ushahidi wa mifano ulitolewa kupitia diwani teule za *Wasakatonge* na *Kimbunga*. Utafiti huu pia uliongozwa na malengo mahususi matatu. Malengo hayo ni: kubainisha vipengele vinavyojenga mwendo wa mashairi; kufafanua dhima ya vipengele vinavyojenga mwendo wa mashairi; na mwisho kutathmini athari za mwendo wa mashairi katika ushairi wa Kiswahili.

Sura ya kwanza inatoa mwelekeo wa tasnifu kwa kuanza na utangulizi, usuli wa tatizo, tamko la utafiti, historia ya waandishi wa diwani teule, malengo ya utafiti, masuali ya utafiti na manufaa ya utafiti. Sura ya pili inafafanua maandiko mbalimbali yanayokwenda sambamba na utafiti huu, mathalani maandiko yanayofafanua dhana ya mwendo ushairi wa Kiswahili na mwanya wa utafiti. Vilevile katika sura hii imeelezwa Nadharia ya Upokezi iliyotumika katika utafiti huu pamoja na mihimili yake.

Sura ya tatu inahusisha methodolojia ya utafiti iliyotumika katika utafiti huu. Sura hii imeeleza kwa kina namna ukusanyaji wa data na uchambuzi wake vilivyofanyika. Vipengele vilivyohusishwa katika kuikamilisha sura hii ni: usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, njia na zana za kukusanyia data, uchanganuzi wa data, itikeli ya utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, mawanda ya utafiti na mwisho tumeeleza kuhusiana na changamoto mbalimbali zilizoukumba utafiti huu pamoja na namna zilivyotatuliwa.

Sura ya nne imehusu mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Sura hii imegawika katika sehemu kuu tatu kulingana na malengo mahususi ya utafiti huu. Katika sehemu ya kwanza tumefafanua vipengele vinavyojenga mwendo katika

ushairi wa Kiswahili. Utafiti umebaini vipengele kadhaa vinavyojenga mwendo wa shairi kama vifuatavyo: lugha, muundo, vina, wizani, maudhui, uteuzi wa maneno, kiimbo, mandhari na wakati, lafudhi, taswira, kibwagizo na maghani. Sehemu ya pili imefafanua dhima zinazotokana na mwendo wa shairi kama kufikisha ujumbe wa mwandishi, kutia hamasa katika usomaji, kuibua hisia kwa wasomaji, kupendezesha mtu kusikiliza, kumpa uhuru mtunzi, kudhihirisha matumizi ya takriri, kujenga uwezo wa kufikiri, kuibua taharuki, kuibua maudhui, kuweka wazi nafasi ya mahadhi na kuonyesha upekee wa mwandishi. Sehemu ya tatu imejadili na kuweka wazi athari za mwendo katika ushairi wa Kiswahili. Athari hizi zimegawika katika sehemu mbili ambazo ni athari chanya na athari hasi.

Sura ya tano ni hitimisho la tasnifu hii na tumehitimisha kwa kufafanua mambo ya muhtasari wa tasnifu, utoshelevu wa Nadharia ya uchambuzi wa data za utafiti, matokeo ya utafiti, mchango mpya uliobainika katika utafiti huu pamoja na mapendekezo kwa tafiti za baadae.

**5.3 Hitimisho**

Sehemu hii inaelezea masuala ya utoshelevu wa Nadharia ambayo imetumika katika utafiti huu, mchango mpya na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

**5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika**

Katika kukamilisha utafiti huu, Nadharia iliyotumika ni ya Upokezi. Nadharia hii imetumika katika kuchambua data na kuendesha mjadala wa utafiti hadi tukapata matokeo mazuri ya utafiti huu. Nadharia ya Upokezi imetuongoza katika kuchunguza mdhihiriko wa mwendo katika ushairi wa Kiswahili mifano kutoka katika diwani teule za *Wasakatonge* na *Kimbunga*. Nadharia imetosheleza mihimili yake. Mihimili hiyo ni minne ambayo tumeitumia katika mchakato wa kuendeshea utafiti huu. Mihimili hiyo ni: Kwanza, kuchunguza msomaji vipi anaweza kupata maarifa yaliyomo ndani ya matini. Pili, msomaji aweze kupokea ujumbe kutoka ndani ya matini kwa usahihikama uliovyokusudiwa na mtunzi. Tatu, sifa ya fasihi ni kufumbwa hivyo msomaji inampasa kufumbua ili kupata ujumbe. Mwisho, nadharia hii imefanikisha kutumika katika kuchunguza mdhihiriko wa mwendo wa shairi katika ushairi wa Kiswahili. Mifano diwani za *Wasakatonge* na *Kimbunga*. Hii ni kutokana na mihimili yake kwenda sambamba na malengo ya utafiti huu na kuweza

kusaidia kubainisha namna ya kazi ya fasihi inavyotoa ujumbe na kuufikisha kwa hadhira Pia, ilisaidia katika kubainisha vigezo vinavyojuulisha ubora wa kazi ya fasihi.

### 5.3.2 Mchango Mpya wa Tasnifu Hii

Utafiti umeibua michango mipya kama ifuatayo:
Kwanza, kudhihirisha kuwepo kwa mwendo wa shairi katika ushairi wa Kiswahili, hii ni kutokana na kutowekwa wazi katika uga wa mashairi na hata ushairi wa Kiswahili. Hivyo mtafiti aliona ni bora kuuchunguza na kuudhihirisha kwa lengo la kuibua na kueneza taaluma inayoweza kuwasaidia watunzi wa mashairi, wasomaji, wahakiki, na wasikilizaji kufikia malengo yao kwa haraka.

Pili, kuonyesha tofauti ya wazi kati ya mwendo unaopatikana katika nathari na ule unaopatikana katika mashairi. Katika nathari mwendo huundwa na matukio ya tanzia au furaha na mipaka ya kiwakati na kijografia wakati katika ushairi mwendo huundwa kwa vipengele vingi ikiwemo matukio ya kitanzia au ya furaha, mipaka ya kiwakati, maghani, kiimbo, mahadhi, vina, wizani, muundo wa shairi, kibwagizo, uteuzi wa lugha (lugha ya mkato) na vinginevyo.

Tatu, msingi mkuu wa mwendo wa mashairi ni mahadhi. Imebainika kuwa mahadhi yanabeba dhima kubwa ya mwendo wa mashairi kutokana upekee ambao haupatikani katika nathari na tamthilia na kupatikana katika mashairi tu. Kwa mfano shairi moja linaweza kughaniwa na watu wawili tofauti kila mmoja atachukua aina ya mwendo wake kwa mujibu wa mahadhi.

### 5.3.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zinazokuja

Utafiti umejikita katika kuchunguza mwendo katika ushairi wa Kiswahili kwa kutumia mashairi kutoka diwani mbili teule. Hivyo, tafiti zinazokuja, tunapendekeza watafiti wengine kufanya tafiti zao kuhusiana na dhana ya mwendo katika tanzu nyingine za ushairi kama vile nyimbo, kaswida, tenzi na ngonjera. Pia, si vibaya kwa tafiti zijazo kuuchunguza mwendo kwa kupitia vipengele vya fani tu au vya maudhui tu na kuonesha namna unavyodhihirika.Vile vile, watafiti wajao wanaweza kuchunguza tofauti na uwiyano uliopo kati ya mwendo wa ushairi na mwendo wa riwaya au tamthilia na athari zake kimatumizi.

## MAREJELEO


Abdullatif, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. London: Oxord.

C.H**.** Holman, (1936). *A Handbook to Literature* New York: Odyssey Press,

Cresswell, J. (2012). *Qualititative Inquiry and Research Design*. Choosing among the fiveTradition (3rd ed) Thousand Oks CA: Sage Publication.

Edwin, M. (2006). *Swahili Poetry*. Nairobi: Kenyatta University Institute of Open Learning.

Fish, Stanley. (1980). *Is there a Text in this Class? The Authority of Interpretives Communities.* Cambridge: Harvard Univesity Press.

Haji, G.H. (1994). *Kimbunga*. Dar es Salaam: TUKI.

Ross, H. (1979). *The Structure of Verse*. New York: The ECCO Press.

Kezilahabi, (1975). *Ushairi wa Mapokeo na Wakati Ujao*. Dar es Salaam: East African Literature.

Kezilahabi, E. (1983). "*Uchambuzi katika Ushairi wa Kiswahili". Katika Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandsihi wa Kiswahili*. Kur. 145-165. Dar es Salaam.

Khatib, M. S. (2012). *Wasakatonge*. London: Oxford University Press.

Khatib, M. S. (2014). *Chanjo Matakwa ya Mwanamume katika Mwili wa Mwanamke*. Dar es Salaam: TATAKI.

Kothari, C. (2004). *Research Methodology and Techniques*. New Delhi: New International (P) Ltd.

Kothari, C. (2008). *Research Methodology and Techniques*. New Delhi: New International (P) Ltd.

Lineberger, (2016). *The Importance of Rhythm in Poetry*. Retrieved from https://study.com/academy/lesson/the-importance-of-rhythm-in-poetry.html umenukuliwa tarehe 21/2/2020.

Iser Wolfgang, (1974). *The Implied Reader*. Baltimore: Johns Hopkin University Press.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi*. *Nadharia Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company.

Njogu, K. & Chimerah, R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Autolitho Ltd.

Madumula, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publisher Limited.

Maitaria, J. N. (2016). "*Ushairi kama Chombo cha Kuhifadhi na Kuelimisha Jamii kuhusu Utamaduni:* Mfano wa Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali" katika *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja*. Nairobi: Moi University Press.

Masinde, E.W. (2007). *Ufundishaji wa Ushairi katika Shule za Upili na Vyuo*. Eldoret: Taaluma Publishers

Massamba, (1983). *Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili katika Makala ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili Fasihi.* Dar es Salaam.

Mayoka, (1993). "*Utangulizi"* katika Andanenga, A. S. *Diwani ya Ustadh Andanenga*. Ndanda Peramiho Ndanda: Benedictine Publication.

Momanyi & Maitaria (2013). *Dhima ya Kibwagizo katika Ushairi wa Kiswahili*. Nairobi: Moi University Press.

Msokile, (1998*). Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. East Afrika Educational Publisher.

Mulokozi, (2007). *Uangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Mulokozi & Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi & Sengo, T. S. Y. (1995). *History of Kiswahili Poetry AD 1000- 2000*. Dar es Salaam: TUKI.

Njogu, K. (1995). *Poetic Serialization*. Kiswahili Metapoeti on Prosodic Knots.

Njogu & Chimera, (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Omar, S. (2009). *Tanzania Hip hop Poetic as Popular Literature*. Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: (Haijachapishwa)

Patton, M. Q. (1990). *Qualitative Evaluationand Research Methods*. London: Sage Publication.

Raj, H. (2005). *Theory and Practice in Social Research*. Delhi India: Third revised edition Surjeet Publication.

Ross, H. (1979). *The Structure of Verse*. New York: The ECCO Press.

Shariff, I. N. (1988). *Tungo zetu, Msingi wa Mashairi na Tungo Nyenginezo*. New Jersey: The Red Sea Press.

Sengo, (1978). *"Utangulizi" katika Kandoro, S. A.* na *Ushahidi wa Mashairi ya Kiswahili na Lugha yake*. Dar es Salaam: Longman

Senkoro, F. E. (1988). *Ushairi Tahakiki*. Dar es Salaam: University Press.

Topan, F. (1975). *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*: O.U.P East Africa.

Tompkin, J. P. (1980). *Reader Response Criticim*. Baltimore Hohms: University Press.

Trochim, B. & Trochim, W. (2000). *The Research Method Knowledge* 3rd Edition. Belmont: Wardsworth Publishing Company.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Tumain, (2010). *https://mwalimuwakiswahili.co.tz ›* Umenukuliwa tarehe 16/8/2019.

Wafula, R. M. & Kamau, N. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomokenyatta Press.

Wanjala, F. S. (2015*). Mwingiliano Tanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embala na Mwakakogwa* (Tasinifu shahada ya Uzamivu), Shule ya Sayansi za Kijamii, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phonex Publisers Ltd.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, (2008). *Kanzi ya Fasihi, Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

## VIAMBATISHO

### A. Miongozo ya Usaili

**A.1 Muongozo wa Usaili kwa Wanafunzi na Wahadhiri Masuali Lengwa ni**

a) Je, unaelewa nini kuhusu mwendo katika ushairi wa Kiswahili?

b) Taja aina za mwendo zinazopatikana katika ushairi wa Kiswahili?

c) Eleza aina za mwendo na sifa zake?.

d) Je, ni vipengele vipi vinavyojenga mwendo katika ushairi wa Kiswahili?

e) Unadhani vipengele hivyo vinajenga mwendo kwa namna gani?

f) Je, dhima mwendo mwendo katika ushairi wa Kiswahili ni zipi?

h) Je, mwendo una athari gani katika utanzu wa ushairi?

i) Je, unadhani ni kwa namna gani mwendo huathiri uelewa wa hadhira ya ushairi?

**A.2 Mwongozo wa Mahojiano kwa Mtunzi**

1. Tafadhali ninakuomba tueleze historia yako kwa ufupi
2. Katika kazi zako za ushairi umegusia suala la mwendo wa mashairi?
3. Tunakuomba tueleze nini maana ya mwendo wa shairi na vipi umeutumia katika kazi yako?
4. Je, unahisi athari gani zinaweza kujitokeza katika ufahamu wa hadhira kupitia mwendo wa mashairi?

## B. TAARIFA ZA WATAFITIWA

| N.A | JINA LA MTAFITIWA | SHUGHULI | MAHALI PA MAHOJIANO | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Dr. Masoud N. Muhammed | Mhadhiri wa Chuo Kikuu (SUZA) | Nkuruma Tawi la (SUZA) | 30/06/2020 |
| 2 | Dr. Omar Salum Muhamed | Mhadhiri wa chuo Kikuu (SUZA) | Ofisini kwake Nkuruma | 13/07/2020 |
| 3 | Dr. Salma Omar Hamad | Mhadhiri na mratibu Chuo Kikuu Huria | Ofisini kwake Nkuruma | 03/07/2020 |
| 4 | Bi Daulat Abdalla Said | Mhadhiri na ni mwanafunzi wa Phd | Ofisini kwake Nkurumah | 30/06/2020. |
| 5 | Mr. Hassan Hija | Mhadhiri na mwanafunzi wa Phd | Ofisini kwake Nkurumah | 08/07/2020. |
| 6 | Mwalim Ali Mwalim | Mhadhiri wa (SUZA) | Ofisini kwake Nkurumah | 04/07/2020. |
| 7 | Abdi Ramadhani Mberwa | Mwanafunzi wa Phd | Ofisini kwao Vuga (SUZA) | 11/07/2020. |
| 8 | Bi Nadhra Haji Ussi | Mwalimu wa fasihi | Nyumbani kwake Magogoni | 14/07/2020. |
| 9 | Mhammed seif Khatib | Mhadhiri na mtunzi wa diwani teule ya *Wasakatonge* | Ofisini kwake Mombasa Zanzibar | 08/07/2020. |
| 10 | Bi Aminia Hassan Hamad | Mwalimu wa fasihi | Ofisini kwake M/ladu Zanzibar | 09/7/2020. |
| 11 | Ali Haji Hassan | Mwanafunzi wa Phd | Ofisini kwao Vug (SUZA) | 10/07/2020. |
| 12 | Ali Haji Gora | Mwakilishi wa mtunzi wa diwani ya *Kimbun* | Nyumbani kwake Bububu Ngalaw | 10/07/2020 |




Mtafitiwa kushoto Bw.Vuai S. Muya akifanya mahojiano na mtafiti katika ofisi yake huko Dunga Wilaya ya Kati Mkoa Kusini Unguja Julai 8, 2020



Mtafitiwa kushoto Mwalimu Ali Mwalimu akifanya mahojiano na mtafiti katika ofisi yake huko Nkurumah nje kidogo ya mji wa Zanzibar Julai 4, 2020




Mtafiti akifanya mahojiano na mtafitiwa Abdi Ramadhan Mberwa katika ofisi zao zilizoko huko Vuga Mjini Zanzibar Julai 11, 2020.

## C. VIBALI VYA KUFANYA UTAFITI

# CHUO KIKUU CHA DODOMA
## OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO

THE UNIVERSITY OF DODOMA
UDOM
Embracing Knowledge

P.O. BOX 259
DODOMA, TANZANIA TEL: +255 (0)26 2323001 NUKUSHI: +255 (0)26 2323001

**Kumb. Na. MA.84/261/02/44** **Tarehe: 6 Aprili, 2020**

Katibu Tawala
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
**Zanzibar**

**YAH: IDHINI YA KUFANYA UTAFITI**

Dhumuni la barua hii ni kumtambulisha ndugu **Vuai Pandu M** ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma mwenye nambari ya usajili **HD/UDOM/00073/T.2018**. Mwanafunzi wetu amefikia hatua ya kufanya utafiti kama sehemu ya mafunzo katika kozi (programu) husika.

Kwa mujibu wa waraka wa Serikali wenye Kumb: Na. MPEC/R/10/1 wa tarehe 4 Julai, 1980, Makamu Mkuu wa Chuo amepewa mamlaka ya kutoa idhini ya kufanya utafiti kwa watumishi na wanafunzi wa Chuo Kikuu kwa niaba ya Serikali na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Hivyo ninapenda kukuarifu kuwa nimetoa idhini ya utafiti kwa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

Aidha ninakuomba umpatie msaada wowote utakaohitaji kufikia malengo ya utafiti wake. Zaidi tunakuomba umruhusu mwanafunzi wetu kuonana na kuzungumza na wataalum wa fasihi, watunzi wa ushairi, wahadhiri, wanafunzi wa shahada ya pili (M.A) na ya tatu (Phd) na wadau wote muhimu kwa utafiti wake katika mkoa wako.

Mada ya utafiti wake ni ***"Mdhihiriko Wa Mwendo Katika Ushairi Wa Kiswahili: Mfano Wasakatonge Na Kimbunga"***

Kipindi cha utafiti wake ni kuanzia April hadi Julai, 2020 na utafanyika maeneo ya Dare s Salaam na Dodoma- atazungumza na wataalum wa fasihi, watunzi wa ushairi, wahadhiri na wanafunzi wa shahada ya pili (M.A) na ya tatu (Phd) wa Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA)na wadau mbalimbali katika mkoa wa Zanzibari kuhusiana na utafiti huo.

Kama kuna pingamizi lolote unaombwa kutushauri ipasavyo. Kwa taarifa zaidi usisite kuwasiliana nasi kupitia kurugenzi ya Utafiti, Machapisho, Ushauri na Ushirikiano wa Kitaasisi S. L. P. 251, Dodoma. Namba ya simu + (255) 262310301, Barua pepe:research@udom.ac.tz.

Wako katika ujenzi wa Taifa,

VICE CHANCELLOR
THE UNIVERSITY OF DODOMA
P. O. BOX 259
DODOMA, TANZANIA

Prof. Faustine K. Bee
**MAKAMU MKUU WA CHUO**

Scanned with CamScanner

**REVOLUTIONARY GOVERNMENT OF ZANZIBAR**

SECRETARY
ZANZIBAR RESEARCH COMMITTEE
P. O Box 239
Tel: 2230806
FAX: 2233788



**RESEARCH/FILMING PERMIT**
**(This Permit is only Applicable in Zanzibar for a duration specified)**

**SECTION**

| | |
|---|---|
| **Name:** | Pandu Mkombe Vuai |
| Sex | Male |
| Date and Place of Birth | 11/01/1974 |
| Nationality: | Tanzanian |
| Passport Number: | - |
| Date and Place of Issue | - |
| Date of arrival in Zanzibar | - |
| Expected date of departure | - |
| Duration of study | Six Month (6) |
| Research Tittles | Mdhihiriko wa Mwendo katika ushairi wa Kiswahili Mfano wasakat |
| Full address of Sponsor | |

| | |
|---|---|
| Name of the authorizing officer: | Abdalla M. Denge |
| **Signature and seal:** | |
| **Institution:** | Office of Chief Government Statistician |
| **Address:** | P. O Box 2321<br>Zanzibar. |
| **Date:** | **16/06/2020** |